# SHUJAA PWAYA KATIKA RIWAYA YA KIDHANAISHI: MFANO WA RIWAYA TEULE ZA EUPHRASE KEZILAHABI

**WESLEY ONGIGE ABAYA**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA SHULE YA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII KWA MINAJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

**JULAI, 2025**

**UNGAMO NA IDHINI**

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

Sahihi..                                        Tarehe.... 01/07/2025

Wesley Ongige Abaya

MAKI/2020/67007

**IDHINI**

Tasnifu hii imewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Mount Kenya kwa madhumuni ya kutahiniwa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili katika Kiswahili kwa idhini yangu kama msimamizi.

Dkt. Alex Umbima Kevogo.

Chuo Kikuu cha Garissa.

Sahihi                                        Tarehe: **31/6/2025**

## HATILINZI

Haki zote zimehifadhiwa, ripoti hii ni kazi yangu binafsi, hairuhusiwi kuibadili na kuiga kwa namna yeyote, kupiga chapa sehemu yeyote, kurudufu nakala, bila kwa idhini ya mwandishi au ruhusa ya Chuo Kikuu Cha Mount Kenya.

**Wesley Ongige© 2024**

# TABARUKU

Kwa mapenzi ya dhati natabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa: Joseph Abaya na Alice Nyaboke na wanangu wapendwa Aziel Amani na Dariel Kipchumba kwa ustahimilivu.

Mount Kenya University

## SHUKRANI

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai, afya na nafasi alionipa ya kusomea uzamili (M.A Kiswahili) hadi kumaliza mwaka wa 2025.

Shukrani zangu za pekee zimwendee msimamizi wangu wa utafiti huu Dkt. Alex Umbima Kevogo wa Idara ya Sanaa na Sayansi ya Jamii katika Chuo Kikuu Cha Garissa kwa kukubali kuwa msimamizi wangu, kuniongoza, kunishauri na kunishirikisha katika mijadala mbalimbali ya kitaaluma hadi kutamatisha utafiti huu, Mola amlipe kila la kheri na amlinde katika maisha yake.

Pia nashukuru familia yangu: Baba yangu Joseph Abaya Otiso, mama yangu Alice Nyaboke Abaya, marehemu dada yangu wa pekee Marcella Nyamoita na Venesa Biyaki (shemeji), kaka zangu Evans Atika, Dennis Amwoma, Joshua Stanton na Christopher Otiso kwa mchango mkubwa wa mawazo na kifedha walionipa. Vile vile, shukrani zangu za dhati ziwaendee watoto wangu wapendwa Aziel Amani na Dariel Kipchumba kwa uvumilivu wao wakati wa masomo yangu.

Isitoshe, napenda kuwashukuru marafiki zangu wa dhati: Francis Maina Macharia tuliyeajiriwa na pamoja katika shule ya upili ya wasichana Sacredheart Mwakiwiwi kwa kunielekeza na kunishauri kama ndugu wa pekee, Lydia Bwari, Marina na Josphine Napoya; aliyechukua jukumu la marehemu dadangu kuniongoza na kunipa ushauri wa kimawazo.

Shukrani zangu ziwaendee wahadhiri wangu wa idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Cha Mount Kenya kunielekeza na kunishauri katika masomo yangu. Mwisho napenda kuwashukuru wanafunzi wenzangu: Solom, Grace, Edith, Faith, Lazline, Judy, Josphine, Nancy, Winnie na Janet kwa kutiana moyo na kushauriana kipindi cha masomo.


Mount Kenya University

## IKISIRI

Kuwepo wa shujaa pwaya katika fasihi si jambo lililozuka hivi karibuni. Ushahidi wa kihistoria unabainisha kuwepo kwa shujaa pwaya katika tamthilia ya urasimi mkongwe wa Kiyunani. Utafiti huu ulichunguza usawiri wa shujaa pwaya katika riwaya teule za kidhanaishi za Kiswahili zilizotungwa na Euphrase Kezilahabi ambazo ni: *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja Wa Fujo* (1975) na *Rosa Mistika* (1971). Mtafiti alilenga kutathmini usawiri wa shujaa pwaya katika riwaya teule zilizochunguzwa. Aidha, utafiti uliazimia kuchunguza ujumbe muhimu unaowasilishwa kupitia kwa shujaa pwaya katika riwaya teule zilizochanganuliwa. Istitoshe, utafiti ulikusudia kutathmini dhima ya shujaa pwaya katika riwaya teule zilizochambuliwa. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Riwaya tatu zilizoshirikishwa katika utafiti huu ziliteuliwa kwa kuzingatia usampulishaji wa kimaksudi. Mtafiti alisoma kwa kina riwaya sita za Kezilahabi na kutumia kigezo cha kuwepo kwa shujaa pwaya kuchagua riwaya tatu zilizochanganuliwa katika utafiti huu. Mtafiti alichanganua riwaya teule zilizoshirikishwa katika utafiti huu akiongozwa na mihimili ya Nadharia ya Udhanaishi iliyoasisiwa na Soren Kiekergaard. Nadharia ya Udhanaishi hujishughulisha na hali ya maisha ya binadamu kwa mtazamo wa falsafa ya kidhanaishi. Swali muhimu katika nadharia hii huwa 'maisha nini?' Wadhanaishi hutafiti na kusaili kwa kina uwepo na hatima ya binadamu duniani. Mbinu ya utafiti iliyotumika katika utafiti huu ni ile ya utafiti wa maktabani. Data iliyokusanywa ni ya kithamano. Data ya kithamano ilichanganuliwa na kufasiriwa kwa kutoa maelezo kwa mujibu wa mihimili ya Nadharia ya Udhanaishi. Maelezo ya kiufafanuzi yalitolewa kuhusu mbinu zilizotumika kusawiri shujaa pwaya pamoja na dhima yake katika kuwasilisha ujumbe muhimu karika riwaya teule. Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa shujaa pwaya amesawiriwa kama aliye na fikra za kimapinduzi, mwasi wa nguzo za kimaadili katika jamii yake na aliyegubikwa na unyume. Baadhi ya ujumbe muhimu unaowasilishwa kupitia kwa shujaa pwaya unahusu malezi, uozo wa maadili, utamaushi, uhuru wa mtu binafsi na nafasi ya mwanamke katika jamii. Dhima kuu ya shujaa pwaya ni kutekeleza majukumu ya kimsingi yanayokuza vipengele vya fani na maudhui katika riwaya husika. Utafiti huu utakuwa na mchango hasa kwa upande wa kuendeleza mbinu za mtindo kwa waandishi chipukizi wanaokusudia kutunga fasihi ya kidhanaishi. Aidha, matokeo ya utafiti yanatoa mwanga kuhusu usawiri wa shujaa pwaya katika riwaya ya kidhanaishi.

Mount Kenya University

## ABSTRACT

The presence of the antihero in literature is not a recent phenomenon. Historical evidence indicates the existence of the antihero in ancient Greek drama. This study analyzed the portrayal of the antihero in selected Swahili novels of a philosophical nature written by Euphrase Kezilahabi, namely *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), and *Rosa Mistika* (1971). The researcher aimed to assess the depiction of the antihero in the selected novels under review. Additionally, the study sought to explore the key themes conveyed through the antihero in the selected novels analyzed. Furthermore, the study aimed to evaluate the role of the antihero in the selected novels examined. This was a library-based study. The three novels included in this study were selected based on purposive sampling method. The researcher reviewed six novels by Kezilahabi and used the criterion of having an antihero to select the three novels analyzed in this study. The researcher analyzed the selected novels in the study guided by the tenets of the Existentialist Theory, propounded by Søren Kierkegaard. Existentialism examines the nature of life and human existence from a philosophical perspective. The key question in this theory is: What is life? Existentialists examine and deeply investigate human existence and destiny in the world. The research method used in this study is that of a library-based study. The data collected is qualitative. The qualitative data was analyzed and interpreted through the lens of the Existentialist Theory. This study gives a detailed analysis of the literary techniques used by the author to portray the antihero and how they were employed to convey important themes in the selected novels. The findings of the study indicate that the antihero is portrayed as someone with revolutionary ideas, a rebel against moral pillars in society, and someone consumed by contradictions. Some of the key themes conveyed through the antihero address social issues with regard to child upbringing, moral decay, selfishness, individual freedom, and the role of women in society. The main role of the antihero is to enhance elements of style and develop major themes in the respective novels. This study will contribute to advancing narrative techniques used in existential literature for use by emerging creative writers intrested in writing philosophical works. Additionally, the study's findings will shed light on the portrayal of the antihero in philosophical novels.

Mount Kenya University

**YALIYOMO**


**UNGAMO NA IDHINI** ........ **Error! Bookmark not defined.**
**HATILINZI** ........ iv
**TABARUKU** ........ v
**SHUKRANI** ........ vi
**ABSTRACT** ........ viii
**YALIYOMO** ........ ix
**SURA YA KWANZA** ........ 13
**MSINGI WA UTAFITI** ........ 13
1.0 Utangulizi ........ 13
1.1 Usuli wa Mada ........ 13
1.2 Suala la Utafiti ........ 16
1.3 Malengo ya Utafiti ........ 16
1.4 Maswali ya Utafiti ........ 17
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ya Utafiti ........ 17
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........ 18
1.7 Umuhimu wa Utafiti ........ 19
1.8 Maelezo ya Istilahi Muhimu ........ 20
**SURA YA PILI** ........ 21
**MAPITIO YA MAANDISHI** ........ 21
2.1 Utangulizi ........ 21
2.2 Usawiri wa Shujaa Pwaya katika kazi za Fasihi ........ 21
2.3. Umuhimu wa Shujaa Pwaya katika usawiri wa Mandhari ya Kazi za Fasihi ........ 22
2.4 Nafasi ya Shujaa Pwaya katika Usawiri wa Maudhui ........ 22
2.5. Misingi ya Nadharia ........ 24
2.5.1 Nadharia ya Udhanaishi ........ 24
2.5.2 Mihimili ya Nadharia ya Udhanaishi ........ 26
2.6 Hitimisho ........ 26
**SURA YA TATU** ........ 27
**MBINU ZA UTAFITI** ........ 27
3.0 Utangulizi ........ 27


Mount Kenya University

3.1 Eneo la Utafiti ........ 27
3.2 Muundo wa Utafiti ........ 27
3.3 Uteuzi wa Sampuli ........ 28
3.4 Vifaa vya Utafiti ........ 28
3.5 Uhalali wa Vifaa vya Utafiti ........ 28
3.6 Kutegemewa kwa Vifaa vya Utafiti ........ 28
3.7 Mbinu za Ukusanyaji Data ........ 29
3.8 Mbinu za Uchanganuzi wa Data ........ 29
3.9 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti ........ 29
3.10 Maadili yanayohusu Mtafiti ........ 29
3.10.1 Maadili kuhusu Waandishi wa Kazi za Fasihi ........ 30
3.10.2 Maadili Kuhusu Mchakato wa Utafiti ........ 30
3.11 Hitimisho ........ 30
**SURA YA NNE** ........ 31
**UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO YA UTAFITI** .... **31**
4.1 Utangulizi ........ 31
4.2 Historia fupi ya Euphrse Kezilahabi ........ 31
4.2.1 Muhtasari wa *Dunia Uwanja Wa Fujo* (1975) ........ 32
4.2.2 Muhtasari Wa Kichwamaji (1974) ........ 34
4.2.3 Muhtasari wa *Riwaya ya Rosa Mistika* (1971) ........ 35
4.3 Usawiri wa Shujaa Pwaya Katika Riwaya za *Rosa Mistika*, *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Kichwamaji* ........ 37
4.3.1 Shujaa Pwaya kama Mwasi wa Misingi ya Kimaadili na ya Kitamaduni iliyowekwa na kuthaminiwa na Jamii yake ........ 38
4.3.2 Shujaa Pwaya anatilia shaka na Kushuku Taasisi na Amali za Kijamii ........ 41
4.3.3 Shujaa pwaya kama Mwanaharakati mwenye Fikra za Kimapinduzi zinazobomoa Nguzo na Mifumo ya Kimapokeo ........ 43
4.3.4 Shujaa Pwaya anakubali Kifo kama Sehemu ya Maisha ........ 44
4.3.5 Shujaa Pwaya kama Kiumbe Dhaifu asiye na Uwezo wa Kuzikabili Changamoto za Maisha ........ 46
4.3.6 Shujaa Pwaya anasitasita Kufanya Uamuzi kuhusu Masuala ya Kimsingi Maishani .. 47
4.3.7 Mfuasi wa Mkondo wa Mawazo unaotafuta Ukweli kwa Undani ........ 49
4.3.8 Kiumbe aliyegubikwa na Unyume na Kinaya ........ 50

4.3.9 Shujaa Pwaya amesawiriwa kama Mtu anayefunga Safari ya Ndani ya Kujitambua .. 52
4.3.10 Mtu anayeelea katika Wimbi la Maisha bila Ridhaa wala Hiari ya Kibinafsi ........... 54
4.4 Ujumbe Muhimu unaowasilishwa na Shujaa Pwaya Katika Riwaya za *Dunia Uwanja wa Fujo, Rosa Mistika* na *Kichwamaji*........................................................................... 55
4.4.1 Misingi ya Malezi na Mandhari ya Ulezi wa Mtoto................................................... 57
4.4.2 Usherati, Uzinifu na Ufasaki ....................................................................................... 60
4.4.3 Elimu ya Kisasa Vyuoni na Elimu ya Kimapokeo katika Jamii.................................. 62
4.4.4 Mauti na Tanzia kama Sehemu ya Maisha .................................................................. 64
4.4.5 Tamaa, Ubinafsi na Uhuru wa Mtu Binafsi................................................................. 66
4.4.6 Utamaushi .................................................................................................................... 68
4.4.7 Migogoro, Mafarakano na Ukinzani katika Jamii ....................................................... 71
4.4.8 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii.............................................................................. 74
4.4.9 Ndoa kama Uwanja wa Fujo ....................................................................................... 76
4.4.10 Mwachano, Uhusiano na Utangamano baina ya Vizazi ............................................ 78
4.4.11 Ulevi na Anasa........................................................................................................... 80
4.4.12 Ushirikina na Uchawi ................................................................................................ 83
4.4.13 Mauaji na Ukatili ....................................................................................................... 84
4.4.14 Utamaduni wa Kiafrika na Athari za Kigeni katika Jamii......................................... 86
4.4.15 Unafiki ....................................................................................................................... 88
4.5 Dhima ya Shujaa Pwaya katika Riwaya za Rosa Mistika, Dunia Uwanja wa Fujo na Kichwamaji................................................................................................................... 89
4.5.1. Dhima ya Shujaa pwaya katika Kuimarisha Ujumi na Umbuji wa Kazi ya Fasihi..... 90
4.5.2 Shujaa Pwaya Kama Mhusika Mkuu na Mwimo wa Msuko wa Riwaya .................... 92
4.5.3 Nafasi ya Shujaa Pwaya katika Kukuza Sifa, Hulka na Wasifu wa Wahusika Wengine ....................................................................................................................... 93
4.5.4 Shujaa Pwaya katika Kuonyesha Uchangamano wa Jamii ya Kisasa .......................... 98
4.5.5 Dhima ya Shujaa Pwaya katika Usawiri wa Mandhari katika riwaya.......................... 99
4.6 Hitimisho ..................................................................................................................... 102
**SURA YA TANO** ....................................................................................................... 104
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**..................................................... 104
5.0 Utangulizi .................................................................................................................... 104
5.1 Muhtasari ..................................................................................................................... 104
5.2 Hitimisho la Matokeo Muhimu .................................................................................... 105

5.3 Mapendekezo ya Utafiti ..... 106
5.4 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi ..... 107
**MAREJELEO** ..... 108
**KIAMBATISHO I: BARUA YA IDHINI KUTIKA KWA KAMATI YA MAADILI** ..... 111
**KIAMBATISHO II: KIBALI CHA UTAFITI KUTOKA NACOSTI** ..... 112

Mount Kenya University

# SURA YA KWANZA

# MSINGI WA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alifafanua usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vilevile mtafiti aliangazia sababu za kuchagua mada hii, umuhimu wa utafiti huu, upeo na mipaka ya utafiti wake pamoja na maelezo ya istilahi maalumu zilizotumika kwenye utafiti.

## 1.1 Usuli wa Mada

Kuwepo wa shujaa pwaya katika fasihi si jambo lililozuka hivi karibuni. Ushahidi wa kihistoria unabainisha kuwepo kwa shujaa pwaya katika tamthilia ya urasimi mkongwe wa Kiyunani. Shujaa pwaya wa awali ni *Thersites* anayesawiriwa katika 'Utendi wa Iliad' uliotungwa na Homer. Isitoshe, shujaa pwaya amesawiriwa katika tashtiti ya Rumi pamoja na kazi nyingenezo za mvuvumko wa fasihi kwa mfano riwaya ya *Don Quixote* iliyotungwa na Miguel de Cervantes. Hata hivyo, istilahi 'shujaa pwaya' kwa maana hiyohiyo ilitumiwa kwa mara ya kwanza mnamo 1805 katika simulizi ya kidayolojia inayojulika kama '*Rameus Nephew*' (Mpwa wa Rameus) ya Denis Diderot (Brombert, 1999).

Ulimbwende wa kifasihi katika karne ya 19 ulisaidia kumfanya shujaa pwaya awe mhusika maarufu katika kazi za fasihi. Katika kipindi hiki, shujaa pwaya amesawiriwa kama mhusika mkuu katika kazi za fasihi zilizotungwa wakati huo. Miongoni mwazo ni riwaya ya kidhanaishi ya Fyodor Dostoyevsky iitwayo '*Notes from the Underground*' (Nyaraka za Siri). Katika karne ya kumi na tisa, usawiri wa shujaa pwaya katika kazi za fasihi uliimarika. Shujaa pwaya wa wakati huo alikuwa jaribosi anayesigana kihulka na kikale cha shujaa wa kimapokeo katika fasihi (Campbell, 1949).

Katika karne ya ishirini na moja shujaa pwaya alipata umaarufu katika kazi za fasihi zilizotungwa na waandishi waliokumbatia falsafa ya kidhanaishi. Miongoni mwa waandishi hao ni Franz Kafka aliyetunga riwaya ya '*The Metamorphosis*' (Mageuzi) mnamo 1915. Wengine ni Jean-Paul Satre

aliyetunga riwaya ya '*La Nausee*' (Kinyaa) mnano 1938 na Albert Camus aliyeandika riwaya ya '*The Stranger*' (Mgeni) mwaka 1942. Mhusika mkuu katika riwaya hizo ni shujaa pwaya anayesuasua kufanya uamuzi kuhusu masuala muhimu ya kimaisha yanayomkabili. Mhusika huyo anaelea maishani na kuyumbishwa na nguvu za majaliwa asizoweza kuzikabili. Isitoshe, maisha ya mhusika huyo yamejaa ukiwa, fadhaa na ukengeushi (Brombert, 1999).

Waandishi wa riwaya za awali za kimagharibi waliathiri kuzuka kwa riwaya ya kidhanaishi ya Kiswahili ikiongozwa na mwandishi maarufu Euphrase Kezilahabi. Athari hizo zinaonekana hasa Kezilahabi anavyowasawiri wasomi, viongozi wa dini, wanasiasa na watawala serikalini. Hawa ni mashujaa wanaoheshimiwa na kuenziwa na jamii zao. Viongozi hawa wanategemewa kuleta mabadiliko chanya katika jamii zao. Hata hivyo, Kezilahabi anawasawiri kama wanajamii wa kawaida waokabiliwa na changamoto za kimaisha zinazowakumba wananchi wa tabaka la chini licha ya kuwa na hadhi, vyeo na mamlaka katika jamii zao.

Polyzogopoulou (2021) anaeleza kuwa shujaa pwaya ni dhana iliyochipuzwa kutoka katika lugha ya Kigiriki ambapo dhana 'pwaya' inamaanisha 'pinga' na dhana ya 'shujaa' inamaanisha 'bingwa.' Kwa kifupi shujaa pwaya ni mpinzani wa matendo ya shujaa wa kitamaduni. Shujaa pwaya amekuwepo kutoka enzi za zamani za maigizo ya Kigiriki ya karne ya kumi na saba. Kwa upande wao, Janicke na Raney (2015) wanaeleza kuwa shujaa pwaya huwa mhusika mwenye pingamizi katika matendo yake ambayo mara nyingi hayarithishi. Allion na Smith (2015) wanaeleza dhana ya shujaa pwaya kuwa ni mpinzani aliyeanza katika masimulizi akiwa na tabia iliyoleta utata kati ya uzuri na uovu na pia wakati masimulizi yanatamatika. Kuna haja ya kufanya utafiti wa dharura kuonyesha dhima ya shujaa pwaya katika fasihi ili kubainisha iwapo ana umuhimu wowote.

Udhanaishi ni mtazamo ambao hukagua kwa upembuzi hali ya nafasi ya binadamu katika ulimwengu anamoishi; vilevile ni falsafa inayozungumzia uhusiano uliopo kati ya binadamu na Mungu na iwapo binadamu anapaswa kuamini kuwepo kwa Mola. Nadharia ya udhanaishi hujikita sana na hali ya maisha

ambapo swali lake kuu huwa maisha ni nini? Wadhanaishi hutafiti kwa kina usawiri wa mwanadamu duniani, pia hukita sana na utafiti unaohusiana na husiano kati ya mtu na Mola (Chimera na Njogu, 1999). Udhanaishi huwa ni hali inayotumiwa kufafanua mtazamo unaohusiana na jukumu na nafasi ya binadamu duniani. Wanjala (2012) anaeleza kuwa udhanaishi ni falsafa au mtazamo wa maisha ulio na shina lake katika swali kuwa, maisha ni nini na yana maana gani kwa binadamu? Kwa njia gani mwanadamu anaweza kuyabadilisha maisha yake yaliyojaa shida, mashaka na huzuni? Kezilahabi ametunga riwaya zinazozingatia falsafa ya kidhanaishi.

Euphrase Kezilahabi ni mwandishi mashuhuri, mshairi na msomi kutoka Tanzania. Kezilahabi alizaliwa kule Ukerewe tarehe 13 mwezi Aprili mwaka 1944 na akaaga dunia tarehe 9 mwezi Januari mwaka 2020. Hadi wakati wa kifo chake alikuwa anafundisha katika Chuo Kikuu cha Botswana. Riwaya yake ya kwanza ni *Rosa Mistika* (1970). Riwaya hii ilifuatwa na Diwani ya *Kichomi* (1973), *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), *Gamba la Nyoka* (1979), *Nagona* (1987), *Karibu Ndani* (1989), *Mzingile* (1993), *Kaptula la Marx* (1996) na *Dhifa* (2008). Baadhi ya hadithi fupi alizozitunga ni *Mayai Waziri wa Maradhi* (1992), *Magwanda Kubilya na Vyama Vingi* (1992), *Cha Mnyonge Utakitapika Hadharani* (1992) na *Wasubiri Kifo* (1992). Kezilahabi ni mkakiki wa jamii anayejiuliza maswali kuhusu kila kipengele cha maisha kuanzia miundo ya jamii ya kitamaduni, dini, elimu ya kimagharibi, siasa hadi falsafa. Isitoshe, Kezilahabi ni mwazaji anayeihakiki kila sehemu ya maisha ya jamii kwa uhalisi unaoshangaza. Mwandishi huyu ni bingwa anayesawiri dhamira zake akizingatia mkabala wa kidhanaishi unaoweka wazi kero na mitanziko ya wanyonge katika jamii yake. Mhusika wake maarufu ni shujaa pwaya ambaye mara nyingi ni msomi wa tabaka la kati anayejikuta kwenye njia panda. Mhusika huyu anakumbwa na hali mbili zinazomtatiza: ajiamini binafsi na kufuata mkondo wake binafsi wa fikra au afuate jamii inayomtegemea atoe uongozi na kuibadilisha (Madumula, 2007). Hatamiye hulemewa na mzigo wa kufanya uamuzi wa busara kisha hukimbilia kwenye mzingile wa nafsi yake na kuyamaliza

maisha yake anapojiua. Mhusika huyu haoni maana ya maisha, amekengeuka na kukata tamaa. Kuna haja ya kuchunguza mhusika huyu kwa kina ili kuelewa usawiri wake katika riwaya za Kezilahabi.

**1.2 Suala la Utafiti**

Jamii ya kisasa ni changamano kiasi cha kwamba mitindo ya maisha inabadilika kila siku. Uchangamano wa kimaisha huonekana pia katika usawiri wa wahusika katika kazi za fasihi. Wasomaji wa kazi za fasihi hujinasibisha na mhusika mkuu aliye shujaa au nguli ambaye wanamwona kama kielelezo cha kuigwa. Kwa kumsawiri shujaa pwaya kama mwasi, Kezilahabi anabisha mazoea ya kumsawiri shujaa kwa misingi chanya inayomwonyesha kuwa kielelezo cha uadilifu. Kezilahabi anabisha mtazamo wa kujenga jamii mpya kupitia wahusika wema pekee. Shujaa pwaya anakiuka misingi ya kimaadili na ya kitamaduni iliyowekwa na kuthaminiwa na jamii yake. Shujaa pwaya anatilia shaka taasisi za kijamii zilizojengeka katika imani na maadili ya kitamaduni. Uhakiki wa wahusika katika fasihi ya Kiswahili umejikita zaidi katika mkabala wa kisosholojia. Utafiti huu umezingatia mkabala wa uchunguzi wa kisaikolojia ambao haujazingatiwa kwa kina na wahakiki. Utafiti wa aina hii umetuwezesha kubaini ruwaza za mienendo na tabia za wahusika zinazojenga hulka zao zinazofuma visa vinavyosimulia maisha ya wahusika hao. Kuna haja kufanya utafiti wa dharura ili kuelewa vichocheo vya kisaikolojia na kifalsafa vinavyowaongoza wahusika wanaosawiriwa kutenda wanavyotenda na kusaili jinsi matendo na tabia zao zinavyochangia kujenga mwonoulimwengu wao. Utafiti huu umechunguza usawiri wa shujaa pwaya katika riwaya tatu za Euphrase Kezilahabi kwa jicho la kisaikolojia na falsafa ya kidhanaishi. Riwaya ambazo zimechunguzwa ni *Dunia Uwanja wa Fujo (2007)*, *Rosa Mistika (1971)* na *Kichwamaji (1974).*

**1.3 Malengo ya Utafiti**

Malengo yafuatayo yalioongoza utafiti huu**:**

i. Kutathmini usawiri wa shujaa pwaya katika riwaya teule za: *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Rosa Mistika* na *Kichwamaji.*

ii. Kuchunguza ujumbe muhimu unaowasilishwa kupitia kwa shujaa pwaya katika riwaya teule za: *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Rosa Mistika* na *Kichwamaji.*

iii. Kutathmini dhima ya shujaa pwaya katika riwaya za: *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Rosa Mistika* na *Kichwamaji.*

**1.4 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu ulijibu maswali yafuatayo:

i. Je, shujaa pwaya anasawiriwa vipi katika riwaya teule za *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Rosa Mistika* na *Kichwamaji*?

ii. Je, ni ujumbe gani muhimu unaowasilishwa kupitia kwa shujaa pwaya katika riwaya teule za *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Rosa Mistika* na *Kichwamaji*?

iii. Je, dhima ya shujaa pwaya ni ipi katika riwaya teule za *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Rosa Mistika* na *Kichwamaji*?

**1.5 Sababu za Kuchagua Mada ya Utafiti**

Mshawasha wa kuchagua mada hii unatokana na hoja kuwa utanzu wa riwaya umeanza kushughulikiwa katika ngazi za kitaaluma. Fasihi andishi imepewa nafsi kubwa, kwa hivyo kuna haja kuhakiki tanzu za fasihi andishi ambazo ni; riwaya, ambayo imezingatiwa katika utafiti huu, hadithi fupi na tamthilia. Riwaya ambayo ni utanzu umekuwa ukishughulikiwa na watafiti wengi na wandishi.

Mtindo ni kipengele muhimu cha fasihi ambacho hutusaidia kuelewa vyema zaidi kazi ya fasihi. Kwa kutumia shujaa pwaya, mwandishi anatumia mtindo wa kipekee unaobainisha kazi yake. Shujaa pwaya ni sehemu ya mtindo unaohusu mhusika na uhusika wake. Watafiti wameshughulikia suala la shujaa kwa jumla lakini hawajatafiti kwa kina suala la shujaa pwaya. Kwa hivyo, kutafiti na kuchanganua mhusika huyo kutafanya kuelewa kwa kina umuhimu wa kutumia shujaa katika kusuka kazi za kifasihi zinazotumia wahusika wa aina hii.



Mount Kenya University

Utafiti unakusudia kutafiti riwaya za kidhanaishi kwa njia ya kuzifanya kueleweka vyema na pia kuchochea utafiti mwingine ili kuangazia vipengele vyake tofauti. Utafiti umeshughulikia kijisehemu cha wahusika jambo ambalo tunaliona litawajenga watafiti wengine kwa kuwafungua macho na kuwachochea kufanya utafiti zaidi wa kiuhakiki kuhusu riwaya za aina tofauti.

Utafiti huu utachangia kuelewa shujaa pwaya kama mmojawapo wa wahusika waliotumika katika riwaya teule za *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja Wa Fujo* (2007) na *Rosa Mistika* (1971) zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi. Kwa kutafiti suala hili, wapenzi wa riwaya watajengeka kifasihi na kuelewa uhakiki wa riwaya ya kidhanaishi. Utafiti utatoa mwanga kuhusu usawairi wa shujaa pwaya pamoja na dhima anayopewa na mwandishi. Pia, utakuwa na manufaa makubwa kwa wanafunzi wanaosomea taaluma ya fasihi katika vyuo vikuu kwa kuwa wataelewa riwaya ya udhanaishi kwa urahisi.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu umehakiki shujaa pwaya ambaye hudhihirika katika kipengele cha fani kinachohusu wahusika na uhusika wao kwa kuzingatia riwaya teule za Euphrase Kezilhabi ambazo ni *Kichwamaji*, *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Rosa Mistika*. Riwaya hizi ziliteuliwa kimaksudi kwa vile zinaweza kuainishwa kama fasihi ya udhanaishi ambayo husheheni shujaa pwaya. Isiotoshe, riwaya hizi tatu za Euphrase Kezilahabi zimeteuliwa kimakusudi na kwa kuwa mwandishi wake ni mtunzi aliyebobea katika kuweka wazi masuala yanayohusu falsafa ya udhanaishi kwa njia ya ubunifu katika jamii.

Mtafiti ameshughulikia suala la ushujaa wa wahusika ambao ni kijisehemu cha kipengele cha mtindo. Mtafiti amechunguza jinsi shujaa pwaya ametumika kusawiri mandhari, nafasi ya shujaa pwaya katika kusawiri wahusika wengine na jinsi shujaa pwaya ametumika kujenga maudhui katika riwaya teule za Euphrase Kezilahabi. Katika riwaya hizi tatu, shujaa pwaya ametumika katika kusawiri mandhari ambamo wahusika wengine wanapatikana.Aidha utafiti umechunguza jinsi shujaa pwaya amejenga sifa za wahusika wengine wanapotangamana nao na kujenga maudhui mbalimbali katika riwaya hizi teule.

Mtafiti amechunguza jinsi mwandishi ametumia shujaa pwaya kujenga hali ya kidhanaishi katika riwaya hizi teule zilizochunguzwa.

### 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa taaluma ya uandishi inayoimarika kadri siku zinavyosonga. Suala la usawiri wa wahusika katika kazi za fasihi ni la kimsingi. Utafiti utatoa mwanga kuhusu usawari wa wahusika katika fasihi ya kidhanaishi. Waandishi chipukiza watapata mwanga kuhusu usawiri wa shujaa pwaya unaofanywa na waandishi waliobobea kwa mfano Kezilahabi.

Wahakiki wa kazi za fasihi watanufaika kutokana na mapendekezo yatakayotolewa na mtafiti kuhusu uhakiki wa riwaya ya udhanaishi. Utafiti utatoa mwanga kuhusu usawiri wa shujaa pwaya katika riwaya hizi kwa misingi ya udhanaishi. Kitaaluma, utafiti utatoa mchango kuhusu misingi ya uhakiki wa fani katika kazi za fasihi kwa kuzingatia kipengele cha wahusika.

Wasomaji watanufaika kutokana na mapendekezo yaliyotolewa katika utafiti huu. Mtafiti ameweza kueleza jinsi wahusika walivyosawiriwa kwa misingi ya udhanaishi. Kwa kufanya hivyo, msomaji anaweza kubaini nyuzi zilizotumiwa na mwandishi kufuma shujaa pwaya katika riwaya ya kidhanaishi. Hili litamwezesha msomaji kuelewa hulka, wasifu na tabia za shujaa pwaya pamoja na dhima yake katika riwaya ya kidhanaishi.

Utafiti huu utasaidia kuelewa zaidi Nadharia ya Udhanaishi iliyoasisiwa na Soren Kierkegerd na kufafanuliwa zaidi na wanafalsafa Nietzsche, Martin Hiedegger, Gabriel Marcel, Karl Jaspers na Jean Paul Satre. Watafiti wanaokusudia kutumia Nadharia ya Udhanaishi watapata mwao kuhusu jinsi Nadharia ya Udhanaishi inavyoweza kutumiwa katika uhakiki wa wahusika katika fasihi ya kidhanaishi.

Mount Kenya University

## 1.8 Maelezo ya Istilahi Muhimu

**Shujaa:** ni mhusika ambaye huonyesha ubingwa katika kusaidia jamii kupitia matendo yake ya kijasiri yasiyo ya kawaida ambayo huwa chanya.

**Shujaa pwaya:** ni mhusika ambaye hufanya mambo kinyume na shujaa wa kawaida kupitia matendo yake ambapo husigana na yale ya shujaa wa kimapokeo**.**

**Riwaya:** Masimulizi ya kubuni ya kinathari yenye msuko au mpangilio fulani wa matukio au ploti inayofungamana na wakati au kusawili wakati na yenye visa vingi vinavyotendeka katika wakati fulani na yenye mawanda mapana yenye uchangamano wa dhamira, visa na wahusika.

**Udhanaishi:** Nadharia inayoshughulikia masuala yanayohusu maisha kwa jicho la kifalsafa kwa mfano, hujaribu kujibu swali: nini maana ya maisha? Hatima ya maisha ya binadamu duniani ni ipi? Nini chanzo cha furaha maishani?

**Wahusika:** ni viumbe wa fasihi wanaofinywa na mwandishi wa kazi za fasihi ili wawe wasemaji katika fasihi wa kupitisha ujumbe kwa hadhira**.**

Mount Kenya University

## SURA YA PILI

## MAPITIO YA MAANDISHI

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Pia sura hii imeelezea nadharia ambayo imetumika katika kuchambua data za utafiti huu. Ufafanuzi wa mambo ya msingi na yaliyo katika sura hii umefanywa na kueleza dhana muhimu katika utafiti huu na yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti.

### 2.2 Usawiri wa Shujaa Pwaya katika kazi za Fasihi

Katika fasihi, kipengele cha wahusika hubeba sehemu kubwa sana na hivyo basi fasihi haiwezi kukamilika bila wahusika. Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya fasihi (Wamitila, 2002). Kazi za fasihi huwa na wahusika binadamu ambao huwa na sifa za maadili, tabia, itikadi na falsafa zinazotambuliwa katika usemi wao na matendo yao. Wahusika hubainishwa mhusika mwingine anapoelezea kumhusu au anaposimulia, hisia, maadili, usemi na vitendo vya wahusika.

TUKI (1998) wanafafanua wahusika kama viumbe wa kisanaa ambao huwakilisha watu na uhalisia wa maisha ya mtu kwa kazi za fasihi ya jamii husika. Kwa kifupi wahusika ni watendaji au viumbe katika kazi ya fasihi na wao ndio nguzo kuu ya dhamira na maudhui kwa sababu ni kupitia kwao ndipo huweza kujitokeza katika kazi ya fasihi. Wahusika hawa wanaweza kuanishwa kwa njia nyingi kwa kutegemea mwandishi au msimulizi wa kazi ya fasihi. Wahusika wanaweza kubainishwa katika makundi mawili ambayo ni wahusika bapa na wahusika duara (Wamitila, 2002) ambaye anazingatia maoni ya Forster (1927).

Njia tofauti zinawezatumiwa kusawiri wahusika ambapo njia hizo hutegemea mwandishi. Pia mwandishi anaweza kuwasuka wahusika katika njia tofauti ambapo ana uhuru wa kutumia wahusika wowote na kuwateua jinsi ya kuwasilisha wao. Wanaosoma na kuhakiki fasihi huwa wanategemea sifa nyingi za

kueleza wahusika hao kwa mfano, elimu, maumbile, hulka yao, lugha, jamii na vionja vyao (Wamitila, 2002).

### 2.3. Umuhimu wa Shujaa Pwaya katika usawiri wa Mandhari ya Kazi za Fasihi

Mandhari ni elementi inayotufichulia lini na ni wapi matukio fulani yalifanyika (Wamitila, 2002) mazingira ni wakati au mahali tukio la kifasihi hubuniwa, lilivyobuniwa au litabuniwa na kufanywa na msanii wa fasihi na hivyo hufaulu kujenga msomaji kihisia au mtazamaji ama msikilizaji kutegemea kazi ya kifasihi aliyoiandaa. Mandhari ni mahali, eneo au sehemu ambapo matendo ya kifasihi yalitendeka, yatatendeka au hutendeka. Mandhari yanaweza kuwa kipindi ambacho matukio hayo yalitendeka.

Mandhari ni mahali matendo au vitendo hutendeka na kutokana na vitendo hivyo, vipengele vingine vya fasihi husawiriwa; kwa mfano maudhui mbalimbali na wahusika ambao wanahusiano mkubwa na mandhari.

### 2.4 Nafasi ya Shujaa Pwaya katika Usawiri wa Maudhui

Maudhui ni kile kilicho ndani ya kazi ya fasihi, yaani, dhamira, ujumbe, migogoro, falsafa na hisia zinazoibuliwa katika kazi hiyo (Wamitila, 2002).

Irungu (1999) amehakiki dhana ya maisha katika novela mbili za Euphraze Kezilahabi ambazo ni *Nagona* na *Mzingile* ambapo ameshughulikia elimu ya mwanadamu na mipaka ya maisha. Utafiti wa Irungu ulitupa mwangaza kuhusu usawiri wa masuala yanahusu maisha ya binadamu kwa misingi ya kidhanaishi. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na huu kwa sababu ulishughulikia usairi wa shujaa pwaya katika riwaya za kidhanaishi ambazo hazikuzingatiwa na mtafiti huyo.

Gichamba (2005) alihakiki sifa za mashujaa na umuhimu wao kwa jamii zao. Utafiti wake ulilinganisha shujaa Fumo Liyongo na Shaka Zulu, na kufafanua umuhimu wa mashujaa hawa kwa jamii zao. Utafiti wa Gichamba ulikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwa sababu ulitoa mwanga kuhusu usawiri wa shujaa

Mount Kenya University

wa kitamaduni katika fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, utafiti wetu ulizingatia usawiri wa shujaa pwaya ambaye huwa anasigana na shujaa wa kitamaduni. Isitoshe, Irungu (keshatajwa) analinganisha usawiri wa jagina katika tendi za Kiswahili ilhali utafiti wetu unajikita usawiri wa shujaa pwaya katika riwaya ya kidhanaishi.

Ochoki (2005) alitafiti sitiari, jazanda, na mwingilianomatini katika riwaya za Kezilahabi ambazo ni *Nagona* na *Mzingile*. Utafiti wake ulifafanua maudhui katika riwaya hizi mbili na jinsi mwandishi alivyojiendeleza mtindo katika uandishi wake. Pia, alichunguza jinsi mbinu za uandishi kama vile sitiari na jazanda zinavyosawiri wahusika na maudhui katika riwaya hizi mbili za Euphrase Kezilahabi. Hata hivyo, utafiti wa Ochoki unatofautiana na wetu kutokana na riwaya zinazochanganuliwa na masuala yanayochunguzwa. Utafiti huu unachunguza usawiri wa shujaa pwaya katika riwaya za *Rosa Mistika*, *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Kichwamaji*.

Mohamed (2017) alihakiki kwa kulinganisha tabia za wahusika wakuu na malengo yao katika riwaya za *Kusadikika* na *Utengano*, ambapo aliweka wazi sifa za wahusika wakuu. Utafiti wake ulikuwa na manufaa katika utafiti huu kwa vile ulionyesha bayana misingi na nguzo za usawiri wa wahusika wakuu katika kazi za fasihi. Aidha, utafiti wa Mohamed (keshatajwa) unabainisha dhima ya mhusika mkuu katika kuendeleza maudhui muhimu ya kazi hiyo. Hata hivyo, utafiti wetu unachunguza mhusika mahususi ambaye ni shujaa pwaya na jinsi anavyosawiriwa katika riwaya ya kidhanaishi.

Haji (2018) alihakiki mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya za *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*. Haji aliweza pia kulinganisha na kutofautisha mbinu zilizotumika kusawiri wahusika katika riwaya hizo mbili. Utafiti wa Haji (keshatajwa) ulikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu anazingatia mojawapo wa riwaya zinazochanganuliwa katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wetu unachunguza jinsi mhusika mkuu aliye na sifa za kuwa shujaa pwaya navyojitokeza katika riwaya ya

Mount Kenya University

Dunia Uwanja wa Fujo. Kwa hivyo, utafiti wetu unapiga hatua zaidi kwa kuonyesha usawiri wa shujaa pwaya kwa misingi ya falsafa ya Udhanaishi.

Ogonda (2019) alitafiti taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili kuanzia mwaka wa 2000 hadi 2006. Aliangazia athari za taswira ya mwanamke kiongozi kwa uongozi, akieleza jinsi wahusika walivyomsawiri mwanamke kiongozi na athari zake kwa uongozi. Utafiti wake ulihusisha tamthilia ishirini na tatu, jambo ambalo linatofautiana na utafiti wetu unaolenga riwaya ya kidhahania.

Kanwa (2022), katika tasnifu yake, alihakiki usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake. Kanwa alichanganua jinsi wahusika wa kiume wanavyowasilisha dhamira na taswira zinazotumiwa na waandishi kusawiri wahusika wa kiume. Utafiti wa Kanwa (keshatajwa) ulikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu unashughulikia suala la usawiri wa wahusika. Hata hivyo, utafiti wetu ulipiga hatua zaidi kwa kumlenga mhusika anayebainisha sifa za ushujaa pwaya katika riwaya ya kidhanaishi.

## 2.5. Misingi ya Nadharia

Massamba (2004) anaeleza nadharia kuwa utaratibu na msingi unaojengwa katika mawazo ambapo utatumiwa kama kielezo cha jambo. Wamitila (2011) naye anaeleza kwamba nadharia ni fikra, mawazo au maelezo ambayo hutolewa ili kueleza kuhusu hali fulani, jinsi inatenda kazi, chanzo chake na mwingiliano wake katika sehemu zote. Hivyo basi nadharia huongoza na kuelekeza msomaji ambaye husoma kazi ya fasihi ili kuifahamu pamoja na vipengele vyake vyote. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Udhanaishi ambayo imefafanuliwa katika sehemu inayofuata.

### 2.5.1 Nadharia ya Udhanaishi

Udhanaishi ni hali inayozingatia masuala yanayohusu maisha au mtazamo unaochunguza kwa kina hali inayomuelezea binadamu duniani, huku ikizungumzia uhusiano na imani katika kuwepo kwa Mola (Camus, 1984). Udhanaishi ni nadharia inayojikita sana katika masuala ya maisha, ambapo swali la

msingi linakuwa: "Maisha ni nini?" Wafuasi wa udhanaishi hutafiti kwa undani nafasi ya mtu duniani, pamoja na kuchunguza uhusiano uliopo kati ya mtu na Mungu (Njogu na Chimera, 1999). Wamitila (2003) anaeleza udhanaishi kuwa ni hali inayotumiwa kufafanua falsafa ya kuwepo kwa maisha duniani. Hali hii inatumiwa kueleza kuhusu maono au mitazamo inayohusiana na jinsi maisha ya mtu, jukumu lake duniani, nafasi yake, pamoja na uhusiano wake na Mola.

Kwenye utafiti huu, mtafiti aliongozwa na Nadharia ya Udhanaishi iliyoasisiwa kwa kiasi kikubwa na Mwanthropolojia Soren Kierkegaard (1813-1855). Kierkegaard anaeleza kuwa mtu hujihisi akitegemea nguvu fulani zinazotoka kwa Mungu, na si kwa uwezo wake mwenyewe. Dhambi zinazotendwa na binadamu humfanya akose amani, na hivyo hupelekea kutubu ili kupata utulivu wa kiroho. Wanadhanaishi wanaamini kuwa Mungu yupo ndani ya kila mtu na kwamba binadamu hutegemea nguvu hizi za kiungu. Anapozitegemea, eanapata utulivu wa kiroho, lakini anapozipuuza, hukumbwa na hali ya kutokuwa na amani. Kierkegaard anaendelea kufafanua udhanaishi kama hali ya kuogopa adhabu kutoka kwa Mungu na kuwa na wasiwasi wa kufanya makosa. Anaweka mkazo kwenye hali ya ubinafsi wa binadamu, ambapo mtu hajali maslahi ya wengine na anapokutana na migogoro, hukimbilia Mungu.

Udhanaishi ulipata msukumo mpya kutoka kwa mwanafalsafa wa Kijerumani Friedrich Nietzsche na wanafalsafa wengine kama Martin Heidegger, Gabriel Marcel, na Karl Jaspers (Wamitila, 2003). Jean-Paul Sartre, mwanafalsafa wa Kifaransa ambaye ni mmoja wa waasisi na waitifaki wa udhanaishi, anasema kuwa binadamu huzaliwa au hujikuta amewekwa katika ombwe fulani (Njogu na Chimera, 1999). Maoni haya yalitolewa baada ya Vita Kuu vya Dunia. Sartre anaamini kuwa binadamu yu huru wa kuishi na kujaribu kuelewa dunia inayomzunguka, lakini anakosa uwezo wa kuepuka maumivu na mateso anayopitia, jambo linalosababisha kukata tamaa. Katika mhadhara wake maarufu, alisisitiza dhana ya "kuzimu ni watu wengine," akimaanisha kuwa uhuru wa kuchagua na kuathiriwa na matendo ya wengine ni chanzo cha matatizo mengi ya binadamu. Sartre pia alisisitiza kuwa dini haina uwezo wa kutatua shida za mtu, na hivyo alielekea katika falsafa ya ubinafsi wa mtu.

### 2.5.2 Mihimili ya Nadharia ya Udhanaishi

Wafula na Njogu (2007) wanabainisha mihimili ya ifuatayo ya Nadharia ya Udhaniashi:

i. Udhanaishi hutilia mkazo matatizo halisi yanayomsibu binadamu.
ii. Hawana imani ya kuwepo kwa Mungu ambaye ni muumba wa dunia.
iii. Bidii ya mtu binafsi ya kujitafutia au kukabiliana na maisha ambapo huishia kwa mauti.
iv. Wadhanaishi hutaja maudhui kama vile uhuru wa mtu mwenyewe, kuweza kujifikiria na kufanya uamuzi binafsi.
v. Wanajadili hali inayotatanisha kwa mfano mashaka na kuchoka kutokana na mambo mbalimbali yatutatizayo na jinsi yanavyoathiri maisha ya mtu.
vi. Wanajadili ukengeushi kama maudhui (hali ya utamaushi au kukosa uhakika)
vii. Wadhanaishi hutumia taswira kama mtindo ili kuchorea msomaji picha mbalimbali za maisha ya shida anayopitia binadamu.

Mhimili wa kwanza, wa tatu, wa nne, wa tano, na wa sita ilisaidia katika kutathmini shujaa pwaya kwa kuzingatia usawiri wa wahusika, mandhari, na maudhui katika riwaya za *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Kichwamaji*, na *Rosa Mistika*. Mhimili wa pili na wa saba ulisaidia kutathmini kipengele cha shujaa pwaya ambacho kinajitokeza kupitia wahusika na uhusika wao, ambapo nadharia hii ilitumika kuhakiki wahusika katika kazi za fasihi.

## 2.6 Hitimisho

Sura hii imewasilisha mapitio ya kazi tangulizi pamoja na dhana za nadharia zilizotumika katika utafiti huu. Aidha, imeeleza nadharia na misingi yake iliyotumika kuongoza na kutathmini utafiti, pamoja na mihimili ya nadharia ya umitindo. Ufafanuzi wa dhana muhimu ambazo zimetumika katika kujenga utafiti huu umeainishwa.

Mount Kenya University

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura ya tatu ilizingatia vipengele vifuatavyo: eneo la utafiti, muundo wa utafiti, uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, uhalali wa vifaa vya utafiti, kutegemewa kwa vifaa vya utafiti, mbinu za ukusanyaji data, mbinu za uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeao ya utafiti, maadili yanayohusu utafiti na hitimisho.

## 3.1 Eneo la Utafiti

Katika kufanikisha malengo ya utafiti huu, ilibidi mtafiti atekeleze utafiti wa maktabani. Usomaji mpana na uhakiki na uchanganuzi wa riwaya teule ambazo ni *Dunia Uwanja Wa Fujo* (2007), *Kichwamaji* (1974) na *Rosa Mistika* (1971) ulifanywa maktabani. Pili, mtafiti alisoma tasnifu, makala, majarida, vitabu na kupekuapekua mtandao ili kupata data ya kuridhisha ili kudhibiti mada ya utafiti pamoja na kupata mawazo yaliyoandikwa kuhusu mada hii. Aidha,  mtafiti alisoma kwa kina maktabani kuhusu misingi ya riwaya na Nadharia ya Udhanaishi ambayo ndiyo nguzo muhimu katika utafiti huu.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Mbinu ya kimaelezo ilitumika pale ambapo mtafiti alidondoa sehemu au matukio ya kimaelezo na kuyachanganua kutoka kwa kazi za fasihi zilizochunguzwa. Sehemu au matukio ya kimaelezo ambayo yamedondolewa katika riwaya teule na kuchanganuliwa ndiyo data ya utafiti. Aidha, mbinu ya kitakwimu ilitumika pale ambapo mtafiti alichagua riwaya teule na kuzichanganua. Mtafiti alichanganua riwaya teule kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mapendekezo ya mihimili ya Nadharia ya Udhanaishi. Mihimili ilisaidia kukusanya data, kuchanganua data na kufafanua na kufasiri data hiyo ili ieleweke vizuri.

### 3.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli iliteuliwa kwa kuuteuzi wa sampuli wa kukusudia. Mtafiti alijikita katika utanzu wa riwaya katika fasihi andishi. Pili, alitathmini riwaya za mwandishi mmoja yaani Euphrase Kezilabi ambazo zilitungwa kwa kuzingatia falsafa ya kidhanaishi. Vilevile, mtafiti alitumia mbinu kusudio katika kuteua riwaya zinazoafiki malengo ya utafiti ili kupata data iliyokidhi mahitaji ya utafiti huu. Riwaya teule zilizoshirikishwa katika utafiti huu ni *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Rosa Mistika* na *Kichwamaji* ambazo mhusika wake mkuu anaakisi sifa za ushujaa pwaya. Riwaya zilizoachwa ni *Gamba la Nyoka*, *Mzingile* na *Nagona* ambazo hazikuafiki kigezo hicho.

Uteuzi wa sampuli kimaksudi ulifanywa kwa kuchunguza riwaya sita za Kezilahabi na kuchagua zile zilizokuwa na shujaa pwaya ambaye angetafitiwa zaidi kuonyesha usawiri wake pamoja na dhima yake katika kukuza maudhui, mandhari na wahusika wenzake.

### 3.4 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vilivyotumika katika utafiti ni riwaya tatu za Euphrase Kezilahabi ambazo ni *'Dunia Uwanja wa Fujo','Kichwamaji'* na '*Rosa Mistika'*. *Utafiti pia utapekua* majarida na kuzingatia utafiti kwenye intaneti kuhusu usawiri wa shujaa pwaya katika kazi za fasihi.

### 3.5 Uhalali wa Vifaa vya Utafiti

Data iliyokusanya ilikuwa halali na kutokana na uchanganuzi wa kina wa riwaya tatu zilizochanganuliwa ambazo ni: '*Dunia Uwanja wa Fujo', 'Kichwamaji'* na '*Rosa Mistika'*. Hili lilizingatia mapendekezo ya Mugenda na Mugenda (2003), kuwa uhalali ni matokeo yaliyotokana na uchanganuzi wa data iliyowakilishwa katika utafiti kwa njia iliyozingatia uhalisia wa mambo.

### 3.6 Kutegemewa kwa Vifaa vya Utafiti

Nadharia ya Udhainaishi ilituongoza katika ukusanyaji wa data muhimu ya utafiti kwa kuchanganua riwaya tatu za Kezilahabi ambazo ni '*Dunia Uwanja wa Fujo', 'Kichwamaji'* na '*Rosa Mistika'*. Mihimili

Mount Kenya University

ya Nadharia ya Udhanaishi ilitumika kukusanya data iliyohitajika na vilevile kufasiri matokeo ya utafiti. Hali hii ilifanya vifaa vya utafiti kuwa vya kutegemewa.

### 3.7 Mbinu za Ukusanyaji Data

Mtafiti alisoma na kuhakiki riwaya za Kezilahabi ambazo ni: *Dunia Uwanja wa Fujo', 'Kichwamaji'* na '*Rosa Mistika'* aliongozwa na mihimili ya Nadharia ya Udhanaishi. Mtafiti alizingatia madhumuni ya utafiti kwa kufanya udondozi wa hoja zilizo muhimu kutoka kwa riwaya zilizochanganuliwa na kuongozwa na mihimili ya nadharia ya udhanaishi.

### 3.8 Mbinu za Uchanganuzi wa Data

Mihimili iliyotokana na Nadharia ya udhanaishi ilitumika katika kuchanganua data katika utafiti huu. Data iliyokusanywa ilifafanuliwa, ilifasiriwa na kutolewa maelezo ya kina kwa mujibu wa mihimili ya Nadharia ya Udhanaishi. Aidha, data ilichanganuliwa na kufasiriwa kwa mujibu wa maelezo ya Nadharia ya Udhanaishi.

### 3.9 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulitumia data ya kiuthamano iliyokusanywa. Data hii ilichanganuliwa, kufasiriwa na kutolewa maelezo ya kiufafanuzi kwa kuzingatia mihimili ya Nadharia ya Udhanaishi. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya ufafanuzi na maelezo. Maelezo haya yalitolewa kwa kuegemea Nadharia ya Udhanaishi.

### 3.10 Maadili yanayohusu Mtafiti

Kamati inayoshughulikia maadili katika Chuo Kikuu Cha Mount Kenya (MKU) iliombwa kibali cha kufanya utafiti huu. Vyanzo vya data iliyotumika katika utafiti huu vimebainishwa na kuonyeshwa kwenye marejeleo ya kazi. Utafiti huu ulitumia vyanzo ambavyo vimebainisha na kuonyeshwa katika marejeleo ya kazi hii. Kazi za wanafasihi wengine na waandishi mbalimbali zilinukuliwa na kuonyeshwa chanzo chake kulingana na kanuni za kunukuu za APA.

Mount Kenya University

### 3.10.1 Maadili kuhusu Waandishi wa Kazi za Fasihi

Baadhi ya kazi za waandishi ambazo zimelindwa na hatilinzi, zimenukuliwa na kubainishwa chanzo chake kwenye marejeleo; sababu ya kuwa wanafasihi hunukuu kazi zilizochanganuliwa ili kutoa ithibati na ushahidi wa kimawazo kwa mujibu wa madai yanayotolewa na ujumbe unaokusudiwa.

### 3.10.2 Maadili Kuhusu Mchakato wa Utafiti

Kupitia kamati inayoshughulikia maadili katika Chuo Kikuu Cha Mount Kenya, Kibali cha kufanyia utafiti kiliombwa kutoka NACOSTI. Kibali cha utafiti pamoja na Barua ya Idhini kutoka kwa Kamati ya Maadili vimeambatishwa katika ripoti hii.

## 3.11 Hitimisho

Sehemu hii imeshughulikia mambo ambayo ndiyo msingi wa utafiti huu. Sehemu hii ndiyo inayohusu methodolojia ya utafiti na ndiyo inayojenga msingi wa mbinu zitakazozingatiwa katika utafiti. Sura inayofuata inaangazia uchanganuzi wa data na usawilishaji wa matokeo ya utafiti.

Mount Kenya University

## SURA YA NNE

## UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO YA UTAFITI

### 4.1 Utangulizi

Sura hii imezingatia uwasilishaji na uchanganuzi wa data iliyokusanywa na usawilishaji wa matokeo ya utafiti ya kufanikisha malengo ya utafiti huu. Vipengele vilivyozingatiwa ni muhutasari wa riwaya teule na kutathmini na kujadili ujumbe muhimu unaowasilishwa kupitia mhusika shujaa pwaya katika riwaya: *Dunia Uwanja Wa Fujo* (2007), *Kichwamaji* (1974) *na Rosa Mistika* (1971). Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa mujibu wa mihimili ya Nadharia ya Udanaishi ili kujibu maswali ya utafiti. Aidha, Matokeo yaliwasilishwa kwa kufasiri na kufafanua data kwa mbinu ya maelezo.

### 4.2 Historia fupi ya Euphrase Kezilahabi

Euphrase Kezilahabi ni mmoja wa waandishi kutoka Tanzania ambaye amejulikana kwa michango yake katika fasihi ya Kiswahili. Aliishi katika kipindi cha mabadiliko makubwa ya kijamii na kisiasa, na kazi zake zililenga kutoa picha ya hali halisi ya jamii ya wakati wake. Euphrase Kezilahabi alizaliwa katika Kisiwa cha Ukerewe kijijini Namagondo mnamo tarehe 13 Aprili 1944. Alisoma katika shule ya Msingi ya Nakasyenge kati ya mwaka wa 1957 na 1967 na baadae akajiunga na Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam kusomea ualimu na fasihi, na alipata cheti cha (B.A) mwaka wa 1970. Alifunza shule ya Upili ya Mzumbe mnamo mwaka wa 1970 kisha akaenda kufunza shule ya Upili ya Mkawa. Katika mwaka wa 1971 alifanya shahada yake ya uzamili na akawa mhadhiri msaidizi katika Chuo Cha Dar es Salaam na kisha akaendelea na masomo ambapo alifanya shahada yake ya uzamivu mwaka wa 1985 katika Chuo Cha Wisconsin Madison.

Mnamo mwaka wa 2012 alielekea nchi ya Botswana kufanya kazi kufunza kama mhadhiri katika Chuo Kikuu Cha Botswana kama profesa wa lugha za kiafrika. Katika uandishi ambapo yeye ndiye mwandishi wa kwanza bara la Afrika aliyandika riwaya za kidhanaishi za Kiswahili ambazo ni: *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974) *na Dunia Uwanja Wa Fujo* (1975). Alizidi kubobea katika uandishi wa riwaya

ambapo aliandika riwaya zingine zaidi kama vile: *Gamba La Nyoka* (1979), *Nagona* (1990) na *Mzingile (*1991). Mnamo mwaka wa 1994 alichaguliwa kama mmoja ya maaji katika utunzaji wa zawadi kwa waandishi waliobobea katika unandishi katika jumuia ya madola.

Katika uandishi wake, alitumia mtindo wa kisasa ambapo alizungumzia mambo yanayohusu jamii kwa mtazamo wa kipekee. Euphrase Kezilahabi ni mmoja wa waandishi ambao waliandika kwa mtindo wa kisasa na ule wa kimajaribio tofauti na waandishi wa zamani ambao walitumia mtindo wa kijadi na ule wa kimapokeo. Masuala ambayo aliyazungumzia katika kazi zake ni pamoja na mtindo wa ushairi na masuala ya utamaduni wa Kiafrika.

Mchango wake umekuwa mkubwa katika ukuaji wa lugha Kiswahili ambapo umekuwa na athari kubwa katika jamii ya kisasa. Katika kazi zake, ameweka wazi na kueleza hali halisi ya jamii ambapo amezingatia masuala ya maisha ya kawaida. Ameeleza kuhusu mabadiliko na athari ya mabadiliko katika jamii. Euphrase Kezilahabi aliaga dunia mnamo mwaka wa 2020 baada ya kuugua kwa muda mrefu akiwa jijini Dar es Salaam.

### 4.2.1 Muhtasari wa *Dunia Uwanja Wa Fujo* (1975)

*Dunia Uwanja Wa Fujo* ni riwaya ya mwandishi Euphrase Kezilahabi ambayo aliandika mwaka wa 1975. Amesimulia kuhusu maisha ya mhusika mkuu ambaye ni Tumaini na maisha ya wanajiji wa Bugolola. Tumaini alikuwa mtoto wa pekee wa Kapinga na Muyango ambaye alilelewa maisha yake ya kudekezwa. Mwandishi anaeleza kuwa ndiye mtoto wa pekee aliyebahatika kuishi baada ya kuzaliwa. Kapinga alikuwa na furaha ya kupata mtoto wa kiume ambaye atakuja kurithi mali yake ndiposa urithi wake aliuachia Tumaini. Kapinga aliaga kutokana na mawazo ambapo alikuwa anawaza kuhusu ni nini mtoto wake atarithi na mke wake alienda kufanya nini alipoenda kuwasalimu wazazi wake.

Mwandishi, Euphrase Kezilahabi, anatoa taswira ya maisha katika kijiji cha Bugolola ambacho kilitawaliwa na ushirikina na uchawi. Uchawi huu ulifanywa na Mugala ambaye ni mamake Kasala.

Uchawi wa Mugala ulikuwa wa kubadilisha watu kuwa vizuu ili awatumie kufanya kazi zake kama vile kuchota maji, kulima, na kazi nyingine za kila siku. Mugala aliishi na Leonila ambaye ni mjuu wake. Leonila ndiye alifanya Tumaini kuzoeana na Mugala kwa kuwa alimhonga ili amruhusu kutoka naye wakati wa usiku. Kijiji hiki cha Bugolola kilikuwa na ushirikiano katika masuala ya usalama na mambo mengine kama vile utamaduni. Wanakijiji walizoea kuketi pamoja na kusuluhisha mambo yao na pia kunywa pombe pamoja. Tumaini ndiye alifichua siri ya vizuu kutumia Leonila. Wanakijiji walishikwa na hamaki na kutaka Mugala kufukuzwa. Mugala alipelekwa katika kisiwa cha wachawi na kuachwa huko.

Tumaini aliwalaghai wasichana kama vile Leonila kimapenzi. Mwandishi anasema kuwa alitumia elimu yake kuwahadaa wasichana kisha kuwaacha bila huruma. Alipompachika mimba Leonila, alimkataa na kukana kuwa mimba si yake. Tumaini alimwambia kuwa hawezi mwoa na kuwa Leonila alikuwa na wanaume wengi. Mungere ambaye ni mamake Leonila asikitika sana akijua kuwa msichana wake ameharibiwa maisha na hataweza kupata mume akiwa amezaa kabla ya kuolewa.

Mwandishi anazidi kutoa picha kuhusu maisha ya Tumaini ambapo atafuta furaha na jinsi ilivyokumbwa na matatizo. Maisha katika kijiji cha Bugolola alimkera kwa kuwa watu wanauawa, uchawi uliwakosesha amani na tabia zake zilikuwa zimeanza kuwakera wanakijiji. Baada ya Tumaini kumwacha Leonila, alianza uhusiano wa kimapenzi na Anastasia. Kilichokuwa kinamsumbua Anastasia ni kutafutiwa mume na pia alijua kuwa Tumaini ana wasichana wengi. Anastasia aliamua kuenda na Tumaini kwa sababu aliona ni vyema kuliko kuolewa na Tembo ambaye ni mzee sana kulingana na umri wake. Tumani alipanga njama ya kumtorosha Anastasia ili asije akaolewa na Tembo na hivyo ndio walioana.

Ndoa ya Tumaini ilianza kukumbwa na shida hapo awali. Shida zilizokumba ndoa hii ni ulevi wa Tumani na tabia yake ya uzinzi. Tumaini, Anastasia na John wanahamia Shinyanga baada ya Tumaini kumtorosha Anastasia kwao na wakati huo serikali ilitangaza Azimio La Arusha ili kuleta mafanikio kwa wananchi. Azimio hili lilileta mchafuko kutokana na kutaifishwa kwa mashamba ya watu, Tumaini akiwa mmoja

wao. Tumaini aliamua kumuua mkuu wa wilaya kwa kuwa ndiye aliyetangaza Azimio hilo na kumalizia kuhukumiwa kunyongwa. Tumaini alighadhabishwa na tangazo hili kwa kuwa alikuwa amefanya mabidiliko katika maisha yake. Alikuwa amefanya maendeleo katika mashamba yake ambapo alifuga wanyama na kupanda mimea. Uamuzi wake wa kumuua mkuu wa wilaya ulisababisha kufungwa kwake na kuhukumiwa kifo.

### 4.2.2 Muhtasari Wa Kichwamaji (1974)

Katika riwaya ya '*Kichwamaji'* mhusika mkuu, Kazimoto alijikuta akiwa ofisini mwa mkuu wa wilaya ambaye anamfahamu akitafuta kazi. Akiwa ofisini, anakumbuka uhasama ulioko katika yake na Manase ambaye ni mkuu wa wilaya. Kinachomshangaza Kazimoto ni jinsi Manase alivyopata kazi hiyo n jinsi aliyotumia wanawake jinsi alivyotaka, kwa mfano dadake; Rukia ambaye alimharibia maisha.

Kazimoto alilelewa katika kijiji cha Mahande ambacho kilithamini na kuwajibika katika malezi. Mwandishi anaeleza na kutupa taswira ya malezi walioipata Kazimoto na Manase ambapo yalikuwa tofauti na wengine. Manase na Kazimoto ni vijana waliopata elimu ya kisasa ambayo ilileta mabadiliko katika maisha yao. Elimu hii ndio inaleta uwajibikaji wa Kazimoto kwa mfano, aliamua kumpeleka Rukia ambaye ni dadake shuleni. Changamoto aliyoipata Rukia katika masomo yake ni kuwa hakuwa na mlezi wa kuishi naye. Kazimoto alimtafutia mtu wa kuishi naye na akapata Manase ambaye alikuwa rafiki yake. Manase alikubali kuishi na Rukia kwa sababu shule yake ilikuwa karibu naye na pia Kazimoto alikuwa amebaki na siku chache akamilishe masomo yake. Wakati mmoja, Manase alimshika Rukia kwa nguvu na kumlazimisha kulala naye. Manase alimharibia Rukia maisha yake ambapo alimtia mimba iliyomfanya kuacha kusoma.

Kazimoto aliamua kulipiza kisasi kwa familia ya akina Manase ambapo alichoma nyumba yao na kupanga kumharibia Sabina maisha. Katika harakati za kupanga jinsi ya kumharibia Sabina maisha, wazo lingine lilimkujia na akabadilisha nia. Kazimoto aliamua kumwoa Sabina. Sabina alikuwa nduguye Manase na ni mtoto wa Kabenga.

Mwandishi anatupa taswira ya maisha ya hawa vijana wawili na akilichotofautiana na maisha ya kizazi cha wazee. Elimu ya hawa vijana iliwabadilisha na wakaanza kuishi maisha ya kibinafsi na ambayo yalijawa na shauku ya anasa. Vijana hawa wanajiingiza katika anasa tofauti ambayo inaathiri maisha yao kwa njia hasi. Usherati na ulevi ulitawala maisha yao; kwa mfano, Kazimoto anamtumia Vumilia kimapenzi. Alizoea kumchukua kutoka nyumbani kwao nyakti za usiku wakiwa na Kalia na kumrudisha usiku. Kalia anajifunza tabia hii kutoka kwa Kazimoto na akaanza kuhangaisha wanawake na wasichana kijijini. Kalia aliwahi kumbaka msichana mmoja liyekuwa anachunga ng'ombe na pia alianza kufanya mapenzi na Tegemea.

Familia ya Mzee Mafuru ilikumbwa na changamoto za kitanzia ambapo, baada ya kifo cha Rukia, kinafuata kifo cha Kalia aliyeuawa kwa utukutu wake kwa kuchomwa mkuki. Ndoa ya Kazimoto na Sabina ilikumbwa na tatizo la maradhi ambapo walijifungua mtoto mwenye kichwa kikubwa na kisha akaaga. Kifo cha mtoto wake kilimfanya Kazimoto kujuta kwa matendo yake na akaamua kujitia kitanzi.

**4.2.3 Muhtasari wa *Riwaya ya Rosa Mistika* (1971)**

Rosa Mistika ni kifungua mimba wa Zakaria na Regina ambao walibarikiwa kuwa na watoto wa kike pekee na mvulana mmoja ambaye alikuwa kitinda mimba. Regina alipitia mateso na unyanyasaji kutoka kwa Zakaria ambaye ni mumewe na kumwachia malezi kwa kiasi kikubwa. Ulevi wa Zakaria ulifanya kupigwa kalamu kama mwalimu hata pia kumalizia kutumia pesa za Rosa za kumlipia shuleni alizopewa na Regina.

Zakaria alikuwa amewachunga wasichana wake sana ambapo hakutaka watangamane na wavulana. Wakati mmoja alipotoka ulevini kurudi nyumbani kama kawaida na kelele zake, alipofika nyumbani Stella alimwambia kuwa Rosa alikuwa amepokea barua pamoja na pesa. Zakaria alikasirika na kumwita Rosa afike mahali yupo pamoja na barua lakini alisitsita na alipomwomba barua alijaribu kuitafuna. Rosa alipata kichapo kikali kutoka kwa Zakaria hadi watoto pamoja na Regina wakaanza kulia. Zakaria alimwambia kuwa asilete umalaya kama mamake.

Bidii ya Rosa katika masomo ilimpa nafasi ya kungia shule ya wasichana ya Rosary ambayo ilisimamiwa na masista. Zakaria hakuwa na pesa za kumpeleka shuleni kwa hivyo ilibidi wauze ng'ombe mmoja ili kupata pesa za kufadhili masomo yake. Rosa alipewa shilingi sabini za kununua sanduku, viatu na shuka. Wakati mmoja Zakaria aliendа kunywa pombe, alikunywa zaidi hadi akashindwa kutembea na ikabidi abebwe na Ndalo na mtu mwingine. Akiwa ulevini, alikunywa pombe kupita kiasi hadi akatumia pesa zilizotakiwa kwa ajili ya shule ya Rosa.

Katika shule ya Rosary, Rosa alijulikana kama msichana mwema na Sista John. Rosa alizoea maisha katika shule hii na likizo ilipofika alienda nyumbani. Akiwa nyumbani Regina alimtuma kwa Bigeyo kumweleza kuhusu ugonjwa wake. Zakaria alipofika nyumbani alipata kuwa Regina ashajifungua mtoto wa kiume. Alifurahi sana na akamwambia Regina kuwa mji umekuwa wake sasa. Rosa aliporudi shuleni, wanafunzi wengine walianza fujo na wengine walianza tabia ya kutoka usiku kuenda mjini na kurudi asubuhi sana. Sista John alimwita Rosa na kumuuliza kuhusu wasichana hao. Rosa alisema majina hayo na baada ya kuwasema, wasichana hao walienda wakararua vitabu vyake, wakachoma nguo na kumwagia maji vitabu vingine.

Rosa alifaulu na kuingia chuo cha mafunzo ya ualimu ambapo maisha yake yalichukua mkondo mwingine alipoanza kuwa na hisia kuelekea kwa wanaume kinyume na matarajio ya babake. Pia mabadiliko haya yalichongewa na wasichana wenzake wakiwa shuleni kwa kuwa walitoka shuleni kuenda kuona wapenzi wao. Haikuchukua muda kabla hajajiingiza katika mambo hayo hadi akaitwa malaya, kwani alianza kulala na mwanaume yeyote kama wasichana wengine waliotaka pesa kutoka kwa wanaume. Kezilahabi anatumia udhanaishi kueleza hali ya maisha ya Rosa kupitia utamaushi kama tukio kuu lilotawala riwaya hii. Rosa alitamauka na kuanza vitendo vya ukware baada kupata habari kuwa Deogratias ambaye ni mchumba aliyetarajia kuwa atamwoa, ana wanawake wengi. Matendo haya yaliwafanya wanaume kumtumia kwa kumaliza haja zao za kimwili na wengine ambao alifikiria ni wachumba walimkataa. Kifo cha  wazazi wake kilimfanya ajione kuwa hana thamana yeyote. Kifo cha

Zakaria kilimpata akitoka kunywa pombe ambapo alichomwa mkuki na Regina naye aliaga kutokana na mshtuko wa kifo cha mumewe. Rosa Mistika naye alijiuua kwa kumeza vipande vya chupa alivyovunja baada ya kupata barua kutoka kwa mchumba wake kuwa hawezi kumwoa.

### 4.3 Usawiri wa Shujaa Pwaya Katika Riwaya za *Rosa Mistika*, *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Kichwamaji*

Usawiri ni mbinu ambayo hutumika katika fasihi kuonyesha hali, wahusika, matukio, hisia za wahusika na mazingira. Pia, ni njia ya kuwasilisha picha au hali katika kazi ya fasihi ambayo humfanya msomaji au mtazamaji kuona, kuhisi au kugusa kile kilichosimuliwa (Wamitila, 2017).

Taswira ni dhana au picha ambayo huibuka kutoka kwa matumizi ya lugha au maandiko katika fasihi. Picha hii huwa ni ya kiakili au hisia ambazo huzalishwa katika akili ya msomaji kutokana na matumizi ya mbinu za fasihi kwa mfano tamathali ya usemi au methali. (Wamitila, 2017)

Kusawiri ni kufanya sura ya kitu kwa kutumia picha, kalamu au mashine za kutolea picha. Maisha yanaweza kusawiriwa kama uundaji wa kazi ya sanaa inayosawiri, kuiga maisha kwa kuzingatia misingi ya maisha ya jamii husika (Msokile, 1993). Usawiri ni kuchora sura kitu kwa kutumia vifaa kama vile kalamu, penseli au chaki. Pia kusawiri ni kutenda kwa kuunda sura ya mtu, kitu au jambo katika akili (BAKIZA, 2010). Kusawiri ni kuchora picha ya kitu, mtu au jambo fulani ili kuleta au kukipa, kumpa sura fulani. Kwa kufanikisha malengo yake, mwandishi ametumia sehemu ya wahusika na uhusika wake kujenga ploti.

Kwa hivyo, mwandishi Euphrase Kezilahabi amewachora au kuwasawiri wahusika wakuu katika riwaya teule kwa njia hasi. Wahusika hawa wakuu wanaofanya mambo ambayo ni kinyume na matarajio ya wanajamii walio wengi kwa njia hasi ndio shujaa pwaya. Matendo yao huwa yanawathiri wahusika wengine au jamii kwa njia hasi na wao huishi maisha ya kidhanaishi ambapo hutamauka mwishowe. Mwandishi amewasawiri shujaa pwaya hawa kuwa muhimu katika riwaya ambapo wasomaji hupata

funzo la kimaadili linakusudiwa kuwabadilisha katika maisha yao. Sehemu inayofuta inajadili usawiri wa Shujaa pwaya katika riwaya teule zinazochunguzwa katika utafiti huu.

### 4.3.1 Shujaa Pwaya kama Mwasi wa Misingi ya Kimaadili na ya Kitamaduni iliyowekwa na kuthaminiwa na Jamii yake

Shujaa pwaya anasawiriwa kama mwasi anayekiuka misingi ya kimaadili na ya kitamaduni iliyowekwa na kuthaminiwa na jamii yake. Mwandishi amemsawiri akivunja kimaksudi maadili ya Kiafrika yanayothaminiwa na jamii nzima. Shujaa pwaya hatii mamlaka yoyote. Aidha, hakubali kuishi chini ya himaya ya misingi ya imani iwe ama ya dini au ya kitamaduni inayoheshimika na kuthaminiwa katika jamii.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, mwandishi amemsawiri Rosa kama mwasi wa misingi ya kimaadili na kitamaduni. Kwa mfano, Rosa alikiuka utaratibu wa utamaduni kuwa uhusiano wa mapenzi huanza katika utu uzima katika ndoa. Jamii ilimtazama cha jicho hasi kama mtu aliyekiuka utaratibu uliokubalika kimaadili na kuwa kahaba. Kitendo cha Rosa cha kupokea barua na pesa kutoka kwa Charles, kinamfanya kusawiriwa kuwa kahaba na babake ambaye ni Zakaria. Hili linabainika katika dondoo lifuatalo:

> " *lazima unionyeshe barua hiyo! Unataka kuniletea umalaya wa mama yako hapa!"*
> (uk 7).

Mwandishi anazidi kueleza jinsi Rosa anakiuka maadili yalioyowekwa na jamii. Kwa mfano Rosa alianza kuwa mnafiki ambapo hakutaka kusema ukweli kwa waliokuwa wameweka imani na matumaini kwake ya kusema ukweli kama vile wakuu wa shule. Rosa alikataa kuwasema na kutoa majina ya wasichana waliokuwa wameanzisha fujo na kelele darasani alipoulizwa na Sista. Pia anakataa kuwasema wasichana ambao wamekuwa wakilala mjini na kuletwa asubuhi kwa gari wakiwa wamelewa.

Katika chuo cha Morogoro TTC, Rosa alibadilika kitabia baada ya kuanza kutangamana na wavulana. Hii inadhihirika wakati Rosa alipopata busu kutoka kwa Deogratias alipokwenda densi mjini. Baada ya kusalitiwa na Deogratias aliamua kutafuta wanaume wengine aliowataka. Jamii inamtazama kwa jicho



Mount Kenya University

hasi kwa kuwa anakiuka ule utaratibu wa vigezo vya kimaadili vilivyowekwa kuhusu suala la mapenzi kabla ya ndoa.

Rosa Mistika alipokuwa bado katika cho cha Morogoro TTC hakuwa na nia ya kutafuta mchumba kwani haja yake ilikuwa ya kupendeza kila mvulana na alipopata mimba alijaribu kuavya mimba hiyo. Sifa za Rosa zilipoufikia utawala wa chuo, padri mmoja alitumwa aende kumwonyesha mwanga na alipofika alipata Rosa na kitabu cha mapenzi na vidonge vya kuzuia mimba. Rosa hakujali hata ujumbe wa padri, aliendelea na maisha yake ya umalaya. Vitendo hivi na dawa ambazo alikuwa anatumia, vinadhihirisha kuwa hakujali maisha yake. Sifa zake zilizidi kuharibika ilipojiingiza zaidi katika anasa na mapenzi ya kiholela. Wanafunzi wenzake katika chuo cha Morogoro walimhusisha na jina la kejeli lililoashiria kuwa alikuwa kama maabara ya majaribio ya kimapenzi, jambo lililodhalilisha utu wake na kuporomosha hadhi yake kijamii. Mwandishi anatueleza kuwa alilala na mkuu wa chuo Bwana Thomas chumbani kwake baada mkewe kusafiri.

Hali hii inajitokeza pia katika riwaya ya *Kichwamaji*, ambapo mwandishi amemsawiri Kazimoto kuwa mwasi wa utamaduni na misingi ya maadili katika jamii yake. Shujaa pwaya, Kazimoto na Manase katika riwaya ya *Kichwamaji* wametawaliwa na ubinafsi ambao unaathiri maisha ya wahusika wengine. Kazimoto aliwachezea wasichana wengine kihisia ilihali hakuwa na nia ya kuwaoa kwa mfano Vumilia. Vumilia alikuwa na matumaini kuwa mapenzi yake na Kazimoto yatawafikisha kilele cha kuoana. Matumaini yake yalifika mwisho aliposkia kuwa Kazimoto anapanga kumwoa Sabina nduguye Manase ndiposa akatamauka na kusema kuwa hana umuhimu katia dunia na akaamua kuenda mjini na kuolewa na Moyokonde.

Usherati na uzinzi ni uozo ulioshamiri katika jamii hii na unawekwa wazi na Kazimoto na wahusika wengine wanapotagusana nao. Kwa mfano Kazimoto anapokutana na Vumilia ambaye hakuwa ameolewa, wanazini. Kitendo hiki kilitendwa mara kwa mara na Kazimoto na Vumilia hadi ulifika wakati Kalia anaanza kuwa na hisia ambazo zilimpelekea kutaka kubaka msichana aliyekuwa anachunga

ng’ombe. Tegemea aliposikia kuwa Kazimoto amekuwa anatoka na vumilia, alileta ugomvi kwa mji wa Mzee Mafuru ili aweze kumwonya Kazimoto:

> *“Jibu lako nalifahamu, Kazimoto, mambo ya wasichana yamekuingilia vile kwamba watu wa nyumbani umewasahau.’’ “Unasema nini? Mtoto gani wewe? Unataka kunidanganya mimi? Kazimoto uongo huu wote ulipata wapi? Unafikiri mimi sikukuona unanyatia mihogoni?”* (uk 36)

Kazimoto akiwa kwa mji wa Tegemea kumchukua Vumilia wakati wa usiku, walisikia Mzee Kabenga akiongea chumbani mwa Tegemea kuonyesha walikuwa na uhusiano. Pia Kazimoto anakumbuka maneno ya Kalia alipomwambia kuwa alimsikia Kabenga akiomba Tegemea ruhusa na msamaha wa kuingia kwake kwa sababu alikuwa amefurushwa kisha hakumletea Tegemea pesa za kutosha.

Kuzini kwa Kalia kulianza baada ya kujionea na kujifunza kutoka kwa Kazimoto na Kabenga, ndio maana anajaribu kubaka msichana aliyekuwa anachunga ng’ombe kwani alihisi ni kawaida kufanya hivyo. Hakuachia hapo hata baada ya kuonywa na kupigwa na Kazimoto, aliendelea kuzini hadi anamwibia babake pesa ili ampelekee Tegemea ambaye walikuwa wakizini pamoja. Pia, alianza kuhangaisha wasichana na wanawake kijijni hadi akaitwa mwehu na babake na kuuawa na wanakijiji alipofumaniwa akizini.

Tumaini amesawiriwa na mwandishi kuwa mwasi wa utamaduni na maadili katika jamii yake. Mwandishi anaeleza kuwa Tumaini alianza kunywa pombe kali akiwa kijijini Bugolola hata alipohamia mjini Shinyanga, aliendelea na kunywa pombe kali ambapo alikuwa kunywa katika baa moja inayoitwa *Africans’ Royal Bar.*

Ulevi wa Tumaini ulizidi hadi ukaanza kuleta athari kwake na kwa wahusika wengine waliotagusana naye. Tumaini alibadilisha na kuchezea wanawake anapokuwa mlevi na kuzini nao hata wakati mwingine hao wanawake walipanga jinsi ya kupata pesa kutoka kwake kama vile Kristina. Ukware ulitokana na ulevi ambapo Kristina anamchukua Tumaini kwake wakati ambapo bwanake alikuwa ashatoka na ameenda:

Mount Kenya University

> "*Tumaini alimshukuru sana mwenye baa kwa wema wake. Kristina alikunywa zile mbili zingine. Chupa hizo ndizo zilizomfanya Tumini aanze kupoteza fahamu zake. "Mimi nyumbani kwangu sina nafasi," Tumaini alisema. "Tutakwenda kwangu. Ni mbali kidogo. Itakuwa lazima tuchukue teksi."* (Uk. 95)

Biashara haramu inayofanywa na wanawake ambao mwandishi anaeleza kuwa wanatumia wanaume walevi kama vitega uchumi. Mwandishi anatupa taswira ya wanawake wanavyovutana kwa sababu ya Tumaini kwa kuwa alikuwa na pesa. Mwanamke mmoja kwa jina Fatuma, anawashawishi wenzake na kuwaambia kuwa hakuna haja ya wao kuvutana kuhusu Tumaini kwa vile hawatapata kile ambacho wanataka. Wanawake hao wanadai kuwa ni Tumaini ndiye uwezo wa kutoa pesa nyingi na yule mwenzio wa kuleta ushindani hataruhusiwa kupata pesa hizo pekee yake. Maneno ya hawa wanawake na wasichana yanaonyesha kuwa kuna biashara ya kujiuza ili wapate pesa katika vyumba vya ulevi, kwa hivyo ulevi umechangia biashara hii.

Kufilisika kwa Tumaini ni kwa sababu ya ulevi na kutumia pesa zake kwa wanawake akiwa vyumba vya ulevini. Alitumia mali na pesa alizoachiwa kama urithi na wazazi wake vibaya baada ya kifo cha babake na mamake. Tumaini anamwambia Kristina kuwa alipewa jina 'Jingojango' kwa sababu hapo zamani alikuwa na pesa si kama wakati huu, kumaanisha kuwa alikuwa amefilisika. Pia wanawake wengine kama Fatuma wanasema kuwa Tumaini ndiye anaweza kutoa pesa nyingi baada ya wao kuvutana kuhusu ni nani atakayefaidika wakati Tumaini anatumia pesa zake kwa ulevi na anasa zingine.

### 4.3.2 Shujaa Pwaya anatilia shaka na Kushuku Taasisi na Amali za Kijamii

Shujaa pwaya anasawiriwa kama mtu anayetilia shaka taasisi na amali za kijamii zilizojengeka katika imani na maadili ya kitamaduni. Shujaa pwaya hatambui wala hatii mamlaka ya taasisi za kisiasa, kidini na zile za kijamii na kiuchumi. Hathamini taasisi hizo hata kama zina mamlaka ya jamii, serikali na dini.

Mwandishi amemtumia Rosa kuonyesha jinsi shujaa pwaya anatilia shaka na kushuku taasisi na amali za kijamii kama vile shule na jamii. Baada ya kuanza kuvutiwa na wavulana ambao Rosa alikuwa ameonywa kuwahusu na babake, alianza tabia ya kulala mjini kama wasicha wengine. Tabia hii

hakurusiwa shuleni na walikuwa wameonywa na masista. Sista John alipovumbua kuwa Rosa analala mjini, aliambiwa kuwa atapelekwa nyumbani kama sheria ilivyo na kuwa atarudi kufanya mtihani wake.

> *"Deogratias! Deogratias! Rosa, tumekusudia kukupeleka nyumbani. Utarudi tu kufanya mtihani wako wa Cambridge."*

Kwa upande wake, Kazimoto alilelewa katika jamii inayothamini heshima, ukarimu na ushirikino ndiposa jamii inawajibika katika malezi na kuyafanya yawe ya ushirikiano. Kazimoto alipotoka nyumbani bila kujulisha mamake, alianza kutafutwa na mamake na hali hii inaleta wasiwasi nyumbani. Aliporudi, mama alijaribu kumuuliza alikoenda na mbona hakumwambia kuwa atatoka, Kazimoto alimjibu kwa ukali. Tabia hii ya ubishi katika jamii na watu waliokuzidi kwa umri inaashiria kukosa heshima ndio maana Kazimoto anaitwa katika kikao na kuonywa na kuelekezwa.

Kifo cha Rukia kilimghadhabisha Kazimoto ambaye alimlaumu Manase kuwa ndiye chanzo cha kifo chake. Kazimoto anaona kuwa Manase alimharibia Rukia maisha yake kwa kumpachika mimba na kukataa kumwoa. Kutokana na hili, anaamua kulipiza kisasi kwa kuchoma nyumba ya akina Manase. Mwandishi anaeleza kuwa Kazimoto alikuwa na hisia kinzani kuhusu kuendelea kulipiza kisasi katika familia hii:

> *"Wazo jingine sasa lilinijia kichwani. Nilikwenda nyumbani kwetu; niliingia ndani ya nyumba yangu kwa mlango wa nyuma. Nilichukua kibiriti nilikiwasha; kugusa tu majani, nyumba ilianza kuungua."* (Uk. 88)

Katika riwaya ya *Dunia Uwanja Wa Fujo*, wandishi anamsawiri Tumaini kama mtu anayeshuku sheria ambayo iliwekwa na viongozi katika taifa. Mwandishi ameonyesha jinsi shujaa pwaya anashaka na amali ya jamii kupitia kwa Tumaini. Jamii yake ilithamini sana ndoa za kupangwa na wazazi. Tumaini ametoka katika familia ambayo inafuata na kuthamini nguzo za utamaduni. Kapinga ambaye ni babake Tumaini alipokuwa akimwoa Muyango, walitumia utaratibu wa kitamaduni uliowekwa na jamii. Tumaini anapokuwa mtu mzima anaona utamaduni huu kama wa kipuzi ndiposa anaushuku na kuamua kufanya vile anavyotaka. Aliposikia kuwa Anastasia amepangiwa kuozwa kwa mzee na wazazi wake, anapanga

njama ya kumtorosha. Tumaini alipanga kumtorosha Anastasia kutoka kijijini kuelekea mjini Shinyanga ambapo wanajificha na kuishi ili wasijekujulikana na Anastasia asije akaolewa na mzee.

Baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha ambalo liliathiri Tumaini na matajiri waliokuwa na mali, Tumaini aliingiwa na roho ya unyama. Mali ambayo Tumaini alikuwa ametengeza kutokana na badiliko lake ya kitabia inatishiwa kutwaliwa na serikali. Tumaini alikuwa ni mmoja wa matajiri waliozalisha mali kutokana na kilimo na ufugaji wa wanyama kama vile ng'ombe wa maziwa. Alikasirishwa na tangazo hilo la Azimio la Arusha lililomfanya kumuua mkuu wa wilaya kwa sababu ndiye aliyetoa tangazo hilo.

### 4.3.3 Shujaa pwaya kama Mwanaharakati mwenye Fikra za Kimapinduzi zinazobomoa Nguzo na Mifumo ya Kimapokeo

Shujaa pwaya amesawiriwa kama anayeamsha harakati za kifikra zinazobomoa mfumo wa maadili wa kimapokeo na kaida zake. Anohoji manufaa ya mifumo hiyo katika jamii. Anauliza maswali magumu kuhusu nguzo, imani na mifumo ya kihafidhina kuhusu maadili, utamaduni na amali za jadi katika jamii yake.

Mvutano kati ya Zakaria na Rosa unaanza baada ya Zakaria kupata habari kuhusu tabia za ukware za Rosa. Zakaria alipojaribu kumkanya, Rosa alipandwa na hasira na kumrushia babake maneno. Mvutano huu unaonyesha kuwa Rosa ameharibu misingi ya malezi iliyowekwa na hivyo anapinga na hataki kuongozwa na babake. Tabia yake ilikuwa ya kuenda na mwanaume yeyote kwa mfano Thomas ambaye ni mwalimu mkuu ambapo jambo hili lilimkera Zakaria na kumfanya ugomvi uliomfanya Rosa kutoa maneno makali mdomoni na kusema kuwa yeye si babake naye Zakaria akamjibu kuwa pia yeye si bintiye:

> *"Kila wakati unatuchunga. Unafikiri utatuoa wewe!" Rosa mwishowe aliyasema yale maneno. Maneno aliyopaswa kusema siku ile aliyopigwa Zakaria, kutunza heshima yake, alifunua mdomo. Maneno fulani yalimtoka mdomoni mwake. "Tangu leo wewe si mtoto wangu." "Tangu leo wewe si babangu." Rosa alidakia bila kukawia.* (uk 58)

Rosa alizidi kuvuruga amani iliyoko hata katika ndoa za wengine. Mke wa Thomas ambaye ni mwalimu mkuu wa shule wanavutana na Rosa kwa sababu Rosa alikuwa anazini na Thomas. Rosa alikuwa mkware hivyo alimtafuta Thomas na wakaelewana kuwa wataenda kwa Thomas. Nyumbani mwa Thomas, Rosa alikunywa sana hadi kujitambua kukawa shida na hapo ndipo Thomas alichukua nafasi ya kuzini na Rosa. Rosa walipofumaniwa na mkewe Thomas, aliumwa na kukatwa sikio na mkewe Thomas kwa kuzini na mumewe.

Kazimoto katika riwaya ya *Kichwamaji* ametawaliwa na ubinafsi ambao unaathiri maisha ya Vumilia. Kazimoto aliwachezea wasichana wengine kihisia bila kuwa na nia ya kuwaoa kama vile Vumilia. Vumilia alikuwa na matumaini kuwa mapenzi yake kwa Kazimoto yatawafikisha kilele cha kuoana. Matumaini yake yalifikia mwisho aliposikia kuwa Kazimoto anapanga kumwoa Sabina dadake Manase ndiposa akatamauka na kusema kuwa hana umuhimu katika dunia na akaamua kuenda mjini na kuolewa na Moyokonde. Maisha ya Vumilia yalionyesha hali ya kutamauka baada ya kudanganywa na Kazimoto. Matarajio yake ya kuolewa na kuishi maisha mazuri yalifikia kikomo.

Baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha ambalo liliathiri Tumaini na matajiri waliokuwa na mali, Tumaini aliingiwa na roho ya unyama. Mali ambayo Tumaini alikuwa amekusanya kutokana na kilimo na ufugaji wa wanyama kama vile ng'ombe wa maziwa ilikaribia kutwaliwa na serikali. Tumaini alikerwa na tangazo hilo la Azimio la Arusha. Hali hii ilimsukuma kumuua mkuu wa wilaya kwa sababu ndiye aliyetangaza taarifa hizo. Alijiuliza maswali mengi kuhusu tangazo hilo na kutaka tangazo hilo lifutiliwe mbali kwani aliona kuwa litamzuia kufanya mipango yake:

> *"Siwezi kutukanwa na mwanasiasa anayetegemea kura yangu! Haiwezekani! Kuniambia mimi "Mnaliona hilo; haya ndiyo manyonyaji haya!" Mimi Tumaini! Mimi sikumkataza kunenepa! Na hata hivyo ninakula jasho langu. Tabu niliyopata. Haiwezekani! Potelea mbali vijiji vyao vya ujamaa ambavyo vimerudisha nyuma maendeleo ya watu wengi. Haiwezekani!* (uk 120).

### 4.3.4 Shujaa Pwaya anakubali Kifo kama Sehemu ya Maisha

Shujaa pwaya anakikubali kifo kama sehemu yake ya maisha. Mhusika huyu anatafakari mustakabali wa maisha yake na kuamua kujiua. Maisha hayana thamani nacho kifo ni kinaonekana kuwa sehemu ya

maisha kwake. Kwa mfano, maisha Rosa yanachukua mkondo mwingine baada kuhisi kusalitiwa na mpenzi ndio maana anakata tamaa na kujiingiza katika ukware bila kujali athari zake. Shuleni aliitwa 'maabara' kwa kuwa kila mwanaume alimfanyia majaribio ya kimwili. Kwa mfano; Thomas ambaye ni mkuu wa shule pamoja na Deogratias wanakuwa na usuhuba wa kimapenzi wa muda mrefu bila kuwa na nia ya kumuoa. Kutamauka kwa Rosa kulimfanya warushiane maneno na Zakaria ambaye ni babake kwa kuwa alifikia kilele cha kuharibika na akajiona kama kwamba hakuwa na thamani yeyote. Pia anakata tamaa anapopata barua kutoka Charles na kugundua kuwa Charles hakumpenda. Masaibu yanaongezeka anapopata habari kuwa babake na mamake wameaga dunia. Isitoshe, anajulishwa kuhusu kifo cha dadake kutokana na mshtuko alioupata kuwa mumewe aliaga dunia. Rosa anachukua hatua ya kujiua kwa kuvunja chupa na kuisiaga na kumeza vipande alipoona kuwa hakuna haja ya kuishi tena:

> *"Rosa aliona ulimwengu wote ukimwonea huruma, lakini sasa aliona kama Kwamba ulimwengu wote ulikuwa ukimchekelea. Kuishi aliona hawezi."* (Uk. 90)

Maisha ya Kazimoto yalianza kukumbwa na shida baada ya kifo cha dadake, mamake na mtoto wake. Alianza kujiuliza maswali mengi kuhusu kifo na mbona kifo kiwepo. Mvutano wa mawazo akilini mwake kuhusu kuwapo Mungu ama kutokuwepo Mungu na kwa nini aruhusu kifo kwa binadamu ulifurika akilini mwake. Mjadala huu anaupeleka kwa Manase ambaye pia haelewi kwa nini kuwe na kifo. Baada ya mkewe kuzaa mtoto aliyekuwa na kichwa kubwa na kisha kuaga, aliona hamna haja ya kuishi duniani ndiposa akaandika ujumbe katika kijikaratasi na kuacha kwa meza:

> *"Nimejiua. Siwezi kuendelea kuzaa kizazi kibaya. Pia sikuona tofauti kati yangu na mdudu au mnyama. Akili! Akili! Akili ni nini? Pia nikiwa duniani sikupata kukutana hata siku moja na mtu anayeaminii kwamba kuna Mungu. Watu wanaoogopa kufa na kwenda. Mimi kabla ya kufa, ninaungama mbele ya ulimwengu kwamba nilimwua mdogo wangu ingawa sikumgusa."* (Uk. 195)

Tangazo la Azimio la Arusha lilimkera Tumani ambapo aliona viongozi na wengine waliolitegemea kuwa walafi wanaotaka kuwanyanganya wenye bidii mali yao. Tumaini hakuona haja ya Azimio hilo kutekelezwa kwa kuwa wengine walikuwa wazembe na kazi yao ilikuwa ni mvinyu tu akiwa anatengeneza mali. Maneno ya mkuu wilaya, Tumaini aliyaona kama matusi kwake ambapo alimtusi

kuhusu unene ndiposa akaamua pia kupanga njama ya kumuua. Hakujali kuwa njama hiyo itasababisha kifo na wala hukuogopa kifo ila kukiona kuwa kawaida.

> *"Ukirudi. Wambie nitawakumbuka daima. Wambie nitakufa. Lakini nitakufa kiume. Sitatoa hata chozi moja. Wambie sina masikitiko kwa jambo nililolitenda. Nitakufa na heshima yangu. Kama nlifanya kosa vizazi vijavyo vitaamua."* (uk. 130).

### 4.3.5 Shujaa Pwaya kama Kiumbe Dhaifu asiye na Uwezo wa Kuzikabili Changamoto za Maisha

Shujaa pwaya wa kisasa amesawiriwa akiwa dhaifu, asiye na uwezo, madaha, mbwembe na mvuto wa shujaa wa kimapokeo. Hana ufanisi wowote katika matendo yake katika jamii. Kezilahabi amemsawiri shujaa pwaya kama asiye na uwezo wa kuzikabili vilivyo changamoto zinazoibuka katika jamii yake. Maisha yake yanapogubikwa na changamoto nyingi, shujaa pwaya anakimbilia ngome ya nafsi yake na kujitenga na wanajamii wenzake. Katika hali hiyo, shujaa pwaya anafadhaishwa na kudumazwa kinafsi. Hali ya kujitenga inamkengeusha na kumpooza katika mahusiano yake na jamii nzima. Katika ubinafsi wake, anaporomoka kiafya na kiakili na kuanza kuwaza kuhusu mauti kwenye upweke unaomzingira.

Mwandishi anasawiri hali hiyo kupitia kwa shujaa pwaya ambaye ni Rosa. Rosa anakata tamaa katika maisha yake pamoja na baadhi ya wahusika wengine kwa mfano anapopata habari kuwa Deogratias alikuwa na wanawake wengine, anakata tamaa kuhusu mapenzi ya dhati na kuchukua hatua kumwacha na kuelekea Mwanza ulevini kumaliza upekwe unaomkabili. Akiwa Mwanza, anajiingiza katika ukware na ulevi ili aweze kukabiliana na kujisahaulisha mawazo kuhusu uchumba wake kwa Deogratias aliyemsaliti na kumlaghai kimapenzi. Shuleni, alijulikana na kubandikwa jina kuwa yeye ni 'maabara' kwani kila mwanaume alimfanyia majaribio ya kiashiki. Kutamauka huku kulimfanya arushiane maneno na Zakaria ambaye ni babake kwa kuwa alifikia kilele cha utovu wake. Pia anakata tamaa anapopata barua kutoka Charles na kugundua kuwa Charles hakumpenda. Masaibu yanaongezeka anapopata habari za tanzia kuhusu kifo cha babake, mamake na dadake aliyeaga dunia kutoka na mshtuko alioupata kuhusu kifo cha mumewe. Rosa anashindwa kuhimili matukio hayo, hakuona haja ya kuishi tena duniani.

Matumaini ya Tumaini yanafikia mwisho aliposkia tangazo la mkuu wa wilaya kuhusu umiliki wa mashamba katika tangazo la Azimio la Arusha. Katika tangazo hilo, yeye na matajiri wengine wenye umiliki mkubwa wa mashamba wangepoteza mashamba hayo ambayo yangetwaliwa na serikali. Tumaini anapoteza matumaini na kujawa na hamaki ilioyomsukuma kutenda unyama ambapo alimuua mkuu wa wilaya aliyetangaza habari hizo. Baada ya kifo cha mkuu wa wilaya, Tumaini alikamatwa na kuhukumiwa kifo.

Kwa upande mwingine, katika riwaya ya *Kichwamaji* utamaushi wa unabainika matumaini ya Kazimoto ya kutafuta kazi yalipofikia mwisho akiwa ofisini mwa Manase kwa kuwa alikuwa ameona dalili ya Salima kupata kazi kwa sababu alikuwa mpenziwe Manase. Kazimoto anakabiliana na hisia hasi kwake Manase katika ofisi ya Manase baada ya kuona kuwa hangepewa kazi hili linazidisha chuki kwake. Kazimoto na Manase wanaonekana kuwa na hisia za utamaushi wanapokuwa wakijadiliana kuhusu kuwepo kwa Mungu na sababu gani zilizosababisha kifo. Wanajiuliza maswali haya kwa ghadhabu. Utamaushi unazidi kumtawala Kazimoto baada ya kifo kilichompata Rukia akiwa anajifungua na pia kutokana na kifo cha mtoto wao na Sabina Isitoshe, anajilaumu kwa kusababisha kifo cha Kalia. Kazimoto anatamauka na kuona hakuna haja ya kuishi tena.

### 4.3.6 Shujaa Pwaya anasitasita Kufanya Uamuzi kuhusu Masuala ya Kimsingi Maishani

Ziolkowski (2004) anaeleza kuwa shujaa pwaya husitasita kufanya uamuzi kuhusu masuala ya kimsingi yanayohusu maisha yake. Hukabiliwa na upungufu wa kutoweza kufanya uamuzi kutokana na mashaka mengi moyoni. Mhusika huyu hana uwezo wa kuchagua baina ya mambo mawili au hali mbili zinazomtatiza. Aidha, Shujaa pwaya yumo katika jamii iliyoparaganyika na kusambaratishwa na ugomvi wa kijamii, mafarakano na mizozo isiyoisha baina ya watu. Jamii yake ina maadili yanayokinzana pamoja na kuwepo kwa migogoro ya kitamaduni. Hali hizi zinachangia kujenga mhusika ambaye ni mwasi, mbishi, mgomvi, mpinzani na asiyepatana na wanajamii wenzake. Hii ndiyo hulka ya shujaa pwaya.

Uamuzi wa Rosa kuingia katika uhusiano alionywa na kukatazwa na Zakaria unampelekea kukosana naye. Zakaria na Rosa wanazozana baada ya Stella kumwambia zakaria kuwa Rosa alipewa barua na pesa. Zakaria alipojaribu kumwomba Rosa barua hiyo, aliitia mdomoni na kuitafuna. Kitendo hiki kilimkasirisha zakaria na kuamua kumpiga Rosa ilikumkomesha tabia yake. Alichukua pesa alizokuwa ameletewa na Charles na kumrushia chini pesa hizo na kumwambia aondoke. Rosa alipigana na msichana mmoja ambaye walisoma naye shule kwa sababu ya kuwa majina yao yaliandikwa na Rosa kwa wale walikuwa wametoroka shule kuenda mjini kwa densi. Msichana huyo alimlaumu Rosa kwa kusababisha kufukuzwa kwao shuleni ndiposa wanapokutana sokoni wanapigana. Walibururana kule sokoni huku wakishikana na kuangushana chini wakiangaliwa na watu kule sokoni.

Kazimoto alianza kuwa na mazoea ya kutoka usiku wa giza kuenda kumchukua Vumilia kutoka kwao wakiwa na Kalia, jambo lilipomfikia Tegemea, alikasirika na kuamua kupeleka ugomvi kwa mji wa Mzee Mafuru. Tegemea alipompata Mzee Mafuru, alitoa onyo ili Kazimoto aonywe. Mvutano kati ya Manase na Kazimoto ulitokana na Rukia kuharibiwa maisha na Manase, jambo ililomfanya Kazimoto kughadhabishwa na kuamua kulipiza kisasi kwa familia ya manase ndiposa anachoma nyumba na hata kumua pia kumharibu Sabina. Kitendo cha kumharibu Sabina hakukufaulu kwani Kazimoto alibadilisha nia na kumuoa. Pia Kazimoto anakumbana njia mbili katika fikra zake. Kazimoto alimfanya kubadili nia ya kutaka kulipiza kisasi kwa familia ya akina Manase kwa kuwa na hisia na mapenzi kwa Sabina nduguye Manase. Kazimoto alijawa na mawazo kuhusu vifo vilivyotokea kwa jamaa yake ndiposa akaleta mjadala kuhusu kuwepo kwa Mungu na kutokuwepo kwa Mungu. Alijiuliza, kwa nini Mungu akamcha binadamu akafa au akapitia mateso ya ulimwenguni?

Maadili ya Tumaini kajijini hayakuwiana na wanakijiji ndiposa anamua kutoka kwa kijiji na kuelekea mjini ili aweze kupata nafasi na wakati wa kufanya vitendo vyake. Tuamaini akiwa kijijini alianza kunywa pombe na kujihusisha katika uzinifu. Pia kunapotokea mgogoro wa kisiasa uliosababisha kifo cha mkuu wa wilaya kwa kutangaza tangazo la serikali kuwa kutakuwa na Azimio la Arusha. Tumainia

anaonekana kukerwa na tangazo hili la Azimio la Arusha ambalo liligusa waliomiliki mashamba na kuwa na mali kiasi fulani. Tangazo hili lilipeleke kifo cha mkuu wa wilaya ambaye aliuawa na Tumaini naye kuhukumiwa kifungu cha maisha gerezani.

### 4.3.7 Mfuasi wa Mkondo wa Mawazo unaotafuta Ukweli kwa Undani

Shujaa pwaya amesawiriwa kama mtu wa kupenda kuandama ukweli alioubuni yeye mwenyewe. Daima ni mfuasi wa mkondo wa mawazo unaotafuta ukweli kwa undani. Jamii pana humkejeli na kumdhihaki shujaa pwaya kutokana na udhaifu wake, uovu wa matendo yake na ufasiki wake. Hata hivyo, shujaa pwaya hadhibitiwi wala kuzuiliwa na upungufu huo wa hulka yake. Upande wa msimamo, shujaa pwaya huepuka hukumu na tuhuma za wanajamii ambao humtazama kwa jicho moja tu, yaani lile la kimaadili pekee. Japo shujaa pwaya kukosa ufanisi, umahiri na uhodari, hakumaanishi kuwa yeye si shujaa (Torrence, 1978). Ushujaa wake huonekana pale anapoonyesha ukakamavu na kutotetereka katika hali zinazomshinikiza kushindwa.

Zakaria anaposkia kuwa kuna vijana wameanza kumtafuta na huwa wanamletea Rosa barua, aliwashika na kuwapiga hadi wakabadilisha na kumwambia kuwa wanatafuta mayai wanunue. Zakaria hakutaka wasichana wake waanze mapenzi na wavulana kwa kuwa aliona hiyo ndio njia ya kuwalea. Mvutano huu ulikuwa kwa ajili ya shujaa pwaya ambaye ni Rosa Mistika kwani vijana Tabia hii ya Rosa Mistika iliendelea bado katika chuo cha Morogoro TTC hakuwa na nia ya kutafuta mchumba kwani haja yake ilikuwa ya kupendeza kila mvulana na alipopata mimba alijaribu kuavya mimba hiyo. Sifa za Rosa zilipomfikia padri, padri mmoja alitumwa aende kumwonyesha mwanga na alipofika alipata Rosa na kitabu cha mapenzi, vidonge vya kuzuia mimba, Rosa hakujali hata ujumbe wa padri, aliendelea na maisha yake ya umalaya. Vitendo hivi na dawa ambazo alikuwa anatumia, inadhihirisha kuwa hakujali maisha na sifa zake kuharibika ila kuingia katika anasa ya mapenzi ya kiholela. Wanafunzi katika chuo cha Morogoro walimpa jina ambalo lilimaanisha kuwa yeye ni mahabara ya kufanyia majaribio ya

kimapenzi. Mwandishi anatueleza kuwa alilala na mkuu wa chuo Bwana Thomas chumbani kwake baada mkewe kusafirihao walikuwa na mtagusano na Rosa.

Kazimoto alizoea tabia kuenda usiku kumchukua Vumilia kutoka kwa hata ingawa jamii haikurusu. Kitendo kinapovumbuliwa na Tegemea, anajawa na amaki ambapo alielekea mji wa Mafuru kumfahamisha. Pia Tegemea hakumfahamisha tu alifoka na kumwonya Kazimoto achane na Vumilia. Onyo hii haikuchukuliwa maanani na hata hivyo alikuwa ashaonywa na Mafuru kuhusu wasichana. Kalia ananza kuzini baada ya kujionea na kujifunza kutoka kwa Kazimoto na Kabenga, ndio maana anajaribu kubaka msichana aliyekuwa anachunga ng'ombe kwani alihisi ni kawaida kufanya hivyo. Uk. 80.

> "*Mbona wewe huwa unafanya. Mimi sijasema lo lote hata kwa baba. Leo nafanya unapiga. Kwa nini? Unanionea tu. Unafikiri mimi mjinga kuwa natazama tu?"*

Anastasia na Leonila wanapigana kwa sababu ya husiano wao kwa Tumaini ambapo Leonila hakufurahia husiano uliopo wa Anastasia na Tumaini. Leonila anamshika na kumwangusha chini na kuvutana kwa muda mrefu huku wakiraruriana nguo karibu wakaa uchi na inatokea Leonila anashindwa ndiposa anamwita Anastasia aje amsaidie. Tumaini alikuwa anawachezea hawa wasichana kihisia ndiposa walipojua kuwa kuna husiano, walianza mvutano. Wivu wa Anastsia kuhusu wasichana waliomtaka Tumaini wakiwa katika maeneo ya pombe, hukumzuia kuwaona kuwataka wasichana hao kama vile Hadija na Kristina. Vitendo vya wasichana hawa vina mkera Anastasia hata hivyo Tumaini anaendelea na vitendo hivo licha ya kumkera Anastasia

### 4.3.8 Kiumbe aliyegubikwa na Unyume na Kinaya

Shujaa pwaya amesawiriwa kuwa dhaifu, hafifu, asiyejiamini, mwenye fedheha na asiye stadi wala makini katika mambo anayoyatenda. Matendo yake huonyesha kinaya au kinyume cha aina fulani. Hata hivyo, kuna wakati ambapo anaonyesha uthabiti, uimara na ushupavu katika matendo yake (Brombert, 1999). Hali hii inaonyesha kuwa licha ya udhaifu wa matendo yake, shujaa pwaya anaweza kuupiku upungufu wake anapopata uongofu au ufufuo.

Katika Nadharia ya Vifani, Northrope (1957) anaainisha bunilizi katika makundi saba. Makundi hayo yanajumuisha: visasili, bunilizi za kilimbwende, tendi, bunilizi za muhakati wa juu na wa chini, tanzia na kinaya. Katika uanishaji huo, Northrope anatumia kigezo cha uwezo wa shujaa kutenda matendo mbalimbali. Uwezo huo unaweza kuwa wa kiwango cha juu au cha chini. Kwa mujibu wa Northrope, shujaa wa visasili, bunilizi za kilimbwende na tanzia ana uwezo wa juu wa kutenda. Uwezo wa shujaa huyo wa kutenda unapiku ule wa binadamu wa kawaida. Shujaa wa aina hii ametunukiwa uwezo usio wa kawaida unaomfanya kuenziwa. Shujaa wa muhakati wa chini husawiriwa katika bunilizi za uhalisia pamoja na futuhi. Mhusika huyu ni binadamu wa kawaida tunayetangamana naye katika shughuli za kila siku. Tunapokumbana naye katika bunilizi, humwona kuwa mmoja wetu katika jamii. Tunaweza kujinasibisha naye kupitia kwa usawiri wake. Katika bunilizi za kinaya, shujaa tunayekabiliana naye ni dhaifu katika uwezo wa utendaji wake kuliko binadamu wa kawaida katika jamii. Tunapodadisi usawiri wa shujaa huyo tunapata kuwa amegubikwa na unyonge, utumwa, ufungwa na utamaushi. Kwa kuzingatia vigezo vya Northrope (1957) tunaweza kumwainisha shujaa pwaya katika kundi la kinaya. Unyume ni sehemu ya hulka ya shujaa pwaya. Shujaa pwaya huonyesha kinaya katika matendo yake kutokana na kuporomoka kwa jamii kimaadili, kuvunjika kwa misingi ya kitamaduni iliyothaminiwa na wanajamii na kuinuka kwa uozo uliokithiri. Uwezo wa shujaa pwaya kujithamini na kujiona bora umepondwa na mazingira dhalimu yanayomlea. Mazingira hayo najisi humwekea vikwazo vya kumdhibiti ambavyo humbadilisha shujaa pwaya na kumfanya abuni njia mbadala za kujihami ili ayakabili. Matokeo yake ni kuwa shujaa pwaya anageuka kuwa mwasi, mkiukaji na mwenye kisasi kwa jamii inayoingilia uhuru wake wa kibinafsi. Mwishoe, shujaa pwaya hujiponza na kujidhulumu kupitia kwa matendo yake mwenyewe.

Mwandishi anamtumia Rosa kinyume na matarajio ya wengi kwani alionekana kuwa jicho la familia yake. Mji wa Zakaria ulikuwa na matumaini kwa kuwa Rosa amewafungulia ndugu zake njia ya elimu ambayo jamii ilitumainia kuwa itainua hathi ya familia. Elimu hujulikana kama kifunguo cha maisha na

hata kusaidia mhusika katika kutegua kitendawili cha binadamu. Inakuwa kinaya kwa kuwa Rosa aliyepata masomo hasaa ya ualimu maisha yanamshinda kuyakimu. Rosa hakuweza kujizuia na kuwazuia wanaume kumtumia vibaya na pia kujizuia kutokana anasa.

Katika *Kichwamaji*, Kazimoto anayafumbua maisha kwa njia ambayo inatatanisha sana kwa watu. Kazimoto alipata elimu ya ambayo inawabadilisha maisha na kuwa na mtazamo tofauti na rika yao katika kijiji chao. Elimu alioipata Kazimoto ilimletea mabadiliko kimawazo na kimatendo ndio maana wanapojadili swala la kuwepo kwa Mungu au kutokuwepo kwa Mungu na swala la kifo, inaashiria kupata elimu fulani. Mwandishi anaeleza kuwa elimu hiyo haikumsaidia katika maisha yake ndio maana anafanya uamuzi mbaya katika maisha yake. Inakuwa kinaya pia kwa kuwa anafaa kuelekeza wenzake kama vile Kalia ilihali anampotosha kimaisha na kusababisha kifo chake.

Maelezo ya mwandishi kuhusu maisha kuwalemea shujaa pwaya katika Kichwamaji na Rosa Mistika, anatumia mbinu hiyo kueleza jnsi inakuwa kinyume kwa shujaa pwaya katika Dunia Uwanja wa Fujo. Anaeleza kuwa Tumaini ambaye alikuwa amesoma na alitarajiwa kufumbua fumbo la maisha na kwa kuwa aliapata maisha yakiwa hali isiyo mtatiza kiuchumi, yanamshinda. Mwandishi anasema kuwa hakuweza kujizuia kulipiza kisasi kwa mkuu wa wilaya. Masaomo yake hakumsaidia kujiondoa katika mitego ya sheria na kuwa alikuika sheria ambapo alisababisha kifo cha mkuu wa wilaya na kuhukumiwa kifo.

### 4.3.9 Shujaa Pwaya amesawiriwa kama Mtu anayefunga Safari ya Ndani ya Kujitambua

Kikale cha shujaa wa visasili vya kimajumui hufunga safari kwenye mchakato unaoanzia katika kugura, kisha anajivumbua au kujitambua na hatimaye kurudi kwao baada ya kupitia mateso na changamoto nyingi. Shujaa hupitia jasura yenye changamoto nyingi kisha hurudi akiwa mshindi (Campbell, 1949). Shujaa pwaya anapitia mchakato wa kitajriba ulio sawa na huo wa shujaa wa kimapokeo. Hata hivyo, mchakato wa safari ya shujaa pwaya ni tofauti kwa sababu ni wa ndani ya nafsi yake na usio na ufahari wala utukufu unaohusishwa na jasura ya shujaa wa kisasili. Kimsingi, safari ya nje inayofungwa na

shujaa wa kimapokeo inabadilika na kuwa safari ya ndani inayofungwa na shujaa pwaya. Safari yenyewe hufungwa katika nafsi au ulimwengu wa kiakili wa shujaa pwaya. Hali ya kujivumbua ya shujaa wa kimapokea inabadilika na kuwa tajriba na mafunzo mapya anayoyapata shujaa pwaya kuhusu udhaifu wake. Safari ya kurudi ya shujaa wa kimapokeo inabadilika na kuwa changamoto za kujitahidi kuishi kwa shujaa pwaya katika ulimwengu uliojaa vurugu na fujo. Shujaa pwaya anajifaragua na kujiimarisha ili akabiliane na changamoto za ulimwengu huo unaobadilika kwa kasi.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, mwandishi anaeleza kuwa shujaa pwaya alijaribu kujifaragua na kujiimarisha kimaisha kwa kutumia elimu ambapo ilimsaidia kuvuka daraja ya maisha. Pia anaeleza kuwa Rosa alifika mahali akaanza kutumia mbinuishi ilikujifaragua kwa mfano kuanza kutafuta wanaume ambapo atawatumia kukimu mahitaji yake. Tabia ilimfanya ajulikane kama chumba cha kufanyia majaribio na hata kumalizia kuvurugana na wengine walio katika ndoa.

Shujaa pwaya, Kazimoto na Manase wanapata Elimu ya ambayo inawabadilisha maisha na kuwa na mtazamo tofauti na rika yao katika kijiji chao. Elimu aliyopata Kazimoto ililetea mabadiliko kimawazo na kimatendo ndio maana wanapojadili swala la kuwepo kwa Mungu au kutokuwepo kwa Mungu na swala la kifo, inaashiria kupata elimu fulani. Elimu hii inaleta uwajibikaji kwa Kazimoto ambapo anaamua kumchukua Rukia ambaye ni dadake ili kufadhili elimu yake. Anampeleka kwa rafiki yake ambaye ni Manase ili aweze kuishi naye kwa muda hadi atakapo maliza masomo yake kwani alikuwa muhula wa mwisho katika masomo yake

Mwandishi Euprase Kezilahabi anaonyeha elimu katika mitazamo miwili kupitia shujaa pwaya ambaye ni Tumaini ambapo ameangazia kwa mtazamo wa kimagharibi na utamaduni wa Kiafrika. Elimu ya kimagharibi ilimwathiri Tumaini kwa njia tofauti ambapo ilimpa kuburi ambapo kilimfanya kuwahadaa wasichana waliokuwa hawajasoma. Tumaini alimlaghai Leonila na kumlazimisha kufanya mapenzi naye hata ingawa alikuwa amejitetea kwa kubainisha hila za vijana waliosoma. Pia kwa upande mwingine wa elimu, mwandishi anasawiri elimu kupitia kwa shujaa pwaya kuwa muhimu katika jamii na kuwa ndio

msingi wa maarifa tofauti tofauti. Dennis anatumika kama kielelezo anapomuuliza Tumaini kuwa usomaji wa vitabu ndio ulimpa hayo maarifa kuhusu maisha. Maarifa ya Tumaini yanatokea pale ambapo anasoma na kujibu wanaosoma gazeti kuhusu maisha. Isitoshe elimu ya maisha huwa haitaji vitabu ila tu busara alikuwa naye binadamu katika ndio maana wengine hushindwa kuthibiti utamaushi katika maisha ndiposa wengine hujitia kitanzi

#### 4.3.10 Mtu anayeelea katika Wimbi la Maisha bila Ridhaa wala Hiari ya Kibinafsi

Shujaa pwaya amesawiriwa kama mtu anayeelea katika wimbi la maisha linalomyumbisha bila ridhaa yake mwenyewe. Maisha ya shujaa pwaya yanadhihirika kupitia kwa hali tatu zinazotambulika bayana (Sartre, 1978). Kwanza kabisa shujaa pwaya anaonekana kuwa na uchovu wa kiakili '*ennui*' unaotokana na msururu wa changamoto za kimaisha zinazomwandama. Pili, shujaa pwaya anaishi maisha yaliyogubikwa na hofu kuu '*angst*' inayotokana na fadhaa ya mkururo wa mashaka yasiyoisha yanayomkumba. Aidha, shujaa pwaya anapatwa na mkengeuko '*alienation*' unaomsukuma katika mzingile wa nafsi yake. Shujaa pwaya anauona ulimwengu kama usiomjali na usiomhitaji kwa hivyo anauambaa na kujitenga nao. Anajifungia katika ngome ya nafsi yake. Hatimaye, shujaa pwaya anakosa msukumo wa ndani unaomchochea kufanya uamuzi wa haraka kuhusu changamoto zinazomkabili yaani '*abulia*' badala yake anasitasita anapofanya uamuzi huo. Neno la Kiingereza '*abulia*' linatokana na msamiati wa Kiyunani '*aboule*' ambalo lina mofimu mbili zilizoambatishwa. Mofimu '*a*' inamaanisha 'hali ya kukosa' nayo '*boule*' inamaanisha 'nia au msukumo wa kufanya jambo'.

Maisha Rosa yanachukua mkondo mwingine kwa kuhisi kuwa amesalitiwa na mpenzi ndio maana anakata tamaa na kujiingiza katika ukware bila kuajli sifa zake. Shuleni alijulikana na kubandikwa jina kuwa yeye ni mahabara kwani kila mwanaume alimfanyia majaribio ya kimwili mifano ni; Thomas ambaye ni mkuu wa shule na Deogratias. Kutamauka huku kulimfanya warushiane maneno na Zakaria ambaye ni babake kwa kuwa alifikia kilele cha kuharibika na hakuwa na thamana yeyote. Pia anakata tamaa anapopata barua kutoka Charles na kugundua kuwa Charles hakumpenda. Masaibu yanaongezeka

anapopata habari kuwa babake na mamake wameaga dunia kutoka na mshtuko alioupata kuwa mumewe aliaga dunia. Rosa anachukua hatua ya kujiua kwa kuvunja chupa na kuisiaga na kumeza vipande alipoona kuwa hakuna haja ya kuishi tena duniani.

> "*Rosa alipomaliza kukisoma kichwa kilimwanga. Aliona kizunguzungu. Jasho lilimtoka. Machozi yalimteremka mpaka kifuani. Rosa aliona ulimwengu wote ukimwonea huruma lakini sasa aliona kama kwamba ulimwengu wote ulikuwa ukimchekelea."* (Uk. 90)

Matumaini ya Kazimoto ya kutafuta kazi yalifika mwisho akiwa ofisini mwa Manase kwa kuwa alikuwa ameona dalili ya Salima kupata kazi kwa sababu alikuwa mpenziwe Manase. Kazimoto anakabiliana na hisia za Manase katika ofisini mwa Manase baada ya kuona kuwa hangepewa kazi ndiposa chuki kwake inazidi kukua. Kazimoto anakumbana njia mbili katika fikra zake ambapo zilimfanya kubadili nia ya kutaka kulipiza kisasi kwa familia ya akina Manase kwa kuwa na hisia na mapenzi kwa Sabina nduguye Manase. Kazimoto alijawa na mawazo kuhusu vifo vilivyotokea kwa jamaa yake ndiposa akaleta mjadala kuhusu kuwepo kwa Mungu na kutokuwepo kwa Mungu. Alijiuliza, kwa nini Mungu akamcha binadamu akafa au akapitia mateso ya ulimwenguni?

Matumaini ya shujaa pwaya yanafikia mwisho aliposkia tangazo la mkuu wa wilaya kuhusu umiliki wa mashamba katika tangazo la Azimio la Arusha. Tumaini aliona kuwa bidii aliokuwa ameweka kwa kujiinua inafika mwisho kwa kupitia njia za kukadamiza wenye bidi. Katika tangazo hilo, yeye na matajiri wengine wenye umiliki mkubwa wa mashamba wangepoteza mashamba hayo kwa serikali. Tumaini anapoteza matumaini na kujawa na hamaki uliomskuma kutenda unyama ambapo alimuua mkuu wa wilaya kwa kutangaza tangazo hilo. Baada ya kifo cha mkuu wa wilaya, Tumaini alikamatwa na kuhukumiwa kifo.

### 4.4 Ujumbe Muhimu unaowasilishwa na Shujaa Pwaya Katika Riwaya za *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Rosa Mistika* na *Kichwamaji*

Ujumbe ni wazo au maadili yanayofikishwa na mwandishi kwa msomaji au msikilizji kupitia hadithi, mashairi au kazi nyingine yoyote ya fasihi. Wazo au maadili haya yanaweza kuwa ya kisiasa, kifalsafa

au kijamii na ambapo huamsha hisia katika msomaji au msikilizaji na pia huweza hamasisha (Wamitila, 2017). Aya zifuatazo zinaeleza ujumbe muhimu unaowasilishwa kupitia kwa shujaa pwaya katika riwaya zilizochanganuliwa.

Mapenzi ni hisia na uhusiano kati ya watu. Uhusiano huu unaweza kuathiri mhusika katika maisha yake kwa njia tofauti. Kwa mfano, Rosa anajipata katika uhusiano wa kimapenzi na Deogratias aliyemsaliti na kumlaghai. Mapenzi haya yanamtamausha na kuanza kujihusisha kiholela na mwanaume yeyote aliyekutana naye.

Uongozi ni suala linalohusu viongozi na jinsi wanavyoongoza jamii na jinsi wanavyokabiliana na changamoto ambazo hukumba jamii kwa mfano ufisadi, uongozi mbaya na uongozi wa kimapokeo. Kwa mfano, Kazimoto anakosa kupata ajira kwa sababu ufisadi katika ofisi ya wilaya ambapo Manase alikuwa mkuu wa wilaya hiyo.

Haki na usawa ni maudhui yanayogusia haki za kibinadamu, usawa uliopo katika jamii na jinsi ya kupinga dhuluma au ubaguzi. Kwa hivyo kipengele hiki katika fasihi hutumika kuelimisha kuhusu umuhimu wa haki na usawa kwa kila mwanajamii. Wasichana walitiwa mimba Deogratias wanakosa haki kwa kuwa alitumia mamlaka yake kuwalazimsha kuavya mimba.

Mabadiliko ya jamii katika fasihi huonyesha mabadiliko katika; utamaduni, siasa na jinsi mabadiliko haya yanavyoshirikisha maisha ya watu, mila, na tamaduni. Tumaini anakosa kuelewa jinsi utadumi unavyokandamiza jinsia ya kike. Anakumbana na haya kupitia kwa Anastasia ambaye alikuwa mpenzi wake.

Ushujaa na ujasiri ni kule kujikakamua kutenda ama kusuluhisha shida ambayo jamii inapitia au mtu hupitia. Binadamu hukutana na changamoto kubwa na hupambana kushinda, wakiwa na sifa ya shujaa na ujasiri. Ujumbe huu huweza kuhusiana na vita, mapambano ya kijamii, au juhudi za kibinafsi za

kutafuta haki. Hamaki za Kazimoto zilimfanya kutafuta haki kwa njia ya kulipiza kisasi kwa familia ya Kabenga. Haki ambayo alikuwa anatufuta ni sababu ya Manase kumharibia maisha Rukia.

Mila na tamaduni ni vipengele ambavyo huzungumzia umuhimu wa tamaduni na mila katika jamii, pamoja na migogoro inayoweza kutokea kati ya mila za jadi na mabadiliko ya kisasa. Migogoro hii hutokea wakati utamaduni na mila ukinzana na mambo au mitazamo ya kisasa. Kwa mfano utamaduni wa kumchagulia mwanamke mume katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* unaleta utengano kati ya Mulele na Anastasia. Anastasia anatoroshwa na Tumaini ili asije akaozwa kwa Tembo.

### 4.4.1 Misingi ya Malezi na Mandhari ya Ulezi wa Mtoto

Malezi ni kazi au tendo inaoyofanywa kwa muda mrefu kwa binadamu ilikumsadia kukabiliana na maisha kwa jumla au sehemu yake ya maisha. Malezi ni kazi au tendo inaoyofanywa kwa muda mrefu kwa binadamu ilikumsadia kukabiliana na maisha  maisha.

Shujaa pwaya  ambaye ni Kazimoto ameonyesha malezi mazuri yaliyotekelezwa na wazazi wake kwa kushirikiana na jamii. Mzee Mafuru pamoja na mkwewe wanawajibika katika kuwalea watoto wao Kazimoto akiwa mmoja wao ndio maana anamsomesha na kumpa wosia kuhusu maisha na kutaka awajibike. Kazimoto anajitwika jukumu la kumsomesha Rukia ambaye ni dadake ndio maana anaghadhabishwa na kitendo cha Manase cha kumharibia maisha kwa kumtia mimba ambayo ilimfanya kushindwa na masomo.

Kupitia kwa Kazimoto, malezi yanasawiriwa kuwa ya ushirikiano ambapo watoto walipewa malezi na mtu yeyote katika. Tuza na Tegemea wanafika mji wa Mzee Mafuru kumsaidia Rukia kujifungua, kuonyesha kuwa ushirikiano ulikuwa katika malezi na walichukulia kuwa mtoto yeyote kwa jamii ni wao.

Kukutana katika kikao kwa familia ya Mzee Mafuru na Mzee Kabenga katika mji wa Mzee Mafuru ili kuzungumzia kuhusu matendo ya wanao ni ishara tosha kuwa malezi yalifanywa kwa pamoja na kwa

ushirikiano katika jamii. Kwa mfano, Kazimoto anapokosa kwa kuonekana na Vumilia, Tegemea anafika mji wa Mzee Mafuru kuripoti kisa hiki na kumwonya dhidi ya kutoka na Vumilia. Vikao viliwekwa na wazee wa kijiji kumwonya na kumrekebisha Kazimoto dhidi ya matendo yake ambao hayambatani na maadili ya jamii.

Mwandishi ameeleza kuhusu malezi ya baadhi ya  wahusika mmojao akiwa Tumaini na athari zake kwao na katika jamii. Wazazi wa Tumaini walionyesha kutepetea katika malezi kwa mwanao ambapo walimdekeza na kutompa mawaidha ya ku jenga katika maisha yake ndiposa anaacha shule kwa kuwa alikuwa na urithi wa wazazi hata kama mamake hakufurahishwa. Malezi haya mabaya ndiyo yalifanya awe na hisia na mtazamo tofauti kuhusu masomo yake na kutakia kifo wazazi wake ili aweze kubaki pekee yake wakutumia mali aliyoachiwa na wazazi katika ulevi na usherati.

Utepetevu katika malezi ya Tumaini waonekana pale ambapo alimchoma jicho mlezi wake na mlezi akampiga kidogo. Tumaini akimbia hadi kwa mamake na kuripoti ambapo mama alimfokea na kumdharau mlezi kuwa jicho lake halina tofauti na la ng'ombe. Uk. 11

> *"Kwa nini umempiga mtoto wangu!" Muyango alifoka. "Alikuwa karibu kunichoma jichoni!" mlezi wake alijibu. " Kuna tofauti gani kati ya jicho lako na ng'ombe! Usirudie tena kumpiga mtoto wangu kwa jambo dogo kama hili!"*

Kutoelekezwa vyema, Tumaini anatoroka kijijini kwa kukosa maadili ambapo aliona kuwa hawtaelewana na wanakijiji kwa mienendo yake potovu ndio anaend mjini ili awe huru wa kufanya mambo yake. Akiwa mjini alijiingiza katika starehe na anasa zote kama vile kuwatumia wasichana na kuwabadilisha vile anataka na kunywa pombe hadi akafilisika.

Kupitia kwa Tumaini, Kasala anawajibika kuwapa watoto wake malezi wanayostahili. Ndio  maana anamcharaza Leonila anapompata na makosa hadi Mugala ambaye ni mamake akajaribu kuzuia na kumsaidia. Mwandishi anaeleza kuwa Kasala alikuwa mkali hadi watoto wake walimuogopa ndio maana walijaribu juu chini wasipatikane kwa makosa hata Tumaini alimwogopa kwa ukali wake.

Wazazi wa Anastasia walimpa malezi aliyostahili hadi wakati mmoja kabla hajaolewa na Tumaini, walimchagulia bwana wa kumwoa na wakapanga ndoa yao. Jambo hili halikumfurahisha Tumaini na Anastasia ndiposa wanapanga na kutorokea Shinyanga siku ya arusi ya Anastasia ili asije akaolewa na mzee. Tamaa na ubinafsi wa wazazi wa Anastasia ndio unaonyesha kuwa wazazi wengine walitepetea katika malezi. Badala ya kumwongoza katika kuchukua hatua ya mkondo mwingine wa maisha, wao ndio wanamwaribia maisha ya kutaka kumuoza kwa mwanaume mzee ili wapate mali.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika* malezi yalikuwa na mitazamo tofauti; kuna waliotazama malezi ya kuwafungia watoto kuwa ndio malezi kamilifu katika jamii, na wengine waliona kuwapa uhuru watoto ndio malezi mema. Zakaria aliona kuwafungia wasichana wake ndio kulea au kuwapa malezi ndio maana Rosa anapopata nafasi na uhuru anamalizi kuwa mlevi na mkware. Zakaria hakuwapa wanawe ushauri kwa mfano Rosa ila tu alifika akiwa amelewa nyumbani na kuwapiga wanapokosea. Kupigwa kwa Rosa kunamfanya kuona maisha hayana maana ndiposa anaamua kumkana babake wanapovutana. Regina ambaye ni mamake Rosa alijaribu kuwashauri wasichana wake jinsi ya kuishi na kukabiliana na maisha ambapo ni tofauti na Zakaria ambaye ni mumewe. Hata baada ya kuskia fununu kuwa Rosa alikuwa na mimba na ashajifungu, alimwandikia barua na kumshauri pamoja na dadake namna ya kukabiliana ujumbe huo na maisha.

Mwandishi ametumia wahusika wengine waliotagusana na shujaa pwaya kuelezea malezi na jinsi yanavyoathiri shujaa pwaya. Kwa mfano Deogratias amabaye ni mkuu wa wilaya ni moja ya  wahusika waliotumiwa kuendeleza malezi yasiyostahili katika jamii. Badala ya kuwa mfano mwema kwa wasichana wadogo kama vile Rosa kwa kuwashauri au kuwapa wosia wema, ndiye anatumika kuharibu maisha yao. Mhusika mwingine ni Thomas ambaye ni mkuu wa shule, aliyetarajiwa kuwa na ushauri wema na kuwaelekeza vijana mifano ya Rosa na wengine kwa njia inayofaa, badala yake anawaharibu.

Malezi ya Rosa Mistika hayakuwa kamilifu au hakupata kuelekezwa katika jamii na wale waliotagusana naye kwa mfano wazazi wake na walimu kama vile Thomas. Aliathirika kwa njia hasi kwa kuwa

alipotoka kimaadili kwa kuwa alianza anasa potovu. Dhuluma na unyanyasaji wa kimapenzi ulimuathiri kisaikolojia, ulitoka kwa aliyewadhania kuwa wachumba wanamfanya kutamauka. Deogratias ambaye ni mkuu wa wilaya anamdanganya kimapenzi ambapo alikuwa na wapenzi wengi, na hivyo hakumthamini Rosa Mistika. Matendo haya ya Deogratias yanamfanya kufanya uamuzi potovu wa kuingia katika ukahaba badala kuongozwa vyema na Deogratias.

Mwandishi ameeleza vizingiti vya malezi kupitia shujaa pwaya Rosa Mistika na jinsi aliweza kukabiliana navyo. Kwa mfano kufungiwa kwake na kutoruhusiwa kutangamana na rika yake au kutoka nje kwa boma ya mzee Zakaria, pia kuelekezwa jinsi ya kuishi akiwa mbali na wazazi. Rosa alipokuwa shule ya Morogoro TTC anashtukia maisha ya kuishi mbali na wazazi na pia kutangamana na wavulana ambao alikatazwa na babake. Rosa alichukua nafasi hii kama uhuru alionyimwa na kujingiza katika anasa zilizomharibia maisha yake.

### 4.4.2 Usherati, Uzinifu na Ufasaki

Uzinifu ni tabia ya mwanaume au mwanamke kujiingiza katika vitendo vya kujamiana na wengine wasio katika ndoa na kiholela holela. Kitendo hiki kinawekwa wazi na shujaa pwaya, Mapenzi kiholela ni hali ya mtu katika jinsia yeyote kujihusisha katika uhusiano wa kimapenzi kiholela kwa watu wengi bila kujali athari kwa mfano mwanaume au mvulana kuwa na wanawake wengi au mwanamke au msichana kuwa na wanaume wengi wanaohusiana katika mapenzi.

Suala hili limewekwa wazi na mawandishi kupitia shujaa pwaya amabaye ni Rosa Mistika. Rosa alilelewa katika malezi ya kufungiwa ambapo kutagusana na wavulana kwa kuwa Zakaria alimwonya kuhusu. Katika shule ya Morogoro TTC, Rosa alibadilika katika tabia baada ya kuanza kutangamana na wavulana. Hii inadhihirika wakati Rosa alipopata busu kutoka kwa Deogratias alipokwenda densi katika mjini. Baada ya kusalitiwa na Deogratias aliamua kutafuta wanaume wale anataka.

Rosa Mistika alipokuwa bado katika chuo cha Morogoro TTC hakuwa na nia ya kutafuta mchumba kwani haja yake ilikuwa ya kupendeza kila mvulana na alipopata mimba alijaribu kuavya mimba hiyo. Sifa za Rosa zilipomfikia padri, padri mmoja alitumwa aende kumwonyesha mwanga na alipofika alipata Rosa na kitabu cha mapenzi, vidonge vya kuzuia mimba, Rosa hakujali hata ujumbe wa padri, aliendelea na maisha yake ya umalaya. Vitendo hivi na dawa ambazo alikuwa anatumia, inadhihirisha kuwa hakujali maisha na sifa zake kuharibika ila kuingia katika anasa ya mapenzi ya kiholela. Wanafunzi katika chuo cha Morogoro walimpa jina ambalo lilimaanisha kuwa yeye ni mahabara ya kufanyia majaribio ya kimapenzi. Mwandishi anatueleza kuwa alilala na mkuu wa chuo Bwana Thomas chumbani kwake baada mkewe kusafiri.

Kazimoto na wahusika wengine wanapotagusana kwa mfano Kazimoto na vumilia ambao hawakuwa wameona wanazini. Kitendo hiki kilitendwa mara kwa mara na Kazimoto na Vumilia hadi inafikia wakati Kalia anaanza kuwa na hisia ambazo zilimpelekea kutaka kubaka msichana aliyekuwa anachunga ng’ombe. Tegemea aliposkia kuwa Kazimoto amekuwa anatoka na vumilia, alileta ugomvi kwa mji wa Mzee Mafuru ili aweze kumwonya Kazimoto.

Kazimoto akiwa kwa mji wa Tegemea kumchukua Vumilia wakati wa usiku, waliskia Mzee Kabenga akiongea chumbani mwa Tegemea kuonyesha walikuwa na uhusiano. Pia Kazimoto anakumbuka maneno ya Kalia alipomwambia kuwa alimsikia Kabenga akiomba Tegemea ruhusa na msamaha ya kuingia kwake kwa sababu alikuwa amefurushwa kisa hakumletea Tegemea pesa za kutosha.

Kalia ananza kuzini baada ya kujionea na kujifunza kutoka kwa Kazimoto na Kabenga, ndio maana anajaribu kubaka msichana aliyekuwa anachunga ng’ombe kwani alihisi ni kawaida kufanya hivyo. Hakuacha tabia hiyo hata baada ya kuonywa na kupigwa na Kazimoto, aliendelea kuzini hadi anamwibia babake pesa ili ampelekee Tegemea ambaye alikuwa wazini pamoja. Pia alianza kuhangaisha wasichana na wanawake kijijni hadi akaitwa mwehu na babake na kuuawa na wanakijiji alipofumaniwa akizini.

Tumaini alijiona kuwa amesoma na ana mali ambayo alirithi na hivyo kuanza kuchezea wasichana kijini. Alimtumia Leonila kwa kumaliza haja zake za kimwili na hata wanapopigana na Anastasia, haimsumbui hata. Leonila anapomwambia mamake kuwa alitiwa mimba na Tumaini, Tumaini anakataa na kusema kuwa Leonila alikuwa na watu wengi na kuwa yeye ni malaya.

Kristina ni mkware kwa kuwa alimchukua Tumaini kwake ili wazini naye akijua kuwa mumewe hakuwepo nyumbani kwa hivyo anahuru wa kumleta mwanaume yeyote vile anataka. Tumaini alipojaribu kukataa, Kristina alimlazimisha waende kwake kuzini na kumwambia kuwa hangemleta kwake kama bwanake alikuwa nyumbani. Kwa hivyo kuzini kwa Kristina wakati mumewe hayupo, ni ishara tosha ya kuwa mnafiki ambapo alijifanya mwaminifu mbele ya mumewe ilihali anamwendea nyuma ya kivuli.

Dennis anajifanya kumpenda mumewe ilihali alikuwa na uhusiano na John rafiki yake Tumaini. Unafiki huu unatokea Tumaini na John wanapoenda kwa Dennis ambapo Dennis anaonekana kuwa na hisia ndiposa anapanga njama ya kumwita John chumbani mwake mwa kulala hili wajifungie ndani na kuzini akijua mumewe hakuwa nyumbani. Unafiki wake ni kuwa anajifanya mwaminifu mumewe akiwa nyumbani ilihali alikuwa anazini kama hayupo.

### 4.4.3 Elimu ya Kisasa Vyuoni na Elimu ya Kimapokeo katika Jamii

Elimu yaweza kutokana na vitabuni au kwa watu katika jamii au mazingira ambapo mwanadamu amelelewa ili yaweze kumsadia katika kukabiliana na hali maisha. Mwandishi ameeleza elimu kwa mitazamo miwili; elimu ya kisasa au kimagharibi na elimu ya kimapokeo na jinsi inavyoathiri wahusika hasaa shujaa pwaya.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, mwandishi anaeleza kuhusu elimu aliyoipata Rosa alipopelekwa shuleni na ile ya kimapokeo. Mitazamo hii miwili ya elimu inaonyesha jinsi ilivyowathiri wahusika wengine na namna wanaitumia kujinasua na kujiumba kimaisha. Elimu ya kisasa ambayo Rosa alipata ilimwathiri

kwa njia hasi. Katika harakati za kupata elimu hii Rosa alijiona kuwa ana uhuru wakufanya chochote ndiposa anamkaripia babake kuhusu malezi. Elimu ya kimapokeo aliyopewa na wazazi wote pamoja na padri ilimsukuma na kumsaidia kwa kiasi. Rosa hakutilia maanani hii kwani ingemsaidia kumtoa katika ngome alimojiingiza.

> *"Rosa, usihamki."*
> *"Hapana, hufahamu taabu zilizonipata."*
> *"Kila mtu anapata taabu humu duniani."*
> *"Padri, maisha yangu yamekwishaharibika, na sijali! Kwanini wewe ujali roho yangu kuliko mimi mwenyewe?"* (uk. 49)

Shujaa pwaya, Kazimoto na Manase wanapata elimu ya kisasa ambayo inawabadilisha maisha na kuwa na mtazamo tofauti na rika yao katika kijiji chao. Elimu aliyopata Kazimoto na Manase iliwaletea mabadiliko kimawazo na kimatendo ndio maana wanapojadili swala la kuwepo kwa Mungu au kutokuwepo kwa Mungu na swala la kifo, inaashiria kupata elimu fulani.

Elimu hii ya kisasa inaleta uwajibikaji kwa Kazimoto ambapo anaamua kumchukua Rukia ambaye ni dadake ili kufadhili elimu yake. Kazimoto aliona umuhimu wa elimu ya kisasa kwake ndiposa anaamua kumsaidia Rukia aipate pia. Anampeleka kwa rafiki yake ambaye ni Manase ili aweze kuishi naye kwa muda hadi atakapomaliza masomo yake kwani alikuwa muhula wa mwisho katika masomo yake. Lakini Manase anamharibia masomo yake kwa kumtia mimba. Kitendo hiki kinamghadhabisha Kazimoto na kutaka kulipiza kisasi kwa familia ya Manase.

Mwandishi Euprase Kezilahabi amesawiri elimu katika mitazamo miwili kupitia shujaa pwaya ambaye ni Tumaini ambapo ameangazia kwa mtazamo wa kimagharibi au ya kisasa na utamaduni wa Kiafrika ua elimu ya kimapokeo. Elimu ya kimagharibi ilimwathiri Tumaini kwa njia tofauti ambapo ilimpa kuburi ambapo kilimfanya kuwahadaa wasichana waliokuwa hawajasoma. Tumaini alimlaghai Leonila na kumlazimisha kufanya mapenzi naye hata ingawa alikuwa amejitetea kwa kubainisha hila za vijana waliosoma.

Athari nyingine ya elimu ya kisasa ambayo inasawiriwa na shujaa pwaya ni ubaguzi wa kijinsia. Ubaguzi unatokea pale ambapo vijana wa kiume ndio walipewa au kupata elimu ya kimagharibi ambapo waliitumia kwa kuwahadaa waliouwa hawajapata elimu hii. Mwandishi anaeleza kauli hii kupitia kwa Leonila aliyemwambia Tumaini kuwa vijana wa kiume waliokuwa wamesoma huwadanganya kwa kuwahadaa walioishia darasa la saba. Tumaini pia anaposema kuwa yeye hupenda wasichana ambao hawakusoma sana. Usemi huu wa Tumaini unaonyesha ubabe dume au taasubi ya kiume katika jamii kwa kutuma wanawake na wasichana kama chombo cha kutimiza haja zao za kimwili, wakintimwa nafasi kama vile masomo huku wanafundishwa kuwatumikia wanaume. Tumaini anasawiri mtoto wa kike kuwa hapaswi kupewa elimu kwa kufanya vile humpotezea bahati ya kutunza ndoa yake au kuolewa.

Pia kwa upande mwingine wa elimu, mwandishi anasawiri elimu kupitia kwa shujaa pwaya kuwa muhimu katika jamii na kuwa ndio msingi wa maarifa tofauti tofauti. Dennis anatumika kama kielelezo anapomuuliza Tumaini kuwa usomaji wa vitabu ndio ulimpa hayo maarifa kuhusu maisha. Maarifa ya Tumaini yanatokea pale ambapo anasoma na kujibu wanaosoma gazeti kuhusu maisha. Isitoshe elimu ya maisha huwa haitaji vitabu ila tu busara alikuwa naye binadamu katika ndio maana wengine hushindwa kuthibiti utamaushi katika maisha ndiposa wengine hujitia kitanzi. Wazazi wachache ndio waliothamini elimu ya kuwa kielekezi katika jamii na kuwasaidia kuepukana na shida za mahali

**4.4.4 Mauti na Tanzia kama Sehemu ya Maisha**

Mauti yametumiwa na mwandishi kuonyesha sehemu ya maisha katika binadamu. Katika maisha ya binadamu kuna kuzaliwa ambapo wanafasihi husema kuletwa duniani, kuoa na mwisho ni mauti. Mauti ya binadamu hutokea au husababishwa na mambo kama vile; kukosa mapenzi ya dhati kutoka kwa jamaa zetu wa karibu, kutengwa na kukosa malezi pamoja na maelekezo kwa wakati unaofaa.

Mwandishi anaonyesha na kueleza jinsi mauti yalivyotekea kwa shujaa pwaya na wahusika wengine wa karibu wa shujaa pwaya. Rosa alipata habari kuwa babake mamake waliaga kwa njia iliyotatanisha wanakijiji. Zakaria anapatana mauti yake anapokuwa anatoka ulevini ambapo alichomwa mkuki kifuani.

Kifo cha Zakaria kinamfanya Regina ambaye ni mkewe kupatwa na mshtuko na kufa. Wanakijiji wanashangazwa namna familia hii ilipata pigo la kimaisha. Naye Rosa alipozipata habari hizi, aliaona kama dunia inamkejeli na kumchekelea ndiposa anachukua vipande vya chupa na kuvivunja na kuvisiaga na kuchanganya na maji. Rosa alimeza vitu hivi ambavyo vilimkata uhai wake baada ya kuona kuwa dunia haimtaki tena.

Kitika riwaya ya *Kichwamaji*, kifo kileta mjadala mkali kati ya Kazimoto na Manase ambao walikuwa na mtazamo tofauti kuhusu kifo wanajiuliza asili ya kifo na mbona kililetwa. Kwa mfano, kifo cha Rukia kilimghadhabisha Kazimoto na kumlaumu Manase kuwa yeye ndiye chanzo ndio maana anaamua kulipiza kisasi kwa kuchoma nyumba ya akina Manase.

Baada ya Kalia kujiingiza katika kitendo cha uzinifu, alipatana na kifo cha alipofumaniwa na wanakijiji alipokuwa akitenda uozo huo. Alikuwa amewahangaisha wanawake na wasichana katika kijiji ndio maana wanakijiji walishikwa na hamaki na kumwondoa uwai.

Wanakijiji wanashangazwa na kifo cha mtoto wa Kazimoto ambaye hakuwa amefikia kuonja maisha dunia. Kifo hiki kilitokea Sabina ambaye ni mke wa Kazimoto anajifungua ambapo mtoto aliaga kabla ya kutolewa kwa sababu daktari alikuwa anashughulikia upasuaji wa mgonjwa na pia mtoto alishindwa kupita kwa kuwa alikuwa na kichwa kubwa.

Wanakijiji wanamvamia mtu mmoja aliyeshukiwa kuwa ni mwizi na kupiga nakumuua bila kumhurumia. Tumaini anashuhudia kifo hiki kwani yeye ndiye aliyewaelekeza wanakjiji waliokuwa wanamkimtafuta mahali alikoelekea mwizi huyo. Anapotazamana na mwizi huyo baada ya kushikwa nakupigwa, alimwonea huruma na kujuta kwamba ndiye amesababisha kifo chake na kuwa kama hangewaonyesha wanakijiji, hangepatana na kifo hicho.

Tumaini anashuhudia ukatili na mauaji wakati walikuwa wametoka na Anastasia na rafiki yake kuelekea mashindano ya densi, ngoma na nyimbo za kitamaduni zilikuwa zinachezwa. Wakiwa wanatazama na

kufurahia mashindano hayo, waliskia kelele na mvutano na walipofika hapo mtu mmoja alikuwa ashauliwa na chanzo cha kifo chake hakikueleweka. Mwandishi anaeleza kuwa inasemekana kuwa alikuwa mwizi na jamii haikutaka amani ivurugike ndiposa anavamiwa na umati uliokuwa katika mashindano ya densi na ngoma.

### 4.4.5 Tamaa, Ubinafsi na Uhuru wa Mtu Binafsi

Ubinafsi ni kujitakia makuu au kujinufaidi bila kujali watu wengine kama watafaidi au kutofaidi. Wahusika kadhaa katika riwaya wameonyesha tamaa na ubinafsi wanapotangamana na wengine na kuathiri wengine kimaisha. Matendo haya ni mojawapo ya maadili hasi kwa jamii na hata mhusika mwenyewe Mwanadamu huwa na ubinafsi anapokuwa ana haja ya kitu fulani ambacho anaona kitamfaidi pekee yake.

Tamaa na ubinafsi ni mojawapo ya ngome ambazo zilimfunga Rosa katika maisha yake. Hakuweza kutafautisha hali ambazo zilikuwa zinampata ndiposa anafanya uamuzi unaomwathiri kwa njia hasi. Rosa anajawa na tamaa ya kuwa na mpenzi au uhusiano na wavulana aliokatazwa na babake. Tamaa na ubinafsi inamalizia kuwa tabia ambapo alianza kuwa mkware. Rosa aliona kuwa amekuwa mtu mzima anauwezo wa kufanya chochote bila kujali wengine. Ubinafsi na tamaa yake inatishia kuharibika kwa ndoa za wengine kama vile Thomas. Rosa alifumaniwa na mke Thomas nyumbani mwake ndio maana akampiga na kung’ata sikio.

Shujaa pwaya Kazimoto katika riwaya ya *Kichwamaji* alitawaliwa na ubinafsi ambao unaathiri maisha ya wahusika wengine kwa mfano. Kazimoto aliwachezea wasichana wengine kihisia ilihali hakuwa na nia ya kuwaoa kama vile Vumilia. Vumilia alikuwa na matumaini kuwa mapenzi yake na Kazimoto yatawafikisha kilele cha kuoana. Matumaini yake yalifika mwisho aliposkia kuwa Kazimoto alipanga kumwoa Sabina nduguye Manase ndio maana alitamauka na kusema kuwa hana umuhimu katia dunia na akaamua kuenda mjini na kuolewa na Moyokonde.

Manase naye anajawa na ubinafsi uliotokana na hisia zake za kimwili kumskuma kumlazimisha Rukia, nduguye Kazimoto na kumtumia na kisha kumtia mimba na kumharibia masomo yake. Hamu ya elimu ya Rukia ilifikia kikomo alipopata ujaa uzito na kulazimika kumwandikia barua ya kumwomba msamaha Kazimoto kwa kuwa ndiye alifadhili masomo yake. Manase alimpa Salima kazi bila kujali watu wengine kama vile Kazimoto aliyekuwa anatafuta kazi katika ofisi za mkuu wa wilaya.

Ubinafsi ni kujitakia makuu au kujinufaidi bila kujali watu wengine kama watafaidi au kutofaidi. Wahusika kadhaa katika riwaya wameonyesha tamaa na ubinafsi wanapotangamana na wengine na kuathiri wengine kimaisha. Matendo haya ni mojawapo ya maadili hasi kwa jamii na hata mhusika mwenyewe.

Mwandishi ametumia shujaa pwaya kuonyesha na kuliweka swala hili la tamaa na ubinafsi wazi kwa mfano Tumaini anaonyesha ubinafsi na tamaa hata akiwa mtoto. Kupitia malezi aliopewa na wazazi wake, ubinafsi na tamaa ilijijenga ambapo aliona kuwa niyeye tu ndio anastahili kupewa chochote atakacho. Mwandishi anasema kuwa Tumaini akiwa mdogo akiona kitu alikuwa analia na kukatalia ili anunuliwe ndio maana alinunuliwa vijigari vingi vidogovidogo vya kuchezea. Wazazi wake hawakumfunza kuwa katika maisha kuna kupata na kuna kukosa na hivyo hakuna haja ya kulia ndio maana alitumia pesa na mali vibaya baada ya kurithi kutoka kwa wazazi. Tumaini alitumia mali na pesa hizo kibinafsi katika anasa za ulevi na kutafuta wanawake wa kutumia bila kujali maisha ya kesho. Alipojua na kuambiwa na mamake kuwa aliachiwa mali na babake ili arithi, aliingiwa na tamaa na ubinafsi ambapo hakuona haja ya maidha ya mamake bali alikuwa na haja na ufunguo wa pesa.

Ubinafsi pia ulijitokeza alipomchoma mlezi wake jichoni na alipopigwa na mlezi alikimbia kumsema kwa mamake ambaye alimfokea mlezi kimadharau. Tabia hii inaonyesha ubinafsi kwani tabia hii ya kuumiza wengine nayeye hakutaka kuumia ni ubinafsi ambao unapotosha maadili yake katika jamii. Wazazi wake wanamdekeza na kulegea katika kumfunza madili ili kuwaheshimu watu wazima. Kwa

kupotoka kimaadili, anajihusisha na mambo ya uozo kijijini na hajali madhara ya mambo ya kwa wanakijiji wenzake.

Baada ya Tumaini kumwonyesha Leonila mapenzi kwa kumdanganya alimtia mimba, anamkataa mbele ya mamake, Mungere aliyetaka kujua kama niyeye alimtia mimba. Tumaini alikana kuwa hakumtia mimba na kuwa Leonila alikuwa na watu wengi ambao alikuwa anatembea nao na ni malaya. Maneno haya yalimchoma Mungere moyoni na kutoa machozi kwa kuwa bintiye hangepata mwanaume mwingine kama Tumaini atakataa mimba hiyo. Tumaini alipomaliza haja zake za kimwili alimkataa Leonila.

Tumaini aliingiwa na tamaa na ubinafsi aliposkia kuwa babake, Kapinga alimwachia urithi wote ambapo hata mawaidha ya mamake aliyemwambia luwa ukoo wa babake upo mikononi yake yalisumbua tu kwa kiasi akilini. Mamake alimwambia kuwa ameachwa na pesa nyingi kwa hivyo achunge asije akaharibu maisha yake. Mawaidha hayo hakuyashika kwani alifikiri jinsi atarithi pesa nyingi na funguo wa mali.

Mwandishi anaeleza kuwa Mugala alitumia uchawi na ushirikina kujinufaidi, kuharibu na kutesa wanajamii wengine. Aliwabadilisha watu wengine kwa kuwafanya vizuu ambao alitumia kufanya kazi zake kama vile kuchota maji na kutafuta kuni. Mwandishi anazidi kueleza kupitia kasala ambaye anasema kuwa mamake, Mugala huwageuza watu na kuwasafirisha nchi za mbali na pia huwaleta vizuu wa uko ambapo amebadilishiwa wa kwao. Mwandishi anamtumia Kasala kueleza kuwa Mugala alikuwa anapata ageni kila mara kutoka sehemu mbali mbali ambapo wengine walifanya kazi ya uchawi. Anasma kuwa wageni hao walibadilisha watu na kuwaleta kwa Mugala kuwabadilisha na kuwa walielewana jinsi wanafanya uchwi huo. Watu wengi waliogopa na kuishi kwa hofu ilihali Mugala aliishi maisha bila hofu kwa kuwa aliogopwa kwa uchawi wake ambao alitumia kujilinda.

**4.4.6 Utamaushi**

Utamaushi ni hali ya kupoteza matumaini katika jambo au tendo lilokuwa linasubiriwa na binadamu. Riwaya hii ya kidhanaishi imetamalakiwa na utamaushi wa wahusika hasaa shujaa pwaya ambapo

mwandishi ameleta dhana hii ya utamaushi miongoni mwa wahusika. Matumaini ya Kazimoto ya kutafuta kazi yalifika mwisho akiwa ofisini mwa Manase kwa kuwa alikuwa ameona dalili ya Salima kupata kazi kwa sababu alikuwa mpenziwe Manase. Kazimoto anakabiliana na hisia za Manase katika ofisini mwa Manase baada ya kuona kuwa hangepewa kazi ndiposa chuki kwake inazidi kukua.

Baada ya Manase kumharibu na kumharibia Rukia masomo, Rukia anatamauka na kuamua kucha masomo na kumwandikia ndugu yake barua, Kazimoto kuwa hangeweza kuendelea na masomo sababu ana mimba na Manase amemfukuza kwake. Matendo haya ya Manase yanamghadhabisha Kazimoto na kuapa kuwa atalipiza kisasi kwa Manase ama familia yake.

Kazimoto na Manase wanaonekana kuwa na hisia za kitamaushi wanapokuwa wakijadili kuhusu kuwepo kwa Mungu na ni sababu gani zilizosababisha kifo. Wanajiuliza maswali haya na hata utamaushi unazidi kuwatawala Kazimoto kifo kilipompata Rukia akiwa anajifungua na si kifo cha Rukia pia kifo cha mtoto wao na Sabina.

Vitendo vya mwanawe Mzee Mafuru vinamtamausha na kuona kuwa Kalia hakuwa na maisha yeyote muhimu kwani alifanya mauvu kijijini ndiposa akamwita mwehu.Kalia alianza kuwa na tabia ya kuwahangaisha wanawake na wasichana katika kijiji na hata akaanza kulala na wanawake ambao hakuwa wameolewa kwa mfano Tegemea. Ni hali ya kukosa matumaini katika jambo fulani au maisha. Mwandishi ametumia udhanaishi katika uandishi wa riwaya hii kuonyesha maisha ya binadamu hasaa wahusika kama vile Tuamaini. Baada ya kifo cha wazazi wake, Tumaini alianza kupotoka kimaadili kijijini ndiposa akamua kuelekea mjini. Tabia yake potovu ilimkosesha matumaini ya mwingiliano na wanakijiji ndiposa akamua kuenda mjini mahali hatakuwa na kutana na wao.

Utamaushi unatokea kwa mwizi aliyekuwa anakimbishwa na wanakijiji kwa kuiba, baada ya kuona kuwa anashikwa anajaribu kumwomba Tumaini msamaha na kuwa asiseme mahali yupo. Mtazamo wake wa

ana kwa ana unaonyesha kukosa matumaini ya kusamehewa ndio maana Tuamaini anajuta kwa kumsema na kuuawa kwake. Anajisemea kimawazoni kuwa kama hangemsema, hangekutana na kifo chake.

Matumaini ya Tumaini yanafikia mwisho aliposkia tangazo la mkuu wa wilaya kuhusu umiliki wa mashamba katika tangazo la Azimio la Arusha. Katika tangazo hilo, Tumaini na matajiri wengine wenye miliki kubwa ya mashamba wangepoteza mashamba hayo kwa serikali. Tumaini anapoteza matumaini na kujawa na hamaki uliomskuma kutenda unyama ambapo alimuua mkuu wa wilaya kwa kutangaza tangazo hilo. Baada ya kifo cha mkuu wa wilaya, Tumaini alikamatwa na kuhukumiwa kifo.

Mwandishi ametumia utamaushi kueleza dhamira yake au kuafikia malengo yake kupitia shujaa pwaya ambaye ni Rosa. Rosa anakata tamaa katika maisha yake pamoja na baadhi ya wahusika wengine kwa mfano anapopata habari kuwa Deogratias alikuwa na wanawake wengine, anakata tamaa na kuchukua hatua kumwacha na kuelekea Mwanza kuenda kukunywa. Akiwa Mwanza, anajiingiza katika ukware na ulevi ili aweze kukabiliana na kusahau mawazo kuhusu uchumba wake na Deogratias aliyemsaliti na kumlaghai kimapenzi.

Maisha Rosa yanachukua mkondo mwingine kwa kuhisi kuwa amesalitiwa na mpenzi ndio maana anakata tamaa na kujiingiza katika ukware bila kuajli sifa zake. Shuleni alijulikana na kubandikwa jina kuwa yeye ni mahabara kwani kila mwanaume alimfanyia majaribio ya kimwili mifano ni; Thomas ambaye ni mkuu wa shule na Deogratias. Kutamauka huku kulimfanya warushiane maneno na Zakaria ambaye ni babake kwa kuwa alifikia kilele cha kuharibika na hakuwa na thamana yeyote. Pia anakata tamaa anapopata barua kutoka Charles na kugundua kuwa Charles hakumpenda. Masaibu yanaongezeka anapopata habari kuwa babake na mamake wameaga dunia kutoka na mshtuko alioupata kuwa mumewe aliaga dunia. Rosa anachukua hatua ya kujiua kwa kuvunja chupa na kuisiaga na kumeza vipande alipoona kuwa hakuna haja ya kuishi tena duniani.

Mount Kenya University

Regina ambaye ni mamake Rosa,  alikata tamaa ya kumwomba mumewe pesa alizompa za kutumia katika usafiri wa Rosa kwenda shule baada ya kugundua kuwa alishazitumia katika ulevi. Anatamauka na kuamua kuanza kutengeneza na kuuza pombe ya kienyeji ili aweze kufadhili masomo ya Rosa pamoja na usafiri wake na pia mahitaji mengine ya familia. Uamuzi huu ulitokana kwa kuwa hapakuwepo na njia mbadala au mfadhili wa masomo ya Rosa na pia upato wa familia ulikuwa chini. Mapato waliopata kutoka kwa kilimo yalitimiza tu mahitaji ya familia tu kama vile kununua chakula.

### 4.4.7 Migogoro, Mafarakano na Ukinzani katika Jamii

Mgogoro ni mvutano kati ya watu wawili au zaidi ,mvutano kati ya makundi mawili au hisia za mtu. Katika kijiji cha Mahende, Kazimoto anavutana na babake kwa sababu ya tabia zake ambazo zilkuwa zimeanza kumkera kijijni za kutoka na kurudi kukiwa giza. Mamake alipojaribu kumrekebisha alileta ugomvi unaonyesha kupotoka kwa madili kwa Kazimoto.

Kazimoto alianza kuwa na mazoea ya kutoka usiku wa giza kwenda kumchukua Vumilia kutoka kwao wakiwa na Kalia, jambo lilipomfikia Tegemea, alikasirika na kuamua kupeleka ugomvi kwa mji wa Mzee Mafuru. Tegemea alipompata Mzee Mafuru, alitoa onyo ili Kazimoto aonywe .

Mvutano kati ya Manase na Kazimoto ulitokana na Rukia kuharibiwa  maisha na Manase, jambo lililomfanya Kazimoto kughadhabishwa na kuamua kulipiza kisasi kwa familia ya manase ndio maana alichoma nyumba na hata kumua pia kumharibu Sabina. Kitendo cha kumharibu Sabina hakikufaulu kwani Kazimoto alibadilisha nia na kumuoa.

Mgogoro wa kimawazo wa Kazimoto ulimfanya kubadili nia ya kutaka kulipiza kisasi kwa familia ya akina Manase kwa kuwa na hisia na mapenzi kwa Sabina nduguye Manase. Kazimoto alijawa na mawazo kuhusu vifo vilivyotokea kwa jamaa yake ndiposa akaleta mjadala kuhusu kuwepo kwa Mungu na kutokuwepo kwa Mungu. Alijiuliza, kwa nini Mungu akamcha binadamu akafa au akapitia mateso ya ulimwenguni?

Mvutano kati ya binadamu inaonyesha kutoelewana kwa matendo ya wengine au hali ya maisha na jinsi yanavyotea. Mvutano huu waweza kuwa kati ya serikali na mtu binafsi, kundi la watu na kundi lingine , kundi na mtu, hisia za mtu kuvutana na mtu na mtu. Mwandishi ameweza kuweka wazi migogoro hii kupitia shujaa pwaya na wahusika wengine.

Mwandishi anaonyesha mvutano wakati wa marekebisho ya kitabia na malezi kati ya Kasala na Mugala anapokuwa anamrekebisha Leonila aliyekuwa amekosa. Mugala anamwambia kuwa atamtandika Kasala kama hatamwachilia Leonila. Kupinga kucharazwa kwa Leonila kunaonyesha mvutano katika malezi hata ingawa hukuleta madhara sana ila tu Tumaini alitumia nafasi hiyo kumchezea Leonila.

Muyango ambaye ni mamake Tumaini alionyesha mvutano wa kimalezi na Kapinga ambaye ni babake Tmaini anapogundua kuwa alikuwa ameamwachia Tumaini mali yote kurithi. Muyango alisema kuwa haya mali anayoachiwa yote akiwa mchanga yatamharibu na kumhaaribia maisha yake hata ingawa hakuwa na uwezo wa kubadilisha uamuzi huo Kapinga.

Maadili ya Tumaini hayakuwiana na wanakijiji ndio maana anamua kutoka kwa kijiji na kuelekea mjini ili aweze kupata nafasi na wakati wa kufanya vitendo vyake. Tumaini akiwa kijijini alianza kunywa pombe na kujihusisha katika uzinifu.

Mgogoro wa kisiasa uliosababisha kifo cha mkuu wa wilaya kwa kutangaza tangazo la serikali kuwa kutakuwa na Azimio la Arusha. Tumainia anaonekana kukerwa na tangazo hili la Azimio la Arusha ambalo liligusa waliomiliki mashamba na mali nyingine. Tangazo hili lilipeleke kifo cha mkuu wa wilaya ambaye aliuawa na Tumaini naye kuhukumiwa kifungu cha maisha gerezani.

Anastasia na Leonila wanapigana kwa sababu ya husiano wao kwa Tumaini ambapo Leonila hakufurahia husiano uliopo wa Anastasia na Tumaini. Leonila anamshika na kumwangusha chini na kuvutana kwa muda mrefu huku wakiraruriana nguo karibu wabaki uchi na inatokea Leonila anashindwa ndiposa

anamwita Anastasia aje amsaidie. Tumaini alikuwa anawachezea hawa wasichana kihisia ndiposa walipojua kuwa kuna husiano, walianza mvutano

Katika Rosa Mistika, Migogoro ni mvutano uliopo kati ya binadamu na binadamu mwingine, kijiji na mtu, mtu binafsi na usasa na utamaduni au ukale. Rosa ametumiwa kama shujaa pwaya na mwandishi kupitisha migogoro katika riwaya hii alipotangamana na wahusika wengine. Mvutano kati ya Rosa na Babake ambaye ni Zakaria kutokana na malezi anayopewa.

Zakaria anaposkia kuwa kuna vijana wameanza kumtafuta na huwa walimletea Rosa barua, aliwashika na kuwapiga hadi wakabadilisha na kumwambia kuwa wanatafuta mayai wanunue. Zakaria hakutaka wasichana wake waanze mapenzi na wavulana kwa kuwa aliona hiyo ndio njia ya kuwalea. Mvutano huu ulikuwa kwa ajili ya shujaa pwaya ambaye ni Rosa Mistika kwani vijana hao walikuwa na mtagusano na Rosa.

Regina, mamake Rosa, alipata masaibu katika ndoa yake tangu aolewe na kulaumiwa na mumewe kwa mambo ya kimaumbile. Mvutano huu na mumewe ulisababishwa nakutozaa mtoto wa kiume ambaye jamii ilithamini sana. Zakaria aliporejea nyumbani  kutoka ulevini, alimpiga na kama kwamba anamkumbusha hali yake ya kuzaa wasichana pekee. Mwandishi anaeleza mgogoro huu kwa kusema kuwa hakuna mwanamke aliyepitia mapigo kama ya regina.

Mgogoro mwingine ni kati ya Zakaria na Rosa baada  ya Stella kumwambia zakaria kuwa Rosa alipewa barua. Zakaria alipojaribu kumwomba Rosa barua hiyo, aliitia mdomoni na kuitafuna. Kitendo hiki kilimkasirisha zakaria na kuamua kumpiga Rosa ilikumkomesha tabia yake. Alichukua pesa alizokuwa ameletewa na Charles na kumrushia chini pesa hizo na kumwambia aondoke.

Mvutano mwingine ni kati ya Zakaria na Rosa baada ya Zakaria kupata habari kuhusu tabia za ukware na alipojaribu kumkanya, Rosa alipandashwa na hasira na kumrushia babake maneno. Tabia yake ilikuwa ya kuenda na mwanume yeyote kwa mfano Thomas ambaye ni mwalimu mkuu ambapo jambo hili

lilimkera Zakaria na kumfanya ugomvi uliomfanya Rosa kutoa maneno makali mdomoni na kusema kuwa yeye si babake naye Zakaria akamjibu kuwa pia yeye si bintiye.

Mke wa Thomas ambaye ni mwalimu mkuu wa shule wanavutana na Rosa kwa sababu Rosa alikuwa wanazini na Thomas. Rosa alikuwa mkware ambapo alimtafuta Thomas na wakaelewana kuwa wataenda kwa Thomas. Nyumbani mwa Thomas, Rosa alikunywa sana hadi kujitambua ikawa shida na hapo ndiposa Thomas alichukua nafasi ya kuzini na Rosa. Rosa walipofumaniwa mkewe Thomas, alikatwa na mkewe Thomas kwa kuzini na mumewe.

Rosa alipigana na msichana mmoja ambaye walisoma naye shule kwa sababu ya kuwa majina yao yaliandikwa na Rosa kwa wale walikuwa wametoroka shule kuenda mjini kwa densi. Msichana huyo alimlaumu Rosa kwa kusababisha kufukuzwa kwao shuleni ndiposa wanapokutana sokoni wanapigana. Walibururana kule sokoni huku wakishikana na kuangushana chini wakiangaliwa na watu kule sokoni.

### 4.4.8 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii

Katika riwaya teule zilizochanganuliwa, mwandishi amesuka mwanamke kwa njia tofauti kupitia shujaa pwaya katika jamii yake kwa namna ya mtagusano. Kwa mfano, shujaa pwaya amesawiri mwanamke kama chombo cha kutimiza mahitaji ya kimwili na mahitaji mengine mwanaume.

Mwandishi amesawiri mwanamke kupitia shujaa pwaya katika riwaya ya *Rosa Mistika.* Jamii imweza kumsawiri mwanamke kuwa mkware kwa mfano Rosa anapoanza uhusiano wa kiholela na wanaume ambao anakutana na wao kama vile Deogratias, Thomas na Charles hadi akabandikwa jina la kuwa mahabara. Pia mwandishi amemsawiri kuwa mvumilivu katika maisha. Regina anavumilia mateso ya mumewe ambaye alikuwa mlevi na mpyro sana. Alizoea kumtusi na kumdharau kwa kuwa hakuwa na mtoto wa kiume. Uk . 23

> *Mshenzi, unanizalia wasichana tu! Unaniletea taabu nyumbani bure tu!'' Zakaria alifoka*.

Kazimoto anamtumia Vumilia kwa haja zake na kumuumiza kihisia alipofikiria kuwa atamwoa wakati mmoja. Vumilia anakasirika na kutamauka ndiposa nasema kuwa hana umuhimu wowote duniani na kuamua kuenda mjini na kufanya ukahaba. Manase alimuharibia maisha Rukia kwa kumtumia ili kutimiza haja zake kimwili na pia kumfukuza kwake alipogundua kuwa amemtia mimba. Kazimoto alimwanini Manse kama rafiki ndiposa akamkabithi Rukia ili aishi naye kwa muda hadi amalize muhula wake wa mwisho shuleni. Uhasama unaingia Manase alipomtumia Rukia na kisha kutusi kuwa ni malaya na mimba si yake na kuamua kumfurusha kwake.

Mwanamke ameonyeshwa kutamauka kupitia kwa shujaa pwaya alipotangamana,mfano Rukia alipogundua kuwa Manase alipachika mimba, aliamua kuacha masomo. Rukia alimwandikia barua Kazimoto na kumwomba msamaha kwa jambo hilo hata ingawa si makosa yake.

Mke amesawiriwa kama chombo cha anasa na starehe. Mwandishi amemchora mwanamke kama chombo cha starehe anayeweza kutumiwa kuwastarehesha wanaume ilimradi kufurahisha nafsi zao, kwa mfano mwandishi anamtumia Kristina kama chombo cha starehe, ambaye alionekana kujifurahisha na Tumaini ili  apate atimize haja zake.

Mke amesawiriwa kama mtu asiye na maamuzi katika jamii. Mwandishi amemchora mwanamke kama mtu asiye na maamuzi katika jamii yake, kwa mfano mama yake Tumaini kushindwa kufanya maamuzi juu mali alizoziacha kama urithi wa Tumaini japo hakupenda kumuachia mtoto wao fedha nyingi kwa kuwa zingemchanganya na kumwangamiza katika maisha yake, lakini alishindwa kubatilisha kutokana na maamuzi yaliyoachwa na mumewe. Pia wazazi wa Anastasia wanamtafutia bwana na wanamwamua na kupanga jinsi ataolewa lakini Tunamaini alipanga na kumtorosha kwao.

Kupitia shujaa pwaya mwanamke amesawiriwa kuwa msaliti katika ndoa yake, kwa mfano Mama Resi ambaye ni mke wa, Dennis alitaka walale na John. Mama Resi anasema mwambia John kuwa alikuwa mtu mzima alifaa kuelewa mambo hayo lakini kwa uwoga alionao John, alitoroka nje na kumwacha

katika chumba cha malazi. Usaliti mwingine pia unatokea pale ambapo Kristina anapoamwambia Tumaini kuwa hawezi kumleta mwanaume mwingine kwake kama mume wake yupo, ndio maana alimleta Tumaini kwa kuwa mumeo alikuwa ameshatoka.

Wanawake wametumika kuendeleza mambo ya uchawi ambayo hayajengi jamii ambayo ni ushirikina na uchawi, kwa mfano Kasala anaposema kuwa alimkanya mamake mambo uchawi lakini akasema kuwa ni urithi ambao hawezi kuacha.

**4.4.9 Ndoa kama Uwanja wa Fujo**

Ndoa ambayo imeelezewa na mwandishi katika riwaya ya *Rosa Mistika*, ilikuwa kati ya Zakaria na Regina. Ndoa hii ilibarikiwa na wasichana na mvulana mmoja. Mwandishi anaisawiri ndoa hii kama uwanja wa fujo kwa ilijawa na misukosuko iliyosababishwa na ulevi, ukosefu wa mtoto wa kiume na utukutu wa watoto. Regina ni mwanamke aliyepitia mengi katika ndoa yake ambapo Zakaria alikuwa anampiga na kudhihaki kwa kukosa mtoto wa kiume. Tangu aolewe na kulaumiwa na mumewe kwa mambo ya kimaumbile. Zakaria aliporejea nyumbani kutoka ulevini, alimpiga na kama kwamba alimkumbusha hali yake ya kuzaa wasichana pekee. Mwandishi anaeleza mgogoro huu kwa kusema kuwa hakuna mwanamke aliyepitia mapigo kama ya Regina.

Mwandishi ametumia shujaa pwaya kutuonyesha jinsi ndoa imesawiriwa katika riwaya ya *Kichwamaji* na jinsi inaathiri wahusika wengine. Kwa mfano ndoa kati Mzee Mafuru na mamake Kazimoto ilibarikiwa na watoto watatu ambao ni Kazimoto ambaye ni kifungua mimba, Rukia ambaye ni mtoto wa kike katika familia na Kalia. Ndoa hii ilikumbwa na shida ambazo zilitokana na watoto kwa mfano utukutu wa Kalia uliosababisha kifo cha kwa kuwa aliwasumbua wanakijiji. Kifo cha Rukia kiliwahuzunisha watu wengi hasaa wazazi wake,kilichotokana na utata wakati wa kujifungua. Wazazi hawa walionyesha kushirikiana na kuwajibika katika malezi ya wanao ndiposa Kazimoto anaendeleza malezi hayo kwa nduguze hata ingawa vifo vinawakumba.

Ndoa kati ya Kebenga na Tegemea iliowapa wanakijiji mshangao kwni hawakutarajia ndoa hiyo na kuwa Kabenga alikuwa na mke na watoto wakubwa. Tegemea hakuwai olewa na hivyo aliapata changamoto katika ndoa hii hata wakati mwingine ugomvi na Kabenga lakini alijaribu kufanya yote kumfurahisha mumewe.

Kazimoto na Sabina, ndoa yao ilitokana na Kazimoto kutaka kulipiza kiasasi kwa familia ya Kabenga, lakini mapenzi yalibadilisha nia yake. Kazimoto aliona haikuwa na haja yeyote ya kumtumia na kumharibu Sabina vile Manase alimharibia Rukia maisha yake. Ilibidi ampende hata ingawa ndoa yao ilikumbwa na tatizo la kifo cha mwanawe ambapo huzuni na maswali mengi kwa Kazimoto yaliwatawala.

Mwandishi ameweza kuonyesha pande mbili za ndoa na mapenzi ambazo ni ndoa na mapenzi ya dhati na mapenzi ya ulaghai. Kwa kutumia shujaa pwaya, Tumaini. Pia ni kuonyesha hali halisi katika jamii kuhusu swala laa ndoa kwa wazee na katika ndoa changa jinsi zinavyosawiriwa katika jamii.

Ndoa na mapenzi ya dhati ni kwa Anastasia na mumewe Tumaini ambapo mwandishi ameonyesha Tumaini akipnga kumtorosha Anastasia kutoka kijijini kuelekea mjini Shinyango ambapo watajificha na kuishi ili wasijekujulikana na Anastasia asije akaolewa na mzee. Anastasia naye anaonyesha mapenzi ya dhati katika ndoa yake kwa kuamua kuolewa na kuishi na Tumaini hata ingawa alikuwa mhuni katika anasa na mlevi. Licha ya Tumaini kuvamiwa na kupigwa na watu wasiojulikana, Anastasia alimhudumia kama mkewe aliye na mapenzi ya dhati kwa kumpelekea chakula.

Mwandishi amesawiri ndoa kuwa na taasubi ya kiume kwa mfano Kapinga ambaye ni babake Tumaini, alionyesha taasubi ya kiume katika ndoa yake anapopanga na kumrithisha Tumaini mali yake yote. Mwandishi anazidi kueleza kuwa hata kama Muyango alikuwa na maoni mazuri, Kapinga aliyapuuza, kuonyesha jamii hii haikudhamini maoni ya jinsia kike.

Ndoa katika jamii hii ilithamini urithi kwa watoto wao hata kuanzia miaka wakiwa wachanga ambapo hajawaelewa jinsi ya kuendesha maisha yao kama watu wazima. Kapinga anamrithisha Tumaini mali yote hata kama alikuwa mchanga ambapo Muyango alihofia kuwa mali hayo yaenda yakamharibu na kuharibu maisha yake. Urithi ulimharibia Tumaini maisha yake na hata kupotoka kimadili anapokuwa kijijni na hata mjini ambapo alianza kutenda uozo kama vile ulevi na ukware na ilihali alikuwa ameoa.

Ndoa za kutafutiwa na kuchaguliwa mume zilithaminiwa na jamii ambapo wazazi waliwachagulia wanawao wachumba hasaa wasichana kuchaguliwa wachumba ambao ni wazee. Anastasia alitoka familia ambapo wazazi walikuwa washampangia ndoa yake na mzee Tembo kabla hajapata mimba ambayo haikumfurahisha. Anastasia hakutaka ndoa hiyo ndiposa anapanga na kutoroka na Tumaini kuelekea mjini, shinyanga kujificha na kuishi uko ili wazazi wasije wakasisitiza kufanyika kwa ndoa hiyo.

Mwandishi ameweza kueleza kuwa ndoa huchukuliwa kuwa safi na kuthaminiwa kukiwa msichana alijitunza vyema katika maisha yake ya ujana kabla hajaolewa. Mungere alitoa machozi ya huzuni alipogundua kuwa Leonila ana mimba ya Tumaini ambayo iliashiria kuwa kutakuwa vigumu kuolewa kama Tumaini atakana mimba hiyo kuwa ni yake. Anastasia ndoa yake inapangwa mapema kabla apate mimba na hii ni ishara kuwa hawezi oelewa.

### 4.4.10 Mwachano, Uhusiano na Utangamano baina ya Vizazi

Mwandishi Euphrase Kezilahabi ameeleza jinsi vizazi vinaonyesha uhusiano, mwachano na utangamano. Anatoa picha mbalimbali za hali ya maisha, mabadiliko ya kizazi katika jamii na mfumo ya kijamii. Katika uhakiki zaidi, kuna tofauti na pia uhusiano kati ya shujaa pwaya na familia zao na jinsi wanavyokabilana na changamoto za kihisia, uchumi na jamii vile vile.

Shujaa pwaya Rosa, anaonyesha uhusiano wake na mwachano kati ya vizazi na changamoto zinazohusiana na masuala ya kijinsia. Bidii ya Rosa katika masomo yake, inaonyesha ndoto kubwa

aliokuwa nayo lakini inaanza kudidimia wakati ambapo anaanza uhusiano na wavulana. Matendo ya Rosa wakati wa kujitambua yanaonyesha tofauti ya mawazo kati ya vizazi, ambapo wazazi wanataka kumfunza mtoto wao kwa njia ya zamani na kumlazimisha kuishi katika maisha ya kimapokeo, lakini Rosa alitaka maisha ambayo alijijengea kwa kujitenga na mifumo hiyo.

Shujaa pwaya Rosa ni kiwakilishi cha kizazi cha kisasa ambacho kinataka mabadiliko katika malezi ya kuchungwa na wazazi. Uhusiano wa Rosa na wazazi unadhihirisha mgogoro wa kijamii na kisaikolojia kwa sababu wazazi wake mfano wa baba, anategemea mitazamo ya kijadi ya malezi ya kuwachunga lakini Rosa anajitenga na kuingia ulimwengu wa sasa.

Tumaini alijikuta katika mabadiliko makubwa yaliyosababishwa na kizazi cha awali ambacho ni wazazi wake. Hakuweza kutangamana kwa muda mrefu na wazazi wake kwani waliaga kabla kuwa mtu mzima. Uhusiano uliopo kati ya wazazi wake ulijionyesha katika malezi yake na wakati alipoachana. Kapinga ambaye ni babake Tumaini, alimpa malezi ambayo yalimkosesha maadili na jamii aliyoachiwa. Maadili yake yalikuwa potovu na ambayo hakuwiana na jamii. Jamii yake ilioko katika kijiji cha Bugolola kilisisitiza madili hata ingawa ni ya kijadi kwa mfano. Mulele na Bukhele ambao ni wazazi wa Anastasia walitaka kumuoza kwa mzee Tembo. Tumaini anapanga namna ya kumtorosha Anastasia ili asije akaolewa na Tembo. Kitendo hiki kinaonyesha mapenzi ya dhati.

Changamoto za kimaisha zilimpata Tumaini alipokuwa anajitambua katika maisha; hakuelekezwa vyema katika maisha na jinsi ya kukabiliana na maisha kwa mfano urithi alioupewa hili kuinua jamii yake. Wakati mmoja alijipata amebadilika na kuanza kutumia mali aliyoachiwa kwa njia inayofaa hata ingawa alikumbwa na tatizo la kujipata katika mkono mbaya wa sheria.

Kazimoto ni shujaa pwaya ambaye alijaribu kuhimili mabadiliko katika jamii na familia. Alijaribu kufuata amali na utamaduni wa jamii lakini anajikuta katika njia panda ya maisha. Elimu ya kisasa aliyoipata inamfanya kutangana na jamii zilizo mjini na kujijini kwa njia tofauti. Mitazamo tofauti na

mawazo aliyoipata kuhusu kuwepo na kutokuwepo Mungu ni kwa ajili ya elimu ya kisasa. Kazimoto anaonyesha uhusiano wake na jamii katika kijiji chao kwa kuwapa heshima na kukubali marekebisho yao katika maisha yake.

### 4.4.11 Ulevi na Anasa

Mwandishi ameweka suala la ulevi na athari zake kupitia shujaa pwaya ambaye ni mhusika mkuu katika maandhari tofauti tofauti na anapotangamana na wahusika wengine. Mwandishi anaeleza kuwa Tumaini alianza kunywa pombe kali akiwa kijijini Bugolola hata alipohamia mjini Shinyanga, aliendelea na kunywa pombe kali ambapo alikuwa kunywa katika baa moja inayoitwa *Africans' Royal Bar* .

Ulevi wa Tumaini ulizidi hadi ukaanza kuleta athari kwake na kwa wahusika wengine waliotagusana naye kwa mfano Tumaini alibadilisha na kuchezea wanawake anapokuwa mlevi na kuzini hata wakati mwingine hao wanake alipanga jinsi ya kupata pesa kutoka kwake kama vile Kristina. Ukware ulitokana na ulevi ambapo Kristina anamchukua Tumaini kwake wakati ambapo bwanake alikuwa ashatoka na ameenda. Tumaini alifumaniwa na kupigwa ambapo alipata majeraha kwa tumbo na watu wasiojulikana alipokuwa anatoka kunywa pombe. Anastasia ndiye alimuuguza majeraha kwa kumkanda kila siku na kumpikia kwani hakuweza kufanya chochote.

Biashara haramu inayofanywa na wanawake, ambapo mwandishi anaeleza kuwa wanatumia wanaume walevi kama vitega uchumi kwa mfano Tumaini. Kwa mfano. Mwandishi anaeleza kwa kutupa taswira ya wanawake wanavyovutana kwa sababu ya Tumaini kwa kuwa alikuwa na pesa. Mwanamke mmoja kwa jina Fatuma, anawashawishi wenzake na kuwaambia kuwa hakuna haja ya wao kuvutana kuhusu Tumaini kwa kuwa hawatapata kile ambacho wanataka. Wanasema kuwa ni Tumaini ndiye anauwezo wa kutoa pesa nyingi na yule mwenzio wa kuleta ushindani hataruhusiwa kupata pesa hizo pekee yake. Maneno ya hawa wanawake na wasichana yanaonyesha kuwa biashara ya kujiuza ili wapate pesa katika vyumba vya ulevi kwa hivyo ulevi umechangia biashara hii.

Kufilisika kwa Tumaini ni kwa sababu ya ulevi na kutumia pesa zake kwa wanawake akiwa vyumba vya ulevini. Alitumia mali na pesa alizoachiwa kama urithi na wazazi wake vibaya baada ya kifo cha babake na mamake. Tumaini anamwambia Kristina kuwa alipewa jina  Jingojango kwa sababu hapo zamani alikuwa na pesa si kama wakati, kumaanisha kuwa alikuwa amefilisika. Pia wanawake wengine kama Fatuma wanasema kuwa Tumaini ndiye anaweza toa pesa nyingi baada ya wao kuvutana kati kuwa ni nani atakaye faidika wakati Tumaini anatumia pesa zake kwa ulevi na anasa zingine.

Mwandishi Euphrase Kezilahabi analiweka wazi tukio hili la ulevi  kupitia shujaa pwaya ambaye ni Rosa Mistika. Mwandishi anaeleza kuwa baada ya Rosa kuwa na mvutano na Deogratias ambaye alikuwa mpenzi wake. Rosa alipopata habari kuwa Deogratias alikuwa na wapenzi wengi na kuwa alikuwa ameoa, alikereka na kuamua kuachana nayeye. Kitendo hiki cha kuwa na waasichana wengi kilimfanya awaze sana na kusababisha ulevi kwa Rosa. Aliamua kuelekea Mwanza kuenda mbali na yeye na kuingia chumba cha kuuza pombe ili awze kusahau masaibu ya mapenzi yaliyompata.

Rosa akiwa katika vyumba hivi vya kunywa pombe kuuza pombe, alinunuliwa na wanaume kwa mfano kijana mmoja aliyemuuliza kama anakunywa nini na Rosa alimjibu kuwa anakunywa ‘Tusker’. Hata hivyo akiwa  kwa bwana Thomas ambaye ni mwalimu mkuu wa Chuo cha Morogoro, wanakuywa na kulewa pamoja na Rosa kumalizia kuwa kulewa zaidi ndiposa anafanya mapenzi na. Baada ya masaibu ya mapenzi kumpata, alianza kuchumbiana na Charles katika harakati hizi, Rosa alimwambia Flora ambaye ni  dadake apitie kwake ambapo walikuwa wanaishi na charles. Baada ya kupika walikula na kisha Charles akaenda kuleta pombe ambapo Rosa ndiye aliyekuwa kunywa nyingi zaidi.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, mwandishi anaeleza ulevi wa Zakaria amabaye ni babake Rosa Mistika kuwa wa hali ya kupindukia. Zakaria alikunywa kupindukia ndio maana hawajibiki kwa mfano anapopewa pesa na Regina za usafiri wa Rosa kuelekea shuleni, anazitumia kwa ulevi. Kitendo hiki ndio kinaonyesha kiwango cha ulevi uliosababisha Zakaria kutotelekeza majukumu yake kama mzazi wa Rosa. Pia hawajibiki kuwapa binti zake mawaidha ya kuwasaidia katika kuhepa mitego ya maisha na



Mount Kenya University

kufumbua mafumbo ya maisha na kutegua vitendawili vya maisha ndiposa Rosa analegea na kushindwa kimaisha . Ulevi huu pia uliwakosesha amani Rosa, dadake na mamake wakiwa nyumbani kwani aliwapigia kelele mara tu alipoingia nyumbani kutoka ulevini. Zakaria alipokuwa anarudi nyumbani, alipiga kelele kutoka mbali na hata akiwa nyumbani alileta vurugu. Akiwa mlevi, hata apate akina Rosa na dada zake wamelala, aliwaamsha na kuwaambia waimbe na wafanye mazoezi kama wanajeshi baada ya kumwamrisha Regina kuwaamsha.

Ulevi unaozungumziwa na mwandishi kupitia shujaa pwaya, ilifanya wahusika kama vile Deogratias aliyekuwa mchumba wa Rosa Mistika na mkuu wa wilaya. Awali Deogratias alizoea kunywa pombe katika vyumba tofauti pia alitumia wanawake vile anataka baada ya ulevi. Sheria katika wilaya hii nikuwa pombe ya moshi ilipigwa marufuku kwa hivyo hakunywewa na wananchi lakini iliuzwa kisirisiri. Kwa hivyo waliovunja sheria walishikwa na kutiwa mbaroni kwa mfano Deogratias walipoenda kunywa pombe eneo la moshi na Zakaria babake Rosa Mistika, alishikwa na kutiwa korokoroni. Ulevi huu ndio mwandishi alitumia kuweka wazi usawiri wa mwanamke kupitia Rosa Mistika na Deogratias ambaye ni mkuu wa wilaya. Kupitia Rosa Mistika, wanawake wamesawiriwa kuwa vyombo vya matumizi ya kutimiza haja za mwanaume kwa mfano, Rosa alipata habari kuwa Deogratias ambaye ni mchumba wake kuwa ana wanawake wengi na huwa anawabadilisha vile anataka katika vyumba hivi vya pombe.

Utepetevu katika malezi na jamii umeonyeshwa kupitia kwa shujaa pwaya ambaye ni Rosa Mistika ambapo jamii haikuwajibika katika kumwelekeza ndiposa elimu ya maisha inamulemea. Badala ya viongozi kama vile Deogratias na  Thomas ambaye ni mkuu wa shule kusaidia kwa kuwapa mawaidha na kuweka sheria za kulinda wasichana ni kinaya kuwa wao ndio wanatumika kuharibu maisha ya wasichana. Deogratias aliwatumia hawa wasichana kutimiza haja zake za kimwili  naye Thomas anamharibu Rosa kwa pombe na pia mapenzi ya kiulaghai ilihali anajua ni mtoto wa shule. Matendo haya yanaonyesha pia matumizi mabaya ya mamlaka ya ofisi za serikali.

Mount Kenya University

Kazimoto alijipata katika anasa alipokuwa akinywa pombe. Jambo hili linadhihirika wakati ambapo Kazomoto alienda kumsalimia rafiki yake anayeitwa Kamata. Kamata alimchukua sehemu ambapo watu wakuwa wanakunywa pombe pia kulikuwa starehe zingine. Kazimoto alikuwa pombe hadi hakuwa anajitambua. Alianza kumsumbua mwanamke mmoja katika eneo hili kwa kutaka mapenzi.

> *"Ninakuhitaji wewe."*
> *"Unanihitaji mimi?"*
> *"Ndiyo."*
> *"Unanihitaji mimi vipi?" Aliuliza.*
> *"Sasa unasemaje?"*
> *"Mwanamke anahitajika kwa kitu gani?"* Uk. 53

Pombe ilimwathiri Kazimoto na kufanya aanze kufanya vitendo vya ajabu alipomwona mwanamke mmoja katika eneo lile la burudani. Marafiki na walevi wengine wanaanza kumcheka na kumwambia Kamata kumpeleka nyumbani.

**4.4.12 Ushirikina na Uchawi**

Ushirikina ni hali ya kuwa na imani katika nguvu za giza ambazo husumbua wanajamii kwa kutumia kutenda maovu. Mwandishi anaeleza kuwa ushirikina na uchawi umesababisha kugawika na kutengana kwa wanajamii.

Katika *Dunia Uwanja wa Fujo* mwandishi ameeleza suala hil kwa kutumia shujaa pwaya ambaye ni Tumaini kwa kuwa ndiye alifichua uchawi wa Mugala. Mugala aligeuza wanakijiji wengine kuwa vizuu na kuwafuga kichakani ambapo aliwatumia wakati wa usiku kutenda mambo yake ya kichawi kwa mfano Kapinga na wengine wasiojulikana na waliosemekana kupotea walipatikana wakiwa wamebadilishwa kuwa vizuu.

Maendeleo katika jamii yalirudi nyuma kwa sababu ya uchawi uliosababisha uoga, mgogoro na utengano. Mugala anasababisha uoga mvutano kijijini kwa kuwa mchawi aliyebadilisha watu kuwa vizuu kwa mfano Kasala alipoambiwa kuwa yeye na mamake anakataa na wanakijiji walitaka kumvamia lakini

akakubali kueleza kuhusu uchawi wa mamake. Wanakijiji waliishi na hofu kwani waliogopa watageuzwa kuwa na Mugala kuwa vizuu na wengine walianza kukosana kushukiwa kuwa walikuwa katika kundi la wachawi mfano ni Leonila na Kasala.

Kutengana kulitokana na uchawi ndio maana wanajamii walitenga sehemu ambayo waliitwa kisiwa cha wachawi ambapo walipeleka wachawi na wengine waliotenda maovu katika jamii. Walipelekwa mbali ili kuwatenga na wanajamii wengine ili wasije wakawasumbua tena ama kuendeleza huo uchawi. Mwandishi anasema kuwa kisiwa hicho kilijulikana kwa kuogopwa na waliopelekwa huko hawakuwai rudi na kuna upweke.

Suala la ushirikina katika *Rosa Mistika* hakuelezwa vilivyo ila mwandishi anasema kuwa baada ya kifo cha Rosa, Regina na Zakaria, wafanya kulinga na imani yao. Imani ya ilionekana kama kwa aliamini kuwa lazima maiti alindwe hata kukiwa na mvua. Kwa hivyo mvua iliponyesha, wtu waliingia ndani ya nyumba wakamwacha mtu mmoja nje kuchunga makaburi.

Ushirikiano na uchawi umesababisha uoga miongoni mwa familia na kutatiza maendeleo katika maisha kwa mfano wachawi wanapowahangaisha akina Rukia usiku kwa kuwarushia mchanga kwa nyumba wanapoingia kulala, Mzee Mafuru anamwita Kazimoto na Kabenga ili wajadiliane jinsi watakomesha vitendo vya wachawi. Kazimoto anakubali kuweka mtego hata ingawa ni salama kwa kukaa juu ya mti iliwaweze kumnasa mchawi anayejaribu kuwasumbua. Wachawi walikuwa na tabia ya kuwarushia mchanga kwa paa la nyumba na kuwagongea ukuta na milango ndiyo maana Rukia na mamake wanaogopa kulala.

#### 4.4.13 Mauaji na Ukatili

Hivi ni vitendo vya kinyamana vinavyotendwa kwa binadamu na wenzao wasiokuwa na roho za utu. Katika riwaya hizi mwandishi amelizungumzia suala hili la ukatili kwa upana ambapo pia mauaji yanatokea katika jamii hii na kusababisha uwoga kwa wanajamii.

Baada ya Kalia kujiingiza katika kitendo cha uzinifu, alipatana na kifo cha alipofumaniwa na wanakijiji alipokuwa akitenda uozo huo. Alikuwa amewahangaisha wanawake na wasichana katika kijiji ndiposa wanakijiji walishikwa na hamaki na kumwondoa uhai. Kalia pia alimtendea msichana mmoja unyama kwa kumshika kwa nguvu na kumbaka.

Wanakijiji wanamvamia mtu mmoja aliyeshukiwa kuwa ni mwizi na kupiga nakumuua bila kumhurumia. Tumaini anashuhudia kifo hiki kwani yeye ndiye aliyewaelekeza wanakjiji waliokuwa wanamkimtafuta mahali alikoelekea mwizi huyo. Anapotazamana na mwizi huyo baada ya kushikwa nakupigwa, alimwonea huruma na kujuta kwa kuwa yeye ndio amesababisha kifo chake na kuwa kama hangewaonyesha wanakijiji, hangepatana na kifo hicho.

Tumaini anavamiwa na watu wasiojulikana anapokuwa anatoka kunywa pombe, anaumizwa sana na kuachwa chini akiuguza majeraha hayo. Bahati inampata kuwa Anastsia ndiye pekee alimhuguza na kumchunga kwa kumpikia na kumsaidia kazi zingine hadi wakati alipopona. Pia anashuhudia ukatili na mauaji wakati walikuwa wametoka na Anastasia na rafiki yake kuelekea mashindano ya densi, ngoma na nyimbo za kitamaduni zilikuwa zinachezwa. Wakiwa wanatazama na kufurahia mashindano hayo, waliskia kelele na mvutano na walipofika hapo mtu mmoja alikuwa ashauliwa na chanzo cha kifo chake hakikueleweka .

Baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha ambalo liliathiri Tumaini na matajiri waliokuwa na mali, Tumaini aliingiwa na roho ya unyama. Alikasirishwa na tangazo hilo la Azimio la Arusha lililomfanya kumuua mkuu wa wilaya kwa sababu ndiye aliyetangaza tangazo hilo.

Mugala anavamiwa na wanakijiji baada ya kusemekana na Tumaini na Kasala kuwa alikuwa mchawi na ndiye wa kubadilisha watu kuwa vizuu na kuwatumia kufanya kazi zake kama vile kuenda shambani na kuchota maji. Alibururwa chini na wanakijiji huku akizomewa na kutemewa mate na kukejeliwa na watu na hata watoto wadogo.

Regina ambaye ni mamake Rosa alipata masaibu katika ndoa yake tangu aolewe na kulaumiwa na mumewe kwa mambo ya kimaumbile. Mvutano huu na mumewe ulisababishwa na kutozaa mtoto wa kiume ambaye jamii ilithamini sana. Zakaria aliporejea nyumbani kutoka ulevini, alimpiga na kama kwamba anamkumbusha hali yake ya kuzaa wasichana pekee. Mwandishi anaeleza kuwa hakuna mwanamke aliyepitia mapigo kama ya Regina.

Ukatili uliosababishwa kwa Zakaria unasikitisha wanakijiji kwa alimzoea kwa kupiga kelele zake na kuimba akiwa amelewa. Kifo chake kilimpata alipokuwa akitoka kunywa pombe, alichomwa mkuki wa kifua na akafa. Kifo hiki kilisababisha vifo vingine viliwi ambapo Regina alipatwa na mshtuko na akakata roho naye Rosa alijiua kwa kumeza vipande vya chupa alivyokuwa amesiaga.

### 4.4.14 Utamaduni wa Kiafrika na Athari za Kigeni katika Jamii

Utamaduni unahusu mila na desturi ambazo utumiwa na jamii katika kuendesha shughuli za maisha kama vile ndoa, michezo, ibada. Utamaduni wa jamii husika ndio kitumbulisho chao au ndicho kigezo cha kutafautisha na jamii nyingine. Mwandishi Euphrase Kezilahabi ameeleza utamaduni wa jamii kupitia shujaa pwaya na kuonyesha athari yake kwa wanajamii na mhusika mwenyewe.

Mwandishi anaeleza kuwa urithi unapewa mtoto wazazi wanapozeeka inafaa kuamuliwa na mwanaume ambaye ni baba kwa mfano Kipanga anaamua kumpa Tumaini urithi wote hata bila kumhusisha Muyango. Maoni ya Muyango kwa urithi huu ulipuziliwa na Kipanga ambapo alionya kuwa urithi huu wa mali unaeza mharibu na kumharibia maisha Tumaini. Utamaduni huu umeonyesha ubaguzi kwa jinsi ya kike au taasubi ya kiume.

Arusi au ndoa haingeweza kufanywa kama mwanamke alikuwa amezaa kabla ya kuolewa kulingana na utamaduni wa jamii husika. Mungere alihuzunika sana alipogundua kuwa Leonila ana mimba ambayo alishuku ni ya Tumaini, aliyekataa baada ya kuulizwa na Mungere. Tumainai alipokana mimba kuwa si yake, Mungere alihuzunika akijua kuwa maisha ya mwanawe yameharibiwa na Tumaini kitamaduni si

rahisi apate mume wa kufanya arusi. Jambo hili linathibitishwa na Mulele aliyetaka kumwoza bintiye kwa Tembo kabla hajapata mimba.

Kulipa mahari wakati wa ndoa ilikuwa ni desturi ya jamii kama njia moja ya kufidia familia na kuleta uhusiano katika familia hizo mbili. Anastasia kabla hajaolewa na Tumaini, alikuwa ashapangiwa ndoa ambapo wazazi wake walimchagulia mume ambaye ni mzee Tembo. Tembo alikuwa ashaanza kupanga kulipa mahari kwa familia ya Mulele.

Tumaini alikuwa hafai kupitia kwa dirisha kwa sababu taabu ambazo mamke, Muyango alipitia akiwa alijifungua watoto wa hapo awali. Muyango alimpa Tumaini kwa kuwa kuzaliwa kwake kulimpa familia matumaini ya kuwa na watoto kwani wa hapo awali walikufa tu wakati wanapozaliwa. Athari inayotoka kwa utamaduni wa kigeni inatokana na elimu ya kigeni ambayo wahusika wengine wanapata. Kwa mfano Tumaini anapopata elimu anabadilisha tabia zake na kuanza kutenda mabo ya kigeni kwa mfano kuwatumia wasichana.

Rosa anajifunza mambo ya kigeni ambayo yanafanya anabadilika kitabia. Malezi ya kufungiwa ambapo kutagusana na wavulana ndio yalionekana ya kitamaduni kwa Rosa. Katika chuo cha Morogoro TTC, Rosa alibadilika katika tabia baada ya kuanza kutangamana na wavulana. Hii inadhihirika wakati Rosa alipopata busu kutoka kwa Deogratias. Matendo haya yaliletwa na wageni kwa waafrika ndiposa yanapatikana mjini.

Katika riwaya ya *Kichwamaji*, mwandishi anaelza kuwa utamaduni wa kiafrika kwa kiasi ulimezwa na mabo ya kigeni kupitia kwa elimu ya kisasa. Kwa mfano katika maisha ya Kazimoto na Manase, elimu walioipata ililetea mabadiliko kimawazo na kimatendo ndio maana wanapojadili swala la kuwepo kwa Mungu au kutokuwepo kwa Mungu na swala la kifo, inaashiria kupata elimu fulani.

### 4.4.15 Unafiki

Mwandishi ametumia mhusika shujaa pwaya na wahusika wengine kuonyesha unafiki katika riwaya hii. Unafiki huu unaonekana na kuelezewa wanapojifanya kawa ni mabaya wazuri au wanatenda mambo mazuri ilihali ni mabaya kwa jamii na watu wengine.

Unafiki unaelezwa na mwandishi kupitia kupitia Tumaini hata wakati akiwa mchanga alionyesha unafiki. Tumaini akiwa mchanga, alimchoma mlezi wake kwa jicho na alipopigwa alikimbia hadi kwa mamake na kumripoti kuwa amepigwa ilihali ni yeye alikuwa amemchoma mlezi kwa jicho. Alifanya mamake amtusi na kumdharau mlezi badala ya kumkosoa Tumaini kwa kutokuwa na heshima kwa watu wazima.

Tumaini alionyesha mapenzi ya kinafiki kwa Leonila kwa kumtumia na kumchezea pamoja na wasichana wengine kijijini. Tumaini alitumia alijiona kuwa amesoma na ana mali ambayo alirithi na hivyo kuanza kuchezea wasichana kijini. Alimtumia Leonila kwa kumaliza haja zake za kimwili na hata wanapopigana na Anastasia, haimsumbui hata. Leonila anapomwambia mamake kuwa alitiwa mimba na Tumaini, Tumaini anakataa na kusema kuwa Leonila alikuwa na watu wengi na kuwa yeye ni malaya.

Kristina ni mnafiki kwa kuwa alimchukua Tumaini kwake ili wazini naye akijua kuwa mume wake hakuwepo nyumbani kwa hivyo ana huru wa kumleta mwanaume yeyote vile anataka. Tumaini alipojaribu kukataa, Kristina alimlazimisha waende kwake kuzini na kumwambia kuwa hangemleta kwake kama mume wake alikuwa nyumbani. Kwa hivyo kuzini kwa Kristina wakati mume wake hayupo, ni ishara tosha ya kuwa mnafiki ambapo alijifanya mwaminifu mbele ya mumewe ilihali anamwendea nyuma ya kivuli.

Dennis alijifanya kumpenda mume wake ilihali alikuwa na uhsiano na John rafiki yake Tumaini. Unafiki huu unatokea Tumaini na John wanapoenda kwa Dennis ambapo Dennis anaonekana kuwa na hisia ndiposa anapanga njama ya kumwita John chumbani mwake mwa kulala hili wajifungie ndani na kuzini

akijua mumewe hakuwa nyumbani. Unafiki wake ni kuwa anajifanya mwaminifu mumewe akiwa nyumbani ilihali alikuwa anazini kama hayupo.

Shujaa pwaya, Kazimoto katika riwaya ya *Kichwamaji* wametawaliwa na unafiki ambao unaathiri maisha ya wahusika wengine kwa mfano. Kazimoto aliwachezea wasichana wengine kihisia ilihali hakuwa na nia ya kuwaoa kama vile Vumilia. Vumilia alikuwa na matumaini kuwa mapenzi yake na Kazimoto yatawafikisha kilele cha kuoana. Matumaini yake yalifika mwisho aliposkia kuwa Kazimoto anapanga kumwoa Sabina nduguye Manase ndiposa akatamauka na kusema kuwa hana umuhimu katia dunia na akaamua kuenda mjini na kuolewa na Moyokonde.

Rosa akiwa shuleni anonyesha unafiki anapoulizwa na sista ataje wasichana waliokuwa wanaenda nje na wanarudi asubuhi. Alikataa kuwasema kwa kuwa hakutaka mvutano na wao na pia tabia na mabadiliko yalikuwa yameanza kuonekana kwake. Alijifanya mzuri kwa wasichana hao na kumbe pia naye ana nia ya kufanya vile wenzake wanafanya. Unafiki wake ulimwathiri kimaisha ndiposa maisha yake yanaharibika.

### 4.5 Dhima ya Shujaa Pwaya katika Riwaya za Rosa Mistika, Dunia Uwanja wa Fujo na Kichwamaji

Usawiri ni kufanya sura ya kitu kwa kutumia picha au kalamu au mashine za kutolea picha (Msokile, 1993). Usawiri ni kitendo cha kuchora sura ya kitu kutukia vifaa kama vile kalamu, penseli au chaki.(BAKIZA, 2010). Kwa hivyo usawiri ni kitendo cha kujenga au kufafanua wahusika katika kazi za fasihi.

Wamitila (2002) anaeleza wahusika kuwa ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya fasihi. Pili, wahusika ni binadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi, na ambao wana sifa ya kimadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na wanayoyatenda. Wahusika huweza kutambulishwa kupitia maelezo ya mhusika au msimulizi, msingi wa hisia, hali ya kimaadili, mazungumzo na matendo ya wahusika.

### 4.5.1. Dhima ya Shujaa pwaya katika Kuimarisha Ujumi na Umbuji wa Kazi ya Fasihi

Shujaa pwaya ametumiwa kuimarisha ujumi na umbuji wa kazi ya fasihi. Mhusika huyu ananogesha masimulizi na kuondoa ukakasi pamoja na uchapwa unaotokana na matumizi ya shujaa wa kimapokeo kama mhusika mkuu. Shujaa wa kimapokeo ni mhusika mkamilifu kihulka asiye na dosari wala mawaa kiasi cha kumfanya asiwe binadamu halisi. Matendo ya shujaa wa kimapokeo ni ya ushujaa hewa ambao si rahisi kuusadiki. Kwa kutumia shujaa pwaya kama mhusika mkuu, Kezilahabi anamdengua shujaa kimapokeo. Shujaa wa kimapokeo huenziwa kwa ukakamavu, ujasiri, mvuto na busara yake. Kwa upande mwingine shujaa pwaya wa Kezilahabi ni mtepetevu, ni mwenye kusitasita katika maamuzi na vilevile mkiukaji wa maadili. Wasomaji hujitambulisha na mhusika huyu ambaye kimsingi ni mhusika mviringo. Shujaa pwaya wa Kezilahabi ana dosari za kihulka, ana ila za kitabia, ana upungufu wa kimaadili na udhaifu wa kimaumbile. Sifa hizi zinampa taswira na mwonekano wa kiuhalisi katika jamii. Kwa kumsawiri kwa misingi hii, Kezilahabi anafanikiwa kumuumba shujaa wa kawaida ambaye msomaji anaweza kujitambulisha naye.

Mwandishi amemuumba Rosa kuwa mlevi. Rosa akiwa katika vyumba hivi vya kunywa pombe kuuza pombe, alinunuliwa na wanaume kwa mfano kijana mmoja aliyemuuliza kama anakunywa nini na Rosa akamjibu kuwa anakunywa 'Tusker'. Hata hivyoakiwa kwa bwana Thomas ambaye ni mwalimu mkuu wa Chuo cha Morogoro, wanakunywa na kulewa pamoja na Rosa kumalizia kuwa kulewa zaidi ndiposa alifanya mapenzi na. Baada ya masaibu ya mapenzi kumpata, alianza kuchumbiana na Charles katika harakati hizi, Rosa alimwambia Flora ambaye ni dadake apitie kwake ambapo walikuwa wanaishi na charles. Baada ya kupika walikula na kisha Charles akaenda kuleta pombe ambapo Rosa ndiye aliyekuwa kunywa nyingi zaidi.

Rosa ameumbwa na mwandishi kuwa anatamauka haraka. Anakata tamaa katika maisha yake pamoja na baadhi ya wahusika wengine kwa mfano anapopata habari kuwa Deogratias alikuwa na wanawake wengine, anakata tamaa na kuchukua hatua kumwacha na kuelekea Mwanza kuenda kukunywa. Akiwa



Mount Kenya University

Mwanza, anajiingiza katika ukware na ulevi ili aweze kukabiliana na kusahau mawazo kuhusu uchumba wake na Deogratias aliyemsaliti na kumlaghai kimapenzi.

Kazimoto anaonekana kuwa na hisia za utamaushi wanapokuwa wakijadili kuhusu kuwepo kwa Mungu na ni sababu gani zilizosababisha kifo. Anajiuliza maswali haya na hata utamaushi unazidi kuwatawala Kazimoto kifo kilipompata Rukia akiwa anajifungua na si kifo cha Rukia pia kifo cha mtoto wao na Sabina.

Shujaa pwaya, Kazimoto katika riwaya ya *Kichwamaji* ametawaliwa na ubinafsi ambao unaathiri maisha ya wahusika wengine kwa mfano. Kazimoto aliwachezea wasichana wengine kihisia ilihali hakuwa na nia ya kuwaoa kama vile Vumilia. Vumilia alikuwa na matumaini kuwa mapenzi yake na Kazimoto yatawafikisha kilele cha kuoana. Matumaini yake yalifika mwisho aliposkia kuwa Kazimoto anapanga kumwoa Sabina nduguye Manase ndiposa akatamauka na kusema kuwa hana umuhimu katia dunia na akaamua kuenda mjini na kuolewa na Moyokonde.

Tumaini amesawiriwa kuwa mnafiki. Tumaini akiwa mchanga, alimchoma mlezi wake kwa jicho na alipopigwa alikimbia hadi kwa mamake na kumripoti kuwa amepigwa ilihali ni yeye alikuwa amemchoma mlezi kwa jicho. Alifanya mamake amtusi na kumdharau mlezi badala ya kumkosoa Tumaini kwa kutokuwa na heshima kwa watu wazima. Tumaini alionyesha mapenzi ya kinafiki kwa Leonila kwa kumtumia na kumchezea pamoja na wasichana wengine kijijini. Tumaini alitumia alijiona kuwa amesoma na ana mali ambayo alirithi na hivyo kuanza kuchezea wasichana kijini. Alimtumia Leonila kwa kumaliza haja zake za kimwili na hata wanapopigana na Anastasia, haimsumbui hata. Leonila anapomwambia mamake kuwa alitiwa mimba na Tumaini, Tumaini anakataa na kusema kuwa Leonila alikuwa na watu wengi na kuwa yeye ni malaya.

### 4.5.2 Shujaa Pwaya Kama Mhusika Mkuu na Mwimo wa Msuko wa Riwaya

Shujaa pwaya wa Kezilahabi amepewa nafasi maarufu katika riwaya mzima. Ndiye mhusika mkuu aliyetarajia kuwa kielelezo kwa msomaji upande wa tabia na maadili. Badala yake Kezilahabi amesawiri kinyume chake. Mhusika huyu japo ni msomi na kiongozi katika jamii yake lakini pia ni mlevi, mzinifu na mkosa maadili. Shujaa pwaya katika riwaya za Kezilahabi zinazochunguzwa amesawiriwa kama muunganiko wa pande mbili zinazokinzana. Pande hizo ni zile za wema na uovu. Hali hii ni kinyume na ile inayosawiriwa katika riwaya ya kimapokeo ambayo ina wahusika bapa wanaonyeshwa upande mmoja kihulka. Shujaa wa kimapokeo anaweza ama kuwa mwema au mwovu. Kwa kutumia shujaa pwaya, Kezilahabi anafumbata pande mbili za kuhulka ndani ya mhusika mmoja. Matokeo yake ni kuwa, anajiepusha na matumizi ya wahusika wawili na wakati huohuo kudhihirisha uhalisia wa maisha katika uumbaji wa wahusika wake.

Rosa ameonyeshwa kuwa mwenye hasira. Mvutano kati ya Zakaria na Rosa baada ya Zakaria kupata habari kuhusu tabia za ukware na alipojaribu kumkanya, Rosa alipandashwa na hasira na kumrushia babake maneno. Tabia yake ilikuwa ya kuenda na mwanume yeyote kwa mfano Thomas ambaye ni mwalimu mkuu ambapo jambo hili lilimkera Zakaria na kumfanya ugomvi uliomfanya Rosa kutoa maneno makali mdomoni na kusema kuwa yeye si babake naye Zakaria akamjibu kuwa pia yeye si bintiye. Hata hivyo mwandishi amemjenga kuwa msomi na mwenye bidii katika masomo yake. Alifaulu katika masomo yake na akawa mwalimu na ni kwa sababu ya bidii yake.

Shujaa pwaya, Kazimoto ambaye ni mhusika mkuu ameumbwa kuwa msomi na mwajibikaji. Elimu aliyoipata inaleta uwajibikaji kwa Kazimoto ambapo anaamua kumchukua Rukia ambaye ni dadake ili kufadhili elimu yake. Alimpeleka kwa rafiki yake ambaye ni Manase ili aweze kuishi naye kwa muda hadi atakapo maliza masomo yake kwani alikuwa muhula wa mwisho katika masomo yake. Lakini Manase alimharibia masomo yake kwa kumtia mimba. Kitendo hiki kilimghadhabisha Kazimoto na kutaka kulipiza kisasi kwa familia ya Manase. Hata hivyo anamuumbua kuwa mkware. Kazimoto na

wahusika wengine walipotagusana kwa mfano Kazimoto na vumilia ambao hawakuwa wameona wanazini. Kitendo hiki kilitendwa mara kwa mara na Kazimoto na Vumilia hadi inafikia wakati Kalia anaanza kuwa na hisia ambazo zilimpelekea kutaka kubaka msichana aliyekuwa anachunga ng'ombe. Tegemea aliposkia kuwa Kazimoto amekuwa anatoka na vumilia, alileta ugomvi kwa mji wa Mzee Mafuru ili aweze kumwonya Kazimoto

Mwandishi amemuumba tumaini kuwa mlevi. Ulevi wa Tumaini ulizidi hadi ukaanza kuleta athari kwake na kwa wahusika wengine waliotagusana naye kwa mfano Tumaini alibadilisha na kuchezea wanawake anapokuwa mlevi na kuzini hata wakati mwingine hao wanake alipanga jinsi ya kupata pesa kutoka kwake kama vile Kristina. Hata hivyo Ukware ulitokana na ulevi ambapo Kristina anamchukua Tumaini kwake wakati ambapo bwanake alikuwa ashatoka na ameenda. Tumaini alifumaniwa na kupigwa ambapo alipata majeraha kwa tumbo na watu wasiojulikana alipokuwa anatoka kunywa pombe. Anastasia ndiye alimuuguza majeraha kwa kumkanda kila siku na kumpikia kwani hakuweza kufanya chochote.

Mwandishi amemsawiri kuwa mwenye mapenzi ya dhati. Ndoa na mapenzi ya dhati ni kwa Anastasia na mumewe Tumaini ambapo mwandishi ameonyesha Tumaini akipanga kumtorosha Anastasia kutoka kijijini kuelekea mjini Shinyango ambapo watajificha na kuishi ili wasijekujulikana na Anastasia asije akaolewa na mzee Tembo.

### 4.5.3 Nafasi ya Shujaa Pwaya katika Kukuza Sifa, Hulka na Wasifu wa Wahusika Wengine

Mbali na kwamba ndiye mhusika mkuu, shujaa pwaya ametumika na mwandishi kuweka wazi sifa za wahusika wengine katika riwaya wanapotangamana katika matendo. Kupitia kutangamana huku, sifa na umuhimu wa mhusika hujitokeza na kuwa wazi wanapoingiliana. Katika *Kichwamaji* shujaa pwaya ambaye ni Manase na Kazimoto wametumika kusawiri wahusika wengine. Unyonge wa Rukia unaojitokeza wazi Manase anapotumia nafasi yake na unyonge wa Rukia kumdhulumu kimapenzi.

Kupitia kwa Manase ndio tunapata unyama unaojijenga kwa Kazimoto kwani alimua kulipiza kizazi kwa familia ya akina Manase aliyedhulumu dadake ambapo aliamua kuwachomea nyumba yao. Kitendo hiki cha Kazimoto kilionyesha kutaka kuadhibu familia ya akina Manase kwani alikuwa analipiza kisasi ndio maana anaonekama mkatili.

Kazimoto alimfanya Nyabuso kuonekana kama mpenda anasa na mnafiki kwa kuwa alipenda kuenda kwa kunywa pombe na wanaume wengine na alijifanya anaenda kufata pombe kumbe alikuwa anatafuta wanaume na mali yao. Alipenda sana wanawake ndio maana hakutaka kujali kujua Nyabusora ni mwanamke wa aina gani kwani haja yake ni kumtumia kwa haja zake za kimwili. Pia kupitia kwa Kazimoto usawiri wa mwanamke unaonekana kupitia Nyabusora kwa mfano mwanamke alionekana kama chombo cha kutimizia haja za kimwili za mwanaume. Kazimoto alimtumia kimapenzi ya ulaghai kwani hakuwa mkewe na alichukuwa nafasi ya udhaifu wao. Mwanamke amechorwa kama mlevi na mpenda anasa, tukio hili linajiweka wazi kwa Nyabusora ambapo alipatikana katika vyumba au sehemu pombe ilikuwa inauzwa.

Mzee Kabenga ambaye ni babake Manase anasawiriwa kuwa mkware. Kitendo kinawekwa wazi kupitia Kazimoto ambapo alikuwa ashajulishwa na Kalia ambaye ni kakake kabla hajashuhudia kwa kumskia katika mji wa Tegemea. Kabenga alikuwa na mke ilihali aliend a kwa Tegemea wakati wa jioni ili asije akajulikana na watu na akatoka asubuhi na mapema. Ukware huu pia unaonekana kwa Manase ambaye alikuwa mkuu wa wilaya kwani jambo hili linadhihirika wakati ambapo Kazimoto alikuwa akitafuta kazi. Kazimoto alipata habari kuwa Manase alikuwa anabadilisha wasichana na wanawake mjini ndio maana hata alijipata katika kitendo cha kumharibia Rukia maisha yake kwa kumtia mimba. Mzee Kabenga ni mpenda amani kwani alikuwa alihusisha watu wengine kwa kuwaleta pamoja ilikusuluhisha mambo amabayo yalijaribu kuvuruga amani kijijini. Wakati ambapo wanakijiji walisumbuliwa na wachawi, Kabenga , Mafuru na wengine walikutana kwa mji wa Mafuru kutafuta njia ya kusuluhisha shida hii ya

wachawi wanaowasumbua. Kazimoto alikubali kusaidia kuwatega wachawi kwa kuwa ngoja akiwa juu mti.

Kazimoto ametumika kusawiri wanawake kama wanyonge ambapo hawana usemi wowote mbele ya wanaume, kwa mfano Rukia baada ya kudhulumiwa na Manase kimapenzi ambapo alitiwa mimba na masomo yake kuharibiwa hakuweza kufanya lolote. Tuza naye anaonekana kutokuwa na usemi mbele ya Mzee Kabenga alipoamua kuoa Tegemea kama mke wapili. Vumilia ni mmoja ya wanawake waliotumiwa na Kazimoto katika kutimiza haja zao za kimwili na kisha kutoolewa na Kazimoto.

Mwandishi ametumia Rosa Mistika kama shujaa pwaya katika kusawiri wahusika wengine katika riwaya, ambapo ametumika kuweka wazi sifa na umuhimu wao wanapotagusana. Kwa mfano Zakaria anaonekana mwajibikaji katika malezi ya watoto wake, haya yanaonekana anapowawekea watoto sheria kali ili wasije watiwa mimba mapema kabla ya kuolewa itakayotatiza masomo yao. Mwandishi anaendelea kufafanua kwa kusema kuwa Zakaria aliendelea kuchunga wasicha wake kama ng'ombe na hata baada ya kuonja utamu wa densi na busu ya Deogratias anamaka akisema kwa kejeli kuwa babake akiwa uko Ukerewe naye akiwa Usukumani anamchunga ni kama atakuja kumwoa wakati mmoja. Zakaria anasawiriwa na Rosa kuwa mlevi ambapo alitumia pesa zake za kusafiria na kulipiwa karo kwa pombe, ndio maana Regina aliamua kuanza kuuza pombe kufadhili safari na masomo ya Rosa. Zakaria pia alifika nyumbani akiwa mlevi hata wakati mwingine alikuwa anaimba kwa mbali hata mkewe anamskia akiwa mbali usiku.

Rosa Mistika amesawiri mhusika kama Charles kuwa msiri ambapo hakuambia Rosa kuwa anamchunguza ndio maana anaamua kumwacha bila kumwambia. Pia Charles alionekana kuwa mdadisi aliposikia kuwa Rosa hakuwa bikira vile alikuwa akisema, ndio maana aliamua kulala naye baada ya Rosa kunywa mvinyo kiwango cha kuwa hajitambui. Baada ya kujua kuwa si bikira alimua kumwacha na uchumba wao ukaishia hapo ndio maana Rosa alijiingiza katika hali ya usherati.

Shujaa pwaya ametumika na mwandishi kusawiri mhusika Zakaria kuwa mwenye taasubi ya kiume. Mwandishi anaeleza kuwa baada ya Zakaria kuwapiga wale vijana waliokuja kumtafuta Rosa, alimgeukia mkewe na kumlaumu na kumtusi:

> "*Mshenzi, unanizalia wasichana tu! Unaniletea taabu nyumbani. Bure tu!'' Zakaria alifoka*. (Rosa Mistika, uk 23)

Zakaria alimdharau sana Regina kwa kuwa hukuzaa mtoto wa kiume na hakumpa hata nafasi ya kuongea nyumbani kwake. Baada ya Regina kufanikiwa kuzaa mtoto wa kiume, Zakaria alifurahi na kumwambia Regina kuwa wakati huo mji ni wake na hapo ndipo alipata nafasi ya kumwambia mbele yake awache ulevi.

Kupitia kwa Rosa, mwandishi ameweza kumjenga mhusika Deogratias kuwa mkware. Ukware huu unaelezwa na mwandishi wakati ambapo Rosa alipofika mjini Mwanza, alisikia wanawake wakisema kuhusu Deogratias. Wanawake hao walisema kuwa Deogratias alipenda wanawake hasaa wasichana na alikuwa ametia wasichana wawili wa shule mimba. Waliendelea kusema kuwa alipenda sana densi ya watoto wa shule ndio maana wakati alikuwa anaenda densi kuwatafuta wasichana walio na joto. Mwandishi anazidi kumsawiri kuwa mkatili kwa mfano aliwatia wasichana wa shule mimba na kuwapa pesa za kutumia katika kuavya mimba na pia kutumia mamlaka yake na pesa za kufunga vijana walionekana na wasichana kwa kuwalipa askari.

Rosa ameweza kusawiri Regina ambaye ni mamake kuwa mwajibikaji katika malezi kwa watoto wake. Regina aliwashauri watoto wake na pia kuwatafutia na kuwatimizia mahitaji yao kwa mfano alianza kutengeneza na kuuza pombe ili aweze kufadhili masomo yao. Regina ameonekana kuwa mvumilivu katika maisha hasaa katika ndoa yake. Zakaria ambaye ni mumewe alimpigia kelele kila wakati kwa kuzaa wasichana wengi. Katika ndoa yake alipitia hali ngumu hata ulevi wa Zakaria na pia kumwachia majukumu yote katika malezi ndiposa alipoaga mwanamke mmoja anasikika akisema kuwa hakuna mwanamke aliyepitia shida kama Regina katika ndoa yake.

Tumaini ametumiwa kama shujaa pwaya ambapo amesawiri na wahusika tofauti katika riwaya anapotagusana na wao kama vile Mugala ambaye alishikwa kwa vitendo vyake vibaya vya kuwa mchawi aliyekuwa amefuga vizuu. Uchawi huu unajulikana baada ya Leonila ambaye alikuwa rafiki wa Tumaini kusema kuwa Mugala ndiye alifuga vizuu na kuwa alikuwa anamsadia tu.

Mwandishi anaendelea kumtumia Tumaini kuonyesha umuhimu wa wahusika wengine kama vile Kasala ambaye ni babake Leonila. Kasala anaonekana kuwa mtu mwenye kuwajibika katika malezi na ndoa. Anamlea Leonila, ambaye anaoneshwa kuwa na heshima ndio maana aliposema kuwa mamake ni mchawi na ndiye aliyefuga vizuu.

Shujaa pwaya, Tumaini ametumika kusawiri sifa za Leonila katika *Dunia Uwanja Wa Fujo* kwa mfano kuwa wadhaifu au wanyonge. Leonila alionekana kuwa mnyonge, hii inadhihirika wakati ambapo alikuwa anakosa babake ambaye ni Kasala alikuwa anampiga sana hadi Mugala aliingililia kumsadia. Udhaifu wake bado unaendelea kuelezwa na mwandishi anapokuwa katika uhusiano na Tumaini, anatiwa mimba na kukataliwa na Tumaini. Tumaini alikana kuwa mimba si yake na hawezi kumwoa na hivyo Leonila alibaki akilia.

Mwanamke amesawiriwa na mwandishi kupitia kwa Tumaini kuwa mpenda anasa, mlevi na mkware. Anasa hizi kwa wanawake zilionekana kwa akina Kristina ambaye walikunywa pombe na Tumaini hadi alilewa. Baada ya muda walianza kuonyesha mapenzi na Tumaini kwa *bar* kutokana na kuwa walevi wa kupindukia. Kristina alimpeleka Tumaini hadi kwa nyumba yake ili walale naye ilihali alikuwa na ameolewa. Mwanamke ameonekana kuwa adui ya mwanamke mwingine. Mwandishi anathibitisha haya kwa kutumia Hadija ambaye wamewai kuwa na uhusiano na Tumaini. Hadija walipokutana na Tumaini, alimuuliza mbona aliacha kumtembelea mbele ya Anastasia. Anazidi kumdharau na kuumiza roho ya Anastasia anamwambia Tumaini waende kwake kwa kuwa baridi imezidi. Wanawake wamesawiriwa kuwa wenye kiburi na majivuno kwa mfano Hadija. Hadija alisema mbele ya Anastasia kuwa akilala na mwanaume yeyote hakosi kurudi kwake.

Kupitia kwa Tumaini, mhusika Kapinga ambaye alikuwa babake anajengwa kuwa mtamaduni. Utamaduni wa Kapinga utatokea wakati ambapo alikuwa anaoa ambapo alifanya mila na tamaduni kwa ndoa yake. Kama mila ya jamii alikuwa atambue mkewe kutoka kwa wanawake waliokuwa wamefunikwa nyuso za na aliposhindwa alienda kwa mganga kutafuta usaidizi. Mwandishi pia amemchora Kapinga kuwa mwenye taasubi ya kiume. Taasubi ya kiume inadhihirishwa kupitia Muyango ambaye alikuwa mamake Tumaini na mkewe Kapinga. Mwandishi anaeleza kuwa Muyango alisikitika kuwa Kapinga alimrithisha Tumaini mali yote bila hata kumwachia kiasi. Muyango alimwambia Tumaini kuwa alishindwa kugeuza mawazo ya Kapinga na hivyo hawezi badilisha hata baada ya kifo chake.

### 4.5.4 Shujaa Pwaya katika Kuonyesha Uchangamano wa Jamii ya Kisasa

Jamii ya kisasa ni changamani kiasi cha kwamba mitindo ya maisha inabadilika kila siku. Uchangamano wa kimaisha huonekana pia katika usawiri wa wahusika katika kazi za fasihi. Wasomaji wa fasihi hujinasibisha na shujaa pwaya wanayemwona kama mmoja wao. Kwa kumsawiri shujaa pwaya kama mwasi, Kezilahabi anabisha mazoea ya kumsawiri shujaa kwa misingi chanya inayomwonyesha kuwa kielelezo cha uadilifu. Kezilahabi anabisha mtazamo wa kujenga jamii mpya kupitia wahusika wema pekee. Kwa njia hii, Kezilahabi anaonyesha mtanziko ulioko katika jamii kuhusu uhuru wa mtu binafsi. Kezilahabi anahoji kuwa binadamu anaweza kufuata uamuzi wake binafsi badala ya kushinikizwa na jamii kupitia kwa kaida na mikatale inayomshurutisha kutenda kwa njia fulani.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, masuala kuu kama vile mapenzi, utamaduni na tofauti katika jamii yanonyesha uchangamano uliopo katika jamii ya kisasa. Rosa alipokua, alijikuta katika maisha ambayo yanamshinda kuthibiti. Alijiingiza katika uhusiano wa kimapenzi ambao hukutimiza azimio lake la maisha ndiposa anaanza mapenzi ya kiholela. Changamoto ambazo zinamkumba zinaonyesha uchangamo uliko katika jamii ya kisasa.

Kazimoto alionyesha mabadiliko ambayo yanaleta mchakato katika jamii. Mabadiliko haya ni katika kitabia na pia kimtazamo.  Elimu ya kisasa ndio inaonyesha uchangamano katika jamii hii. Udadisi wa



Mount Kenya University

Kazimoto kuhusu maisha ambao ulionekana katik mjadala wa Kazimoto na Manase kuhusu Mungu na Kifo, ni uchangamano katika jamii. Changamoto ambazo Kazimoto alipitia kwa mfano ukosefu wa ajira, vifo na hata msongo wa mawazo inathibitisha jinsi jamii ya kisasa inakabiliana na maisha.

Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, inachunguza maisha ya shujaa pwaya katika mandhari yake ya utajiri na umaskini katika familia tofauti. Pia kuna tofauti katika tabaka lililosoma na tabaka ambalo halikupata elimu ya kisasa kupitia shujaa pwaya na wengine waliotangamana naye. Kizazi cha sasa kupitia Tumaini kinaishi kutumia mali katika anasa na starehe ambazo hazingiliani na matarajio ya jamii kwa mfano ukware, ulevi na ukatili.

### 4.5.5 Dhima ya Shujaa Pwaya katika Usawiri wa Mandhari katika riwaya

Wamitila (2002) anaeleza manadhari kuwa ni ile elementi ambayo hutufichulia wapi na lini ambapo matukio fulani yalifanyika. Mandhari ni mahali ama wakati tukio la kifasihi lilivyobuniwa na kutendeka na msanii na hivyo hufanikiwa kujenga hisia ya msomaji au msikilizaji ama mtazamaji kulingana na kazi yake ya fasihi aliyoiandaa. Manadhari ni sehemu ambayo kazi ya fasihi ilitendeka, inatendeka au itatendeka.

Mandhari ni mahali matendo au vitendo hutendeka na kutokana na vitendo hivyo, vipengele vingine vya fasihi usawirishwa kwa mfano maudhui mbalimbali na wahusika ambao wanahusiano mkubwa na mandhari. Mwandishi wa riwaya hizi teule ametumia jazanda kuumba mandhari na kuonyesha uhusiano uliopo katika mandahari hayo na vipengele vingine.

Shujaa pwaya amesawiri mandhari katika *Kichwamaji* kuwa ya malezi ambapo katika kijiji cha Mahende ndipo shujaa pwaya Kazimoto amelelewa na kukuzwa hata ingawa tabia yake ilianza kuwa na mbaya. Katika Mahende, mandhari haya yalisawiri shujaa pwaya kuwa mdadisi kwani alichunguza mzee Kabenga aliyekuwa na tabia ya ukware. Ukware huu unaonekana kwa Kalia ambaye alikuwa kijana mdogo ambaye alikuwa anajihusisha na mambo ambayo alijifunza kutoka kwa Kazimoto ambaye ni

ndugu yake. Kalia alikuwa anaiba pesa kutoka kwa Mzee Mafuru akimpelekea Tegemea ili amruhusu kulala na kufanya mapenzi naye. Mandhari haya kijiji cha Mahende yalitumika kuweka wazi matukio kama vile malezi kwa shujaa pwaya. Malezi ya Kazimoto yalikuwa ya ushirikiano kwani wanakijiji walishirikiana katika kusaidiana kwa malezi ndiposa Kazimoto anewekwa katika mikutano ya kumrekebisha. Mandhari haya yalionyesha udhaifu wa wahusika waliotegemewa katika malezi kwa kuwa wao ndio wanaharibu vijana badala kuwaelekeza kwa mfano Tegemea.

Saku ni mandhari ambapo shujaa pwaya, Kazimoto alitembea na maskani ya Kamata ambaye alikuwa rafiki yake. Mandhari wameonyesha ukatili kwa watu ambapo Kamata alitendewa unyama na watu waiojulikana. Kamata alipigwa hadi karibu kuaga dunia kwa sababu mkewe alikuwa mrembo. Mwanadishi anaeleza kuwa kuna wanaume ambao walikuwa wanamtaka Matilda ambaye ni mkewe Kamata na hawakutaka aolewe naye. Katika mandhari haya ukware unathibitishwa kupitia Kazimoto ambaye Kamata alimletea Nyabuso walale naye baadaa ya kunywa pombe.

Mwanza ni mji ambao mwandishi ametumia kuelezea matukio tofauti kupitia shujaa pwaya ambaye ni Kazimoto. Kazimoto anatumika kuleta utengano ulitokea kwa Vumilia na Tegemea baada ya kujua kuwa Kazimoto hakuwa na nia ya kumwoa na kuwa alikuwa ameoa Sabina na mamake ameolewa na Kabenga. Vumilia hakupendezwa na matukio haya, kwani alihisi upweke ikabidi kuenda Mwanza kufanya ukahaba. Kazimoto akiwa Mwanza walikutana naye na akataka awakutanishe na Tegemea. Kazimoto anaonyesha umuhimu wa mandhari haya kwa kuwa vitendo kama vile ulevi na ukahaba ulifanywa wahusika kama vile Vumilia na Kazimoto. Maskani ya Vumilia yalionyesha umaskini mwandishi anaposema kuwa nyumba yao ilikuwa imetengenezwa kwa madebe yaliyo na mashimo.

Dar es salaam ambapo ni mandhari ya elimu ambapo Kazimoto alipata elimu yake iliyomwezesha kupata kazi ya kuwa mwalimu. Pia Dar es salam ndipo Kazimoto alianza kuwa mpenda raha kwani alienda kujipa raha katika vyumba vya densi, kunywa pombe na pia wakati mwingine kutafuta wanawake au wasichana wa kufanya anasa nao. Hospitalini mahali Sabina alipelekwa kujifungua mtoto waliokuwa

wakitarajia na Kazimoto ilisawiri taasubi kiume kutoka kwa Kazimoto. Msemo wake wa kuwa alifikiria na alikuwa anatarajia mtoto wa kiume ndio inaonyesha taasubi ya kiume. Kazimoto akiwa kwake na mkewe baada ya mtoto wao kuaga kwa kuwa alikuwa na kichwa kubwa, mazungumzo yake na Sabina yanaonyesha kutamauka. Katika fikra za Kazimoto, anasema kuwa ni laana na pia anajiuliza maswali kuwapo kwa Mungu katika maisha.

Tumaini amelelewa katika kijiji cha Bugolola ambapo ushirikina ulikuwa wa juu sana, wachawi walitatiza kwa watu kwani wengine kama vile Mugala walifuga vizuu waliotumia katika uchawi wao. Tumaini aliamini kulikuwa na wachawi ndio maana anashuku Mugala kuwa mchawi na kumsema kwa Munangwe kulipotokea msuko wa watu wawili kupotea kutoka kijijni. Mandhari haya ndio yanatupa picha jinsi Tumaini anasumbuliwa na watu wasiojulikana kwa kurushiwa mchanga usiku na mlango wake kuhamishwa, ndipo anaamua kuhamia nyumba nyingine.

Wanakijiji wa Bugolola wengi walikuwa maskini sana na mwandishi anaonyesha taswira ya umaskini kupitia Tumaini anaposema kuwa, Tumaini aliachiwa urithi na wazazi baada ya kuaga na wao ndio waliojiweza katika kijiji cha Bugoloa na hivyo basi aliatamani wakati wa kurithi mali ya wazazi ufike haraka.

Lutare ni mandhari ambaye mwandishi ametumia Tumaini kusawiri na kuleta matukia kama vile utamaduni, ukatili na utengano. Tumaini walipofika Lutare, walipata makundi tofauti tofauti yakijiandaa katika mashindano ya ngoma za kitamaduni. Ngoma hizi zilichezwa kulingana na utamaduni ambapo ulikuwa unafanywa kila misimu ya miaka. Wachezaji wa sherehe hizi walijipaka masizi ya chungu, usoni na majivu mwili mzima na pia walicheza densi kulingana na midundo ya ngoma. Katika mandhari haya, vurugu inatokea ambapo watazamaji walifumukana na kuelekea mahali vurugu ilitokea. Kulikuwa na watu walioigwa rungu kwa vichwa vyao hadi vikavuja damu na kufa kwa kuwa walikuwa wezi. Sheria katika eneo hilo zilitiliwa mkazo na kila mtu katika jamii alikuwa azifuate ndio maana Tumaini anaingiwa nawasiwasi anahamia kwingine akisema kuwa hapo watu wanauawa ovyo ovyo.

Eneo la Shinyanga ni muhimu kwa sana kwa sababu mandhari haya yalibadilisha mtazamo na maisha ya shujaa pwaya. Mikutano ya kisiasa na matangazo muhimu kwa wananchi yalifanywa katika eneo hili kwa mfano Azimio la Arusha. Tangazo hili halikuchukuliwa na wepesi na shujaa pwaya kwa sababu lilimwathiri kwa njia hasi ambapo alikuwa apoteze shamba na mali ambayo alichiwa arithi na babake. Mkuu wa wilaya alitangaza azimio la Arusha ambao lilimkera Tumaini na akaamua kupanga njama ya kumuua mkuu wa wilaya. Tumaini alitiwa gerezani na kufungwa kwa kufanya ukatili ambapo alimuua mkuu wa wilaya.

Ukerewe ambapo Rosa Mistika amelelewa, ndio inatuonyesha picha wazi yake ya kuwa jasiri ambapo alimjibu Zakaria ambaye ni babake kwa kumwambia kuwa yeye si mtoto wake baada ya mvutano, haikuwa kawaida kumjibu Zakaria hasaa watoto wake kwani alikuwa mkali hadi watoto wake walikuwa wanamwogopa.

Mji wa Mwanza ni mahali Rosa alipelekwa kusoma shule ya upili, ambako alijulikana kuwa mwenye bidii na mwaminifu ndio maana akachaguliwa kuwa mkubwa wa darasa lake ma Sista John, hata ingawa hakuweza kuwasema wanafunzi wengine waliokuwa na tabia ya kutoroka nje ya shule. Tabia ya kutowasema ilionyesha kuwa msiri hadi pale ambapo alitishiwa na Sista John kuwa atafukuzwa ndipo alipowasema wenzake.

**4.6 Hitimisho**

Tumaini, Rosa na Kazimoto ni zao la ubunifu aali wa mwandishi. Hii ina maana kuwa wahusika hawa ni vielelezo vya usanifu wa hali ya juu wa mwandishi unaolenga kutimiza dhima za kisanaa anazowatwika. Katika uumbaji wao kuna ubunifu, uwazaji na ung'amuzi wa hali juu. Katika kumuumba kila mmoja wa wahusika hao watatu tunaona juhudi za kimaksudi zinazofanywa na mwandishi kufinyanga ruwaza fulani za tabia zinazoendana na wajibu anaomtwikwa kila mmoja wa wahusika hao katika riwaya.

Mount Kenya University

Mount Kenya University

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inahusu muhtasari wa utafiti, kujibu maswali ya utafiti, mchango wa uafiti na mapendekezo kuhusu kufanya utafiti zaidi. Pia sura hii ndio ya mwisho na itatathimini jumla ya utafiti, lengo kuu na maswala ya utafiti.

## 5.1 Muhtasari

Sehemu hii tumeeleza muhtasari unaohusu shujaa pwaya katika riwaya teule: *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja Wa Fujo* (1975) zilizoandikwa na mwandishi Euphrase Kezilahabi kuanzia sura ya kwanza hadi ya tano. Kila sura tumeanza kwa kutanguliza ujumbe ulioelezewa na kutoa maelezo na mijadala na kisha kuhutimisha sura husika. Sura ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla ambao unatoa maelezo kuhusu mada ya utafiti pamoja na kueleza umuhimu wa kutafiti mada hii. Katika sura hii, maelezo kuhusu taarifa za awali za utafiti ambazo ni: usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu ya kuchagua mada ya utafiti, umuhimu wa utafiti na maelezo ya istilahi muhimu.

Kufanikisha utafiti huu unaohusu shujaa pwaya, tumekita kwenye malengo matatu; kutathmini usawiri wa shujaa pwaya katika riwaya teule. Katika lengo hili, tumeangazia jinsi mwandishi amewachora au kuwasawiri shujaa pwaya katika riwaya teule. Pili ni ujumbe umuhimu unaowasilishwa na shujaa pwaya katika riwaya teule na jinsi ameathiri wahusika wengine. Mwisho ni kutathmini dhima ya shujaa pwaya katika riwaya teule ambapo ametumika katika kusawiri maandhari na pia kusawiri wahusika wengine.

Sura ya pili nayo inaeleza mambo matatu muhimu ambayo ni: mapitio ya maandishi ambapo ufafanuzi w kazi tangulizi mbalimbali zinazohusu mada na ambazo mtafiti alipitia, misingi ya nadharia na mihimili ya nadharia iliyotumiwa katika utafiti.

Nayo sura ya tatu inaeleza mbinu za utafiti ambapo imeanza kufafanua mbinu mbalimbali zinazotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti. Taarifa za utafiti zimekusanywa kwa mbinu kwa mbinu kuu tatu za ukusanyaji wa data, mbinu hizo ni pamoja na udondosi na mbinu za uteuzi wa sampuli na mbinu zilizotumika katika uchambuzi wa data za utafiti.

Katika sura ya nne, tumeeleza kuhusu uwasilishaji na uchambuzi wa data. Sura hii ndio kiini cha utafiti kwa sababu data zote zilizokusanywa maktabani na mtandaoni, zimewasilishwa na kuchambuliwa katika sehemu hii. Uchambuzi wa data za utafiti, umefanywa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo na uchambuzi. Kwa hivyo sura hii imebainisha na kujadili matokeo ya utafiti kuhusu usawiri wa shujaa pwaya.

**5.2 Hitimisho la Matokeo Muhimu**

Umuhimu wa maswali yetu ya utafiti ni kuwa yalituongoza katika utafiti na matokea kadhaa yalibainika. Matendo ya shujaa katika jamii yalisababisha kutokea kwa wapinzani ambao ni shujaa pwaya. Wapinzani hawa walipinga mambo mazuri yaliofanywa na shujaa na wakawa wamepotoka kimaadili katika jamii. Matendo ya shujaa pwaya yaliwahumiza wananchi au jamii husika. Shujaa pwaya amesawiriwa na mwandishi katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) kuwa mpenda anasa katika maandhari mbali mbali, elimu, unyanyasaji, ulevi na kifo. Katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974), shujaa pwaya ni Kazimoto ambaye ni mtoto wa mzee Mafuru na nduguye Kalia na Rukia. Mwandishi amemsawiri Kazimoto kuwa msherati, mlevi na akamtumia kulipiza kisasi kwa familia ya mzee Kabenga katika mandhari mbalimbali. Mwandishi amemtumia na kumsawiri Tumaini katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) kama msherati, mlevi. Hata hivyo shujaa pwaya ametumiwa kupitisha ujumbe muhimu kama vile; anasa, kulipiza kisasi na ulevi na malezi.

Kwa jumla utafiti huu una mchango katika taaluma ya fasihi hususani katika utanzu wa riwaya za Kiswahili. Mchango huo umebainisha usawiri wa shujaa pwaya katika riwaya teule Kiswahili: *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja Wa Fujo* (1975) ambapo ni muhimu katika fasihi

sehemu ya wahusika na uhusika wao. Pili utafiti umeweza kuwa kichocheo kwa waandishi wakongwe, pia waandishi chipukizi na wasomi wa riwaya za Kiswahili. Utachochea katika uandishi ambapo wataweza kuzingatia sehemu ambayo haijazingatiwa sana.

Tatu ni kuwa utafiti huu una mchango mkubwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kueneza na kukuza na kwa kuinua na kutumia istilahi za Kiswahili. Istilahi hizi zitapanua msamiati kwa Kiswahili kupitia kwa wasomi na pia waandishi wa fasihi. Fauku ya hayo, utafiti huu umegundua kuwa shujaa pwaya alitokana na shujaa wa jamii. Jamii zilipitia shida hasaa njaa, usalama kutokana na kuvamiwa na jamii zilizokuwa zinajulikana zina uwezo wa kushinda vita na kusababisha vifo. Katika jamii kukatokea wa kujitolea na kuokoa jamii kutoka vita na pia kutafuta njia mwafaka ya kusuluhisha shida wanazozipitia. Matendo ya shujaa yalifanya jamii kuamini. Katika jamii hapakosi wapinzani wa shujaa wanaokuwa na wivu na wanaotenda maovu katika jamii na hawa ndio shujaa pwaya. Matendo ya shujaa pwaya yametokana na maisha ya udhanaishi katika jamii. Kwa hivyo, shujaa pwaya ni mhusika muhimu katika fasihi ambapo husaidia kujenga maudhui na dhamira ya mwandishi.

### 5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Bila shaka, hakuna utafiti ambao unweza kuchukuliwa kuwa umekamilisha kila kitu katika eneo ulilolichunguza. Kwa hivyo kuna maeneo mengine ambayo hajashughulikiwa kama inavyostahili. Kwa sababu hiyo, utafiti zaidi unaweza kuitajika kutafiti shujaa pwaya katika kazi zingine za fasihi andishi kama vile shujaa pwaya katika tamthili, hadithi fupi na riwaya nyingine. Katika karne hii waandishi wengi wameandika na kujikita katika wahusika wanaopinga shujaa katika jamii, hivyo nimuhimu kutafiti kuhusu shujaa pwaya katika kazi zote za kifasihi.

Mount Kenya University

### 5.4 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Utafiti zaidi unafaa kufanywa kuhusu shujaa pwaya wa kike katika riwaya, tamthilia na hadithi fupi za kisasa. Waandishi wengi na wengine ni chipukizi, wameandika kuhusu jinsia ya kike na maisha yao. Hivyo basi kuna haja ya kufanya utafiti zaidi kuhusu shujaa pwaya wa kike.

Waandishi wengi wa kisasa wa fasihi wametumia mitindo tofauti na waandishi wa zamani ambapo wamezungumzia masuala ya kisasa yaliyotokana na athari ya teknolojia. Teknolojia imeathiri maisha na mienendo ya binadamu, hiyo haja ipo ifanyiwe utafiti katika kazi hizi za waandishi.

Mwisho ni kuwa utafiti zaidi unaweza fanywa kuhusu lugha na mtindo wa waandishi wa zamani na ukilinganishwa na wa karne ya ishirini na moja. Sababu ya kutafiti zaidi ni kuwa Kiswahili kama lugha inayokua kwa kasi ambapo mitindo na misamiati imechimbuka, hivyo kuna haja ya kuifanyia utafiti.

Mount Kenya University

# MAREJELEO


Ali Vuai Haji (2018). “Kutathmini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania

Allison, Scott T. & Greg Smith. (2015). Reel Heroes & Villains: Two Hero Experts Critique the Movies (Volume 2). Virginia: Agile Writer Press.

Buliba na wenzake (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za utafiti*. Dar es Salaam: Serengeti Educational Publisher limited.

Cohen, L. Manion, L. na Morrison, K. (2000). *Research Methods in Education*. New York: Routledge Falmer.

Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English Style*. London: Longman Group.

Enon, J. C. (1998). *Education Research, Statistics and Measurements*. Kampala: Makerere University.

Faustine Stella (2017). “Falsafa ya Waafrika na ujenzi wa mtindo wa uhalisiajabu katika riwaya za Kiswahili.” Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Gibbe, A. G. (1978). “*Dhima ya Mhakiki “, katika: Mulika.* Dar es Salaam: TUKI.

Gibbe, A. G. (1978). *“Fasihi na Jamii: Baadhi ya Washairi wa Kiswahili 1960-1977” katika. Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI. Juzuu la 48/1.

Hegel, G. W. F. (1971). *Introduction to Aesthetics.* Oxford: Clarendon.

Janicke, S.H. & A.A. Raney. (2015). Communications 40: 485-495. doi: 10.1515/commun2015-0022.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi, Nadharia, Mbinu na Matumizi.* Dar es Salaam: Daud Publishing Company.

Kairu, W.M. (2005). “Uhalisi na Mtindo wa Ken Walibora Katika Fasihi ya Watoto”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Kezilahabi, E. (1971). Rosa Mistika. Nairobi: Kenya Literature Bureau Publishers and printers Limited.

Kezilahabi, E. (1974, 2008). Kichwamaji. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Kezilahabi, E. (1975). Shaaban Robert: Mwandishi wa Riwaya. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (2006). *Utandawazi, Kiswahili na Dhana ya Wakati*. Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI 2005. Dar es Salaam: TUKI.

Kezilahabi, E. (2007). Dunia Uwanja wa Fujo. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Kezilahabi, E. (2008). Kichwamaji. Vide-Muwa Publishers.Nairobi.

King’ei, K. & Kisovi, C. N. M. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Literature Bureau.

Miza Omar Mohamed (2017). “Ulinganishi wa tabia za wahusika wakuu na dhamira katika riwaya.” Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuua Cha Huria cha Tanzania.

Mlacha, S.A.K. & J.S. Madumulla (1991). Riwaya ya Kiswahili. Dar es Salaam: DUP.

Mohochi, E. S. (2000). “Usimulizi Wa Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini,” katika *Nordic Journal of African Studies* 9 (2), uk. 49-59.

Mungai, C.I. (1999) “ Dhana ya maisha katika Novela mbili za Euphrase Kezilahabi.”Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi

Ngara, E. (1982). *Stylistics Criticism of the African Novel*. London: Heinmann.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999): Ufundishaji wa fasihi, nadharia na mbinu, Jomo Kenyatta Foundation Nairobi.

Stokes, P. & Wall, T. (2014). *Research Methods*. New York: Palgrave.

Tolstoy, L. N. (1960). *What is Art? Translated by Almyer Mande*. New York: Macmillan.

Wafula, R.N. & Njogu, K. (2007). Nadharia za uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publication Limited.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Mount Kenya University

## KIAMBATISHO I: BARUA YA IDHINI KUTIKA KWA KAMATI YA MAADILI

**Mount Kenya University**

REF: **MKU/ISERC/4213**

TO: **WESLEY ONGIGE ABAYA**

Date: 13 August 2024

REG: **MAKI/2020/67007**

Dear Sir/Madam,

**RE: SHUJAA PWAYA KATIKA RIWAYA YA KIDHANAISHI: MFANO WA RIWAYA TEULE ZA EUPHRASE KEZILAHABI**

This is to inform you that **Mount Kenya University** has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is **3009**. The approval period is **13/08/2024 - 12/08/2025.**

This approval is subject to compliance with the following requirements:

i. Only approved documents including informed consents, study instruments, MTA will be used

ii. All changes including amendments, deviations and violations are submitted for review and approval by **Mount Kenya University**

iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours of notification

iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affect the safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours

v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions

vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal

vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to **Mount Kenya University**

Yours sincerely,

MOUNT KENYA UNIVERSITY
ETHICS REVIEW COMMITTEE
P. O. Box 342 - 01000,
THIKA

**Dr. Alfred Owino, PhD**

**Chairman, Mount Kenya University ISERC**

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika.
Cell: +254 709 153 000 | +254 709 153 200
Email: info@mku.ac.ke Web: www.mku.ac.ke

## KIAMBATISHO II: KIBALI CHA UTAFITI KUTOKA NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 472668

Date of Issue: 22/August/2024

**RESEARCH LICENSE**



This is to Certify that Mr.. Wesley Ongige Abaya of Mount Kenya University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Kiambu on the topic: SHUJAA PWAYA KATIKA RIWAYA YA KIDHANAISHI: MFANO WA RIWAYA TEULE ZA EUPHRASE KEZILAHABI for the period ending : 22/August/2025.

License No: NACOSTI/P/24/39408

472668

Applicant Identification Number

Director General

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

See overleaf for conditions

# SHUJAA PWAYA KATIKA RIWAYA YA KIDHANAISHI: MFANO WA RIWAYA TEULE ZA EUPHRASE KEZILAHABI

*by* WESLEY ONGIGE ABAYA


**Submission date:** 12-Jun-2025 11:03PM (UTC+0300)

**Submission ID:** 2697795630

**File name:** WESLEY_ONGIGE_FINAL_REPORT.docx (1.96M)

**Word count:** 29227

**Character count:** 16872


Mount Kenya University

SHUJAA PWAYA KATIKA RIWAYA YA KIDHANAISHI: MFANO WA RIWAYA TEULE ZA EUPHRASE KEZILAHABI

ORIGINALITY REPORT

| 11% | 10% | 1% | 6% |
| --- | --- | --- | --- |
| SIMILARITY INDEX | INTERNET SOURCES | PUBLICATIONS | STUDENT PAPERS |

PRIMARY SOURCES

mwalimuwakiswahili.co.tz
Internet Source

1 core.ac.uk
Internet Source

www.coursehero.com
Internet Source

2 scholar.mzumbe.ac.tz
Internet Source

3 Submitted to Mount Kenya University
Student Paper

repository.udom.ac.tz 2%

4 ir-library.ku.ac.ke
Internet Source

1%

5 repository.out.ac.tz
Internet Source

1%

6 Submitted to University Der Es Salaam
Student Paper

1%

7 journals.udsm.ac.tz
Internet Source

1%

8 pseudepigraphas.blogspot.com
Internet Source

1%

9 kijuekiswahili.wordpress.com
Internet Source

<1%

10 Submitted to Eiffel Corporation
Student Paper

11

Mount Kenya University

13

28

14

15

16

17

18

19

20

21

22

23

24

25

26

27

elibrary.pu.ac.ke
Internet Source

Submitted to Pwani University
Student Paper

erepository.uonbi.ac.ke
Internet Source

manyama1.blogspot.com
Internet Source

ir-library.egerton.ac.ke
Internet Source

Submitted to University of Rwanda
Student Paper

lengaripolebahati.blogspot.com
Internet Source

Submitted to International School Moshi
Student Paper

Submitted to Kenyatta University
Student Paper

jifunzekiswahili.art.blog
Internet Source ir-

Mount Kenya University

| | | |
|---|---|---|
| libr ary | repository.suza.ac.tz:8080<br>Internet Source | <1% |
| .m ma rau | Submitted to University of Nairobi<br>Student Paper | <1% |
| .ac .ke :80 | ir.mu.ac.ke:8080<br>Internet Source | <1% |
| 80 Inter net Sourc | Submitted to The University of Dodoma<br>Student Paper | <1% |
| | | <1% |
| | | <1% |
| | | <1% |
| | | <1% |
| | | <1% |
| | | <1% |
| | | <1% |
| | | <1% |
| | | <1% |
| | | <1% |

Mount Kenya University

| | | |
|---|---|---|
| 29 | | <1% |
| 30 | www.ajol.info<br>Internet Source | <1% |
| 31 | github.com<br>Internet Source | <1% |
| 32 | opus.lib.uts.edu.au<br>Internet Source | <1% |
| 33 | zebradoc.tips<br>Internet Source | <1% |
| 34 | repository.chuka.ac.ke<br>Internet Source | <1% |
| 35 | 1library.net<br>Internet Source | <1% |
| 36 | fdocumenti.com<br>Internet Source | <1% |
| 37 | www.grafiati.com<br>Internet Source | <1% |
| 38 | Submitted to National University of Singapore<br>Student Paper | <1% |
| 39 | www.msomibora.com<br>Internet Source | <1% |
| 40 | docplayer.net<br>Internet Source | <1% |
| 41 | afribary.com<br>Internet Source | <1%<1% |
| 42 | kisiwachamaarifa.co.tz<br>Internet Sourc | <1% |
| 43 | medicine.kau.edu.saparliament.go.tInternetSourc | |

Mount Kenya University

<1 %

| | | |
|---|---|---|
| 44 | studentsrepo.um.edu.my<br>Internet Source | <1 % |
| 45 | taifaleo.nation.co.ke<br>Internet Source | <1 % |
| 46 | www.rucu.ac.tz<br>Internet Source | <1 % |
| 47 | zbook.org<br>Internet Source | <1 % |
| 48 | repository.maseno.ac.ke<br>Internet Source | |
| 49 | www.doria.fi<br>Internet Source | |
| 50 | www.magiran.com<br>Internet Source | |
| 51 | ir-library.mmust.ac.ke<br>Internet Source | |
| 52 | onlinetuit.blogspot.com<br>Internet Sourc <1 % | |

<1 %

<1 %

<1 %

<1 %

Mount Kenya University

Mount Kenya University

Exclude quotes Off Exclude bibliography Off

Mount Kenya University

Mount Kenya University